Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Nane - Tarehe 12 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

### TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Nafurahi kuona kwamba Waheshimiwa Wabunge wanadai haki yao ya kusalimiwa na Spika. Waheshimiwa Wabunge, Kikao cha leo kinaanza. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, taarifa ya leo, leo ndio siku ambapo alipangiwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulihutubia Bunge hili. Kwa ajili hiyo, baada ya tangazo fupi nitakalolitoa, nitasitisha shughuli za Bunge ili Waheshimiwa Wabunge wakapate chai, ili wawe tayari kuwa kwenye viti vyao wakati Mheshimiwa Rais atakapowasili kwenye viwanja vya Bunge ambayo ni saa 3.45. Naomba Waheshimiwa Wabunge wakati huo tuwe tumesharudi kwenye viti vyetu.

Tangazo linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati za Hesabu za Serikali, anasema: "Nakuomba Mheshimiwa Spika, uwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali kuwa watakutana leo tarehe 12 Februari, 2004 katika Ukumbi Na.133 katika Kumbi za Kamati mara baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais." Hiyo ni Kamati ya Hesabu za Serikali.

Baada ya tangazo hilo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 4.00 asubuhi hii.

*(Saa 3.02 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 4.00 asubuhi)*

*(Saa 4.00 asubuhi Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokwishawaeleza kwamba leo ndio siku iliyopangwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhutubia Bunge hili, sasa napenda kuwaarifu kwamba amekwishaingia katika majengo ya Bunge na kabla hatujamkaribisha ndani, ningependa kukumbusha kwamba jana Bunge hili lilipitisha Azimio la kumruhusu Mheshimiwa Makamu wa Rais aweze kuwa pamoja nasi siku ya leo. Nawatangazia kwamba tayari amekwishaingia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa Mheshimiwa Rais anaingia Ukumbini. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
*Mhe. Benjamin W. Mkapa alingia ndani ya ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameshaingia kwenye Ukumbi wa Bunge. Kwa niaba yenu, sasa namkaribisha ili afanye kazi iliyomleta ya kulihutubia Bunge hili. Karibu sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MHESHIMIWA BENJAMIN W. MKAPA**

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda sote tuungane kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake zilizotuweka hai tangu nilipohutubia Bunge hili Tukufu, mara ya mwisho tarehe 30 Januari, 2002 hadi leo hii. Namshukuru pia kwa afya yangu inayoimarika siku hadi siku. *(Makofi)*

Nanyi Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa salaam zenu za pole na dua kwa ajili ya afya yangu zilizowasilishwa kwangu na Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa nimelazwa hospitali kule Uswiss. *(Makofi)*

Nilipohutubia wananchi tarehe 31 Desemba, 2003, niliwaambia kuwa ningependa katika kipindi cha uongozi wangu kilichobaki, nielekeze nguvu zangu kwenye kuimarisha uendelevu wa mageuzi na mafanikio yetu na unyumbulifu wa Taifa letu kisiasa, kiuchumi na kijamii pamoja na kuweka mkazo mpya kwenye kujenga uwezo wa Watanzania kutumia fursa za kujiendeleza ambazo mafanikio yetu ya mageuzi yanaziweka mbele yao.

Niliahidi pia kuwa, *inshallah* ningetafuta fursa ya kufafanua nini hasa nilichokuwa nazungumzia. Hakuna fursa iliyo bora kwa lengo hilo kuliko hii ya kuzungumza na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Bunge hili si tu mahali ambapo Watanzania wote wanawakilishwa, bali pia ni mshirika wangu mkuu katika kutekeleza yote ninayokusudia kuyafanya. Na kwa vile nchi hii ni yetu sote kiasi kwamba hata viongozi na wafuasi wa Vyama vya Upinzani nao hufaidi matunda ya kazi za Chama Tawala na kuathirika tusipopiga hatua mbele, nimeomba viongozi hao wawe hapa kunisikiliza na ninakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kuwaalika. *(Makofi)*

Kwa heshima, naomba sasa niwatambulishe na kuwaomba wasimame ili Waheshimiwa Wabunge nao wawatambue. *(Makofi)*

*(Hapa Viongozi wa Vyama vya Upinzani waliokuwa katika Gallery walisimama na kuwasalimia Wabunge)*

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kurejea kwenye muhtasari nilioutoa kuhusu sura kuu za mwelekeo wa miezi 20 ijayo.

(i) Kuongeza kasi ya kubadili mtazamo wa Watumishi wa Umma kwenye Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ili wajue kuwa kazi yao ya msingi sasa ni kuwasaidia na kuwawezesha wananchi kujiendeleza. *(Makofi)*

(ii) Kujenga na kuimarisha uwezo Kitaifa wa udhibiti, uratibu na usimamizi wa uchumi wa soko.

(iii) Kufikiria upya haki za wanyonge wakiwemo wananchi walio katika Sekta isiyo rasmi hasa zile haki za kumiliki raslimali na mitaji ikiwemo nguvu zao na ardhi kama mbinu ya kuwawezesha kuingia katika mfumo rasmi wa uchumi wa Kitaifa. *(Makofi)*

(iv) Kuweka kipaumbele kinachostahili kwenye mauzo nje ya nchi ikiwemo kuongeza thamani yake kwa kuyasindika na kukaribisha uwekezaji kwenye viwanda vitakavyotupatia haraka uwezo wa kufanya hivyo; na

(v) Kuendelea kubainisha kero za wananchi na kuondoa vikwazo vilivyoko katika njia ya Watanzania walio tayari kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono katika kuweka kipaumbele kwenye maeneo haya na wawe wabia wa Serikali katika utekelezaji wake wa dhati. Nawaomba mambo mawili ya msingi kabisa.

Kwanza, nawaomba wazingatie wakati wote ukweli kuwa nchi yetu ni maskini na kama alivyotuasa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, tunapaswa kukimbia wakati wengine wakitembea. Kwa kweli mimi nimechoka kila mara kusikia Tanzania inaitwa moja ya nchi maskini kuliko zote. Inawezekana kuachana na fikra hiyo ya umaskini lakini sio kwa kasi yetu ya sasa. Nchi nzima ikiongozwa na Bunge hili inapaswa kubadili *gear* na tuoneshe dunia kuwa baada ya kubuni sera na mwelekeo sahihi, sasa tunachochea mwendo kweli kweli. *(Makofi)*

Sijengi hoja ya kugeuza Bunge hili kuwa muhuri wa Serikali wala sithubutu, lakini najenga hoja ya mazingira ya kibunge yanayoiwezesha Tanzania kukimbia badala ya kutembea. Najenga hoja, kwa Kiingereza ya *a sense of urgency.*

Pili, naomba katika kuzungumza na wananchi na pamoja na Uchaguzi Mkuu ujao mwakani, sisi sote tusiwape matumaini kuwa ipo Serikali yenye majibu yote na uwezo wote. Serikali ya aina hiyo haipo popote duniani. Serikali haina muujiza wa peke yake, lakini inawezekana kupata muujiza wa Kitaifa kwa kushirikiana kutafuta ufumbuzi wa matatizo kwa kujituma na kukubali wajibu wa kujiendeleza kama mtu binafsi na kama jamii. Dhana ya kwamba wajibu wa Serikali ni kutoa na wajibu wa wananchi ni kushukuru ni sawa na mbio za sakafuni mwisho wake ni ukingoni. Dhana hiyo inaweza kumpatia Mgombea kura, lakini haitatufikisha mbali kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka 42 ya Uhuru wa Tanzania Bara na miaka 40 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Tanzania imeudhatiti Uhuru wake wa kisiasa na kujenga umoja wa Kitaifa usio na shaka ambao kwa kiasi kikubwa umesaidia kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya amani na utulivu.

Katika Bara hili lenye historia ya vurugu za kisiasa na ghasia, Tanzania iliyozaliwa mwaka 1964 kwa kuunganisha nchi mbili huru, Tanganyika na Zanzibar, hadi leo hii ndio Muungano pekee wa aina hiyo unaoendelea na kuweka hai matumaini ya umoja wa Bara la Afrika. *(Makofi)*

Serikali zetu zinabadilishwa kupitia sanduku la kura kwa kuheshimu Katiba ya Taifa. Hakuna Rais, wala Mawaziri Wakuu, wala Mawaziri Viongozi Bara na Zanzibar walioachia madaraka na kisha kulazimika kuikimbia nchi hii. Wote wanaishi nasi na wanaheshimiwa. *(Makofi)*

Tanzania ni nchi ya kidemokrasia. Serikali ya Awamu ya Tatu Tanzania Bara na Awamu ya Sita Tanzania Zanzibar zimefanya kazi kubwa kuimarisha misingi ya uhuru wa raia, demokrasia, haki na usawa kwa mujibu wa Katiba. Siwezi kusema Tanzania sasa ni peponi. Pote duniani Vyama vya Upinzani vinakuwa na malalamiko na shutuma ya aina fulani dhidi ya Chama Tawala na Serikali yake. Ni mambo ya kawaida kwenye ushindani wa kisiasa. *(Makofi)*

Matatizo ya kisiasa Zanzibar kufuatia Uchaguzi Mkuu uliopita yametatuliwa kwa amani na majadiliano. Matukio ya Januari 26, 27, 2001 ambapo wenzetu na ndugu zetu walipoteza maisha yao, yamebaki kama kasoro na si hulka ya Watanzania. Ni kasoro na ni kasoro haifai kutukuzwa. Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. *(Makofi)*

Tunaandaa mfumo endelevu wa ushindani wa kisiasa ambao ni wa kistaarabu, huru na wa amani Zanzibar na Tanzania nzima. Kwetu sisi majadiliano ndio njia muafaka zaidi na ya uhakika zaidi ya kuendesha siasa huko tuendako. Kama alivyosema Mshairi mmoja maarufu Kahlil Gibran, "Tunapogeukiana na kushauriana, tunapunguza idadi ya maadui zetu." *(Makofi)*

Mimi binafsi na Chama cha Mapinduzi hatutaki uadui kwenye siasa, tuko tayari kushauriana na kuelewana na wote wenye nia njema. Utayari wetu umedhihirika kwenye mwafaka baina ya Vyama viwili Vikuu CCM na CUF uliowekwa saini tarehe 10 Oktoba, 2001 ambao umeendelea kuimarika na umechangia kwa kiasi kikubwa utulivu wa kisiasa uliopo sasa Zanzibar, kielelezo kimojawapo kikiwa

uchaguzi mdogo wa Mei, 2003. Naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kutekeleza wajibu wake chini ya mwafaka na kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi yanayoonekana wazi. *(Makofi)*

Katika miezi ijayo, tutapendekeza mabadiliko ya Katiba ambayo kwa maoni yetu yatasaidia kuimarisha demokrasia katika nchi yetu. Tutatimiza pia ahadi yetu ya kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao na tutazidi kuongeza nafasi na uwakilishi wa wanawake katika vyombo vya maamuzi. Kwa upande wa Bunge, ninakusudia idadi yao isipungue asilimia 30 ya Wabunge kabla sijaondoka madarakani. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo mawili katika siasa nchini mwetu yasiyoniridhisha. La kwanza, ni udhaifu wa Vyama vya Upinzani.

Miaka michache iliyopita nilielezea hofu hiyo kwa kofia yangu ya Urais. Lakini nikajibiwa kuwa si kazi yangu kufikiria udhaifu wa Vyama vya Upinzani. Mimi ninaamini wako Watanzania wengine walio na wasiwasi kama wangu, maana ama tunao ushindani wa kweli wa timu zinazokaribiana kwa nguvu au tunafanya mzaha. Ni nia yangu CCM iendelee kutawala daima, lakini naelewa pia faida kwa Taifa na Vyama vya Upinzani makini vinavyoweza kutuamsha tusilale usingizi na CCM ikiwa macho kwa faida ya wananchi na Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili linalonifadhaisha ni kauli za baadhi ya viongozi wa kisiasa na wanachama wao ambazo zinaonesha kutojali thamani ya amani na utulivu nchini. Wapo hata wanaothubutu kuzungumzia damu kumwagika japo sijasikia wakijitolea damu yao wenyewe hata kwa jambo jema kama vile kutunisha akiba ya damu kwenye Hospitali zetu. Pengine hakuna sifa muhimu kwa nchi yoyote kama sifa ya amani na utulivu. *(Kicheko/Makofi)*

Kiongozi au mtu anayewania uongozi lazima ajifunze kuheshimu thamani ya uhai wa raia. Inachukua muda mrefu kwa nchi kujijengea sifa ya amani na utulivu, lakini ni rahisi sana kuibomoa hasa ukipata viongozi wasiothamini uhai wa raia, walio tayari kuutumia kama ngazi ya kuingia madarakani. Katika nchi huru ya kidemokrasia hakuna uhalali wowote wa kutumia fujo na vurugu kutafuta madaraka. *(Makofi)*

Naomba sana kuwa tunapoelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa baadaye mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani, tusithubutu hata kuwazia matumizi ya fujo na vurugu na sisi Serikalini wenye dhamana ya utulivu na usalama nchini hatuwezi kuruhusu siasa za fujo na vurugu. Ni wajibu wetu Kikatiba kudumisha amani na usalama nchini kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka kuhakikisha kuwa vikwazo dhidi ya ushiriki wa wananchi kwenye utawala na maendeleo ya nchi yao vinaondolewa, maana demokrasia sio siasa tu, demokrasia ni uchumi vile vile. Kwa asiye na chakula, demokrasia ni anasa. Kwa wananchi walio wengi, demokrasia iliyo karibu nao ni Serikali za Mitaa. Kwa sababu hiyo, Serikali ilibuni na inaendelea kutekeleza mpango wa uboreshaji wa mfuko wa Serikali za Mitaa ili kuongeza uwajibikaji kwa wananchi, kutoa huduma bora zaidi na kurahisisha jitihada zao za kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, kielelezo cha utashi wa kisiasa wa kuimarisha Serikali za Mitaa ni kiasi cha fedha kinachokabidhiwa kwa Halmashauri. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana mara 24 la ruzuku ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa kutoka shilingi bilioni 12.3 mwaka 1995/1996 hadi shilingi bilioni 292 mwaka huu wa fedha. Huu ni uwezeshaji kimapato kwa Halmashauri utokanao na mafanikio ya mageuzi yetu ya uchumi. Upo pia uwezeshaji kielimu. *(Makofi)*

Mafunzo ya kuimarisha utendaji yametolewa kwa Wakuu wa Mikoa wote, baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Makatibu Wakuu wa Mikoa na viongozi wengine wengi sana wa Serikali za Mitaa mpaka wa chini kabisa. Yote hayo yanawezekana kutokana na mafanikio ya mageuzi yetu ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mafanikio hayo pia yamesaidia uwezeshaji kiutendaji. Makatibu Tarafa wote wamepewa pikipiki ili kuwawezesha kusimamia vizuri shughuli za maendeleo. Pikipiki hizo zisingepatikana kama si mageuzi ya uchumi tuliyoyafanya. Ni mafanikio ya mageuzi hayo ndio vile vile yaliyoipa Serikali uwezo wa kufuta

kodi mbalimbali zilizokuwa kero kwa wananchi kwa miaka mingi. Wanaokebehi mageuzi waulizwe, ingewezekanaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nitalitilia mkazo katika kipindi changu kilichobaki ni mabadiliko ya fikra za viongozi na watendaji wa Serikali ili kila mmoja ajue kwamba maslahi yake binafsi na maendeleo ya Wilaya au Mji unaohusika vinategemea sana mafanikio ya uwekezaji, uzalishaji, huduma na biashara. Wakati umefika sasa hata kwa Halmashauri kushindwa kuvutia wawekezaji na wafanyabiashara. Watumishi wa Umma waelewe kwamba nyakati zimebadilika na tunahitaji mbinu mpya kukabiliana na changamoto za leo na zijazo.

Ipo hadithi ya Bwana mmoja aliyekuwa anatembea barabarani, akamsimamisha mtu mmoja na kumwuliza wakati: "Saa ngapi sasa?" Mtu yule akaangalia saa yake na kumjibu: "Hivi sasa ni saa kumi." Yule Bwana aliyeuliza akakuna kichwa na kusema: "Unajua ninyi wenye saa mnanichanganya sana. Siku nzima ya leo nimekuwa nauliza watu wakati na kila mara ninapewa jibu tofauti." *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa na mimi ninawaambia Watumishi wa Umma kwamba wasiwalaumu wenye saa wala wasichanganyikiwe, ukweli ni kuwa nyakati zinabadilika haraka na majibu nayo lazima yabadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ni kama vile kila mmoja anakubali kwa wepesi kuwa uwekezaji mkubwa na biashara, mahali pake ni Dar es Salaam. Hivi leo Mkoa wa Dar es Salaam na hususan Jiji la Dar es Salaam huchangia karibu asilimia 82 ya mapato yote ya Serikali. Hali hii sio nzuri hata kidogo. Chanzo cha maendeleo ni uwekezaji, uzalishaji, huduma na biashara. Kwa kadri mambo hayo yanavyofanyika Dar es Salaam, ndivyo maendeleo yatakavyoelekea Dar es Salaam na kuzidi kuwavuta vijana toka pande zote za nchi kuja Dar es Salaam kwa matumaini kuwa huko ndiko kwenye uwekezaji na hivyo kwenye ajira na kwamba huko ndiko kwenye maendeleo na hivyo maisha bora.

Bila Halmashauri kwenye Mikoa mingine kufanya bidii kuvutia uwekezaji huko waliko, tatizo hili haliwezi kwisha hakutakuwa na usawa wa kijiografia kwenye maendeleo ya Taifa. Ndio maana nachukua fursa hii kuupongeza Mkoa wa Kilimanjaro kwa kuwa mstari wa mbele kujiandaa kuvutia wawekezaji na kuitisha Kongamano la Uwekezaji Kilimanjaro lililofanyika tarehe 14 na 15 Agosti, 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini uchumi wa soko lazima udhibitiwe kwa maslahi ya Taifa na walaji ili kuwalinda wateja na kuhakikisha kunakuwa na ushindani wa haki kwenye biashara. Serikali imeanzisha mamlaka mbalimbali za uratibu na usimamizi. Mamlaka zote hizo zina kazi kubwa na zitahitaji kuimarishwa sana katika siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla uchumi wa Tanzania umeendelea kuboreka katika miaka ya hivi karibuni kufuatia utekelezaji wa kina uliofikiwa katika marekebisho mbalimbali ya uchumi na Sekta ya Fedha. Viashiria vya mafanikio ya hivi karibuni yaliyoleta kutengemaa kwa uchumi mpana ni pamoja na kuongezeka kwa mitaji katika Sekta za Umma na Sekta Binafsi na kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni na kujenga uwezo wa kutosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa miezi saba mpaka nane hivi sasa ukilinganisha na miezi 6.3 katika mwaka 2001.

Kuanzia mwaka 1990 hadi Desemba, 2003, Kituo cha Uwekezaji *(Tanzania Investment Centre)* kimeidhinisha jumla ya miradi 2,527 inayokadiriwa kutoa nafasi za ajira 497,539. Asilimia 44 ya miradi hiyo ni ya wawekezaji wa ndani; asilimia 32 ni ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na asilimia 32 ni ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wa nje na ni asilimia 24 tu ndiyo ya wawekezaji wa nje peke yao. *(Makofi)*

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa imeendelea kuongezeka kutoka asilimia 3.3 mwaka 1997 hadi asilimia 6.2 mwaka 2002. Wastani wa ukuaji huu wa kiuchumi wa asilimia 5.6 kwa mwaka kwa miaka mitatu mfululizo, unatia moyo hasa ukilinganishwa na wastani wa ukuaji wa uchumi Barani Afrika wa asilimia 3.4 katika kipindi hicho hicho. *(Makofi)*

Kwa sababu ya ukame, inakadiriwa kuwa mwaka 2003 uchumi umekuwa kwa asilimia 5.7 na mfumuko wa bei umeongezeka kidogo kutoka wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2002 hadi asilimia 4.6 mwezi Desemba, 2003 kwamba ukame huu haukuathiri sana utulivu wa uchumi mpana. Ni ishara ya mafanikio makubwa ya mageuzi yetu ya uchumi. Tutaendeleza mageuzi hayo na tutayaimarisha ili kamwe tusirudi nyuma tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya Azimio la Arusha kusema fedha si msingi wa maendeleo ni kwa vile hatukuwa na fedha. Kwa hiyo, Azimio likasisitiza kuwa huwezi kupanga maendeleo kwa kutegemea kitu ambacho huna. Ni hoja nzito na ya haki kabisa. Lakini dunia inabadilika na mahitaji ya maendeleo hayo nayo hubadilika.

Kwenye orodha ya mambo ambayo Azimio lilituambia ni muhimu kwa maendeleo yaani ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora, napenda niongeze lingine nalo ni mitaji. Ipo mitaji ya aina nyingi. Mtaji wa Maskini ni nguvu zake. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini wakati umefika pia kutumia siasa safi na uongozi bora kuongeza upatikanaji wa mitaji ya fedha na inawezekana.

Sote tutakumbuka hali ya uchumi ilivyokuwa mwaka 1995 na wala sisemi hivyo kwa kulaumu. Nimlaumu nani wakati mimi pia nilikuwa sehemu kamili ya Serikali zilizopita, nikiwa Waziri wa miaka mingi? *(Makofi)*

Lakini ukweli ni ukweli na ukweli ni kuwa wakati ule ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa chini ya asilimia 3 kwa mwaka. Mfumuko wa bei ulikuwa karibu asilimia 30, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ndogo isiyotosha hata miezi minne ya thamani ya bidhaa na huduma kutoka nje. Serikali ilikuwa inakusanya mapato yasiyozidi wastani wa shilingi 25 bilioni kwa mwezi. Nidhamu ya matumizi ya Serikali na usimamizi wa fedha za umma ilikuwa mdogo sana. Uwajibikaji Serikalini na katika Sekta ya Umma kwa ujumla ulikuwa mdogo na Serikali ilikuwa inadaiwa kulia na kushoto, nje na ndani ya nchi.

Aidha, ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi ulikuwa hauridhishi na uwekezaji ulikuwa unasuasua. Misaada ya nje ilikuwa michache na ilipatikana kwa masharti magumu. Kweli yupo anayetaka turudi huko? Kiongozi msomi au Mwandishi wa Habari aliye makini atakosaje kulinganisha tulikotoka na tulipo leo? Ni kweli bado kuna kazi kubwa ya kufanya. Lakini hiyo si sababu ya kupuuza yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya mambo ya mwanzo yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu, ilikuwa ni kubuni Sera na mikakati itakayoongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ili Serikali iweze kuboresha huduma za uchumi na za jamii na hivyo kusaidia jitihada za kupunguza umaskini. Tuliimarisha Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na kuipa madaraka kamili ya kukusanya mapato bila kuingiliwa na Serikali.

Aidha, Serikali ilianzisha utaratibu thabiti wa majadiliano na wadau hasa walipa kodi wakubwa kuhusu sera za kodi na utawala wa ukusanyaji wa kodi. Matokeo yake leo *TRA* inakusanya wastani wa shilingi 108 bilioni kwa mwezi ikilinganishwa na shilingi 25 bilioni mwaka 1995. *(Makofi)*

Hadi mwisho wa mwezi uliopita pamoja na matatizo ya ukame, *TRA* ilikuwa imeshavuka lengo lake la miezi saba ya kwanza ya mwaka huu wa fedha kwa kukusanya shilingi 788.3 bilioni ikilinganishwa na lengo la shilingi 757.4 bilioni yaani wamevuka lengo kwa karibu shilingi 30.9 bilioni. Naomba Bunge hili liungane nami kuwapongeza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Kwa dhati kabisa viongozi na watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kazi nzuri na kuwataka waendelee mbele. Tuna kazi ya kupiga vita umaskini. Jambo la pili, lilikuwa kurejesha mahusiano mazuri na nchi wafadhili na mashirika ya fedha ya kimataifa. Leo tunapata misaada yenye thamani zaidi ya mara nne ya ile tuliyokuwa tunapata kabla ya 1996.

Aidha, Tanzania ilikuwa moja ya nchi nne za kwanza kufuzu mtihani wa kufutiwa madeni chini ya mpango wa *HIPC* jambo ambalo limetuongezea uwezo wa kutoa huduma za uchumi na za jamii. *(Makofi)*

Fedha zinazotolewa kwa sekta za kipaumbele kwenye vita dhidi ya umaskini ikiwemo Elimu, Afya, Barabara, Maji, vita dhidi ya Ukimwi na Kilimo. Sasa ni mara nne zaidi ya kiwango cha mwaka 1996. Tumeimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali na kutumia kile tu tulichonacho. Leo Tanzania ni miongoni mwa nchi maskini zinazosifiwa sana kwenye eneo hili la nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchumi mpana tulivu ni nyenzo muhimu sana ya kuvutia uwekezaji, kuchochea ukuaji wa uchumi, kupanua nafasi za ajira, kuongeza mauzo ya nje, kuongeza mapato ya Serikali na kuongeza misaada ya nje pamoja na mikopo yenye masharti nafuu. Uwezeshaji wananchi kimitaji nao unahitaji ushindani kwenye Sekta ya Fedha. Tumepiga hatua kubwa ukizingatia tulikotoka, Benki ya Biashara sasa ziko 26. Taasisi nyingine za fedha ziko 6. Kuna Kampuni za Bima zaidi 10. Tumeanzisha Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF)* unaoongezea kwenye huduma inayotolewa na mifuko iliyopo ya *PPF, NSSF* na *LAPF,* soko la mitaji limeanzishwa na linakuwa, ipo sera mpya ya mikopo midogo midogo. Umeanzishwa mfuko wa kudhamini mikopo kwa sekta za kipaumbele ambazo ni pamoja na vyama vya ushirika na kampuni zinazozalisha bidhaa maalum kwa ajili ya kuuza nje na umebuniwa mfuko wa hisa za pamoja *Unit Trust of Tanzania.* Maeneo hayo yote yana mchango mkubwa katika kukua kwa uchumi na kuwawezesha Watanzania kimtaji. Nitakazania sana eneo hili katika siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusisahau tulikotoka na wala tusione haya kujivunia mafanikio yetu. Lakini kamwe tusiridhike, maana ukweli ni kuwa bado ipo kazi kubwa mbele yetu na matatizo bado ni mengi. Lakini tumeweka msingi mzuri na hakuna sababu ya kukosa ujasiri wa kwenda mbele na kuanza kuangalia nyuma. Katika miaka michache ijayo tutaweka mkazo katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuchochea uwekezaji na ukuaji wa uchumi kwa kasi kubwa zaidi, asilimia 6 haitoshi. Tunataka kufika asilimia 8 na kuzidi hapo. Huduma za benki na vyombo vya fedha zitatakiwa kurahisisha upatikanaji mitaji na kushiriki kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Marekebisho ya Sheria ya Ardhi yatasaidia, Bajeti ya Serikali nayo itatumika kuboresha miundombinu na kuondosha vikwazo vingine vya uwekezaji na biashara. *(Makofi)*

Pili, tutatumia Bajeti ya Serikali kuchochea upatikanaji wa ajira kwa kutumia Sera za mapato na matumizi hasa kupitia mifuko ya udhamini wa mikopo kwa wawekezaji wadogo na wa kati.

Tatu, Bajeti ya Serikali pia itatumika kama kichocheo cha kuinua uzalishaji wa kilimo kwa njia za udhamini na uwezeshaji hasa kuhusu upatikanaji wa pembejeo na mbegu.

Nne, tutaendelea kuboresha usimamizi wa fedha za Serikali ili mapato yanayoongezeka kutokana na mafanikio ya mageuzi yetu yatumike kwa ufanisi katika vita dhidi ya umaskini na kuwawezesha wananchi kujiendeleza.

Tano, kwa kadri uchumi unavyokuwa na ukusanyaji kodi unavyoboreshwa tuna lengo la kuongeza mapato ya Serikali kutoka asilimia 12 ya Pato la Taifa hivi sasa hadi asilimia 15 ifikapo mwaka 2006 na asilimia 18 ifikapo mwaka 2008.

Sita, tutaanzisha mpango wa kubainisha na kutambua kisheria mitaji na raslimali za watu walio katika sekta isiyo rasmi pamoja na kubaini na kuondoa vikwazo vinavyofanya iwe vigumu kwao kuingia kwenye Sekta rasmi inayotambuliwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umaskini una sura nyingi, upo umaskini wa kukosa kauli katika masuala yanayohusu mtu na upo umaskini wa kipato miongoni mwa sura nyingine za umaskini. Nimekuwa Rais kwa zaidi ya miaka nane sasa na mambo mawili kuhusu umaskini yananitatiza sana kinadharia.

La kwanza, ni namna ya kupima umaskini. Wengi wanapenda kutumia kigezo cha mapato, tena kwa dola za Marekani kwa siku. Lakini hicho ni kigezo finyu sana na kisicho sahihi hata kidogo. Ni

kipimo kinachokazania umaskini wa kipato tu, wakati umaskini hauna sura ya mapato peke yake. Isitoshe kwa uchumi uliojikita kwenye sekta isiyo rasmi kuna uhakika gani kuwa takwimu zetu zinabeba ujumla wa mali na raslimali za jamii zetu. *(Makofi)*

Mfugaji wa Kitanzania anaweza kuwa anahama kila baada ya miezi michache, nyumba yake wala haistahili kuitwa nyumba na mfukoni hana pesa. Lakini ana ng'ombe kati ya 500 na 1,000. Halafu anaambiwa anaishi kwa chini ya dola moja kwa siku. Mimi nafikiri wakati umefika tuwe na tafsiri ya umaskini inayozingatia mazingira yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Jambo la pili linalonitatiza linahusu swali la msingi kabisa. Hivi sasa vita dhidi ya umaskini inapigwanaje? Na ni nani hasa mwenye wajibu wa msingi kupigana na umaskini. Maana huishi kusikia au kusoma kwenye vyombo vya habari kuwa Serikali haipigi vita umaskini au mageuzi hayasaidii kupiga vita umaskini.

Ninyi Waheshimiwa Wabunge ni wawakilishi halali wa wananchi. Naomba mnisikilize vizuri. Umaskini wa kauli unapigwa vita kwa kuwapa watu kauli na hilo tumejitahidi kuwa *reforms*. *(Makofi)*

Lakini umaskini wa kipato haupigwi vita kwa kuwagawia watu pesa. Mtaniwia radhi, lazima ni lazima niweke jambo hili wazi, maana utakuta mtu mzima mwenye akili timamu anauliza kote, "Kama mageuzi yamefanikiwa mbona sina pesa mfukoni?" Serikali ina mpango gani. Serikali hii haipigi vita umaskini." Mwisho wa kunukuu.

Ukweli ni kuwa anayekuahidi kuwa Serikali inaweza kukuondolea umaskini wa kipato, anakudanganya. Nchi hii haiwezi kuushinda umaskini wa kipato kwa hadaa kama hizo. Hadaa zinazowafanya wananchi wabweteke, wasijitume vya kutosha, wakingojea msaada. Serikali makini haifanyi hivyo. Yapo mambo makuu manne niliyoyaahidi kwa nyakati mbalimbali kama mkakati wa vita dhidi ya umaskini.

Kwanza, ni kuwapa watu kauli juu ya mambo yanayowagusa ikiwemo ushirikishwaji wa kidemokrasia katika kupanga, kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo, hususan ile ya kuondoa kero zao. Miradi mikubwa kama *TASAF* na *MMEM* imejengwa imara juu ya dhana hii. Kama vile vile ulivyo mpango wa kuboresha Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Pili, ni kuweka mazingira bora ya uchumi kukua na ajira kupatikana ikiwepo mazingira yanayovutia uwekezaji na kurahisisha biashara.

Tatu, ni kupeleka kiasi kikubwa zaidi cha Bajeti ya Serikali kwenye maeneo muhimu kwa vita dhidi ya umaskini ambayo tumekubaliana Kitaifa kuwa ni Elimu, Afya, Maji, Barabara za Vijijini na Ukimwi.

Nne, ni kuweka mazingira mazuri kwa wananchi kujiendeleza, ikiwemo kwa kubaini na kisha kuondoa vikwazo vyote kwa wananchi wanaotaka na walio tayari kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, nafurahi wanapojitokeza wananchi kutathmini vita dhidi ya umaskini niliyoahidi kuongoza. Lakini wafanye tathmini ya haki kwa yale niliyoahidi na niliyoyataja hapa. Haya niliyoyataja hapa ndiyo niliyoyaahidi na niko tayari kupimwa nayo. Lakini sikuahidi, wala Chama changu hakikuahidi kuweka fedha mifukoni mwa watu. Tuliahidi fursa, na fursa zinawafaa wanaozitumia, haziwezi kuwafaa wasiozitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, idadi kubwa ya Watanzania ni wakulima, wafugaji na wavuvi. Kwa hawa na kwa hali halisi ya nchi yetu, ipo njia moja tu ya uhakika ya kuwawezesha kutumia fursa za kujiendeleza katika mazingira ya uchumi wa soko. Njia hiyo ni ushirika. Pamoja na matatizo yote yaliyovisibu vyama vya ushirika bado ukombozi wa uhakika wa wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara ndogo ndogo ni umoja kupitia ushirika. Nguvu ya mnyonge ni umoja. *(Makofi)*

Sheria mpya ya ushirika inaweka mazingira mazuri ya kuimarisha ushirika na kuwapa wanachama kauli kubwa zaidi ya kidemokrasia katika uwendeshaji wa vyama vyao. Sheria hii pia itasaidia kudhibiti wizi na ubadhirifu mambo ambayo huko nyuma yalihujumu ushirika kwa kuwavunja moyo wanachama. Lakini Sera na Sheria zitakuwa na maana tu iwapo wanachama wenyewe watakuwa jasiri kudhibiti viongozi wao na mwenendo wa ushirika wao hivyo tumeanzisha mpango wa elimu ya ushirika shirikishi ili kuwajasirisha wanachama kuwapa mbinu za ujasiri amali na mbinu za kusimamia vizuri zaidi vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, mitaji nayo ni muhimu. Hali ya mitaji ya vyama vingi vya ushirika hasa vya mazao ya kilimo ni mbaya sana. Hivyo Serikali imeamua kuvisaidia na kuviwezesha vyama hivyo kimtaji kupitia utaratibu wa udhamini wa mikopo kwa mauzo ya nje *(Export Credit Guarantee Scheme)* unaoviwezesha kukopa fedha za kununulia mazao ya wakulima na kuyauza nje ya nchi. Nazishushuru benki zinazoshirikiana nasi, *CRDB* na *Kilimanjaro Cooperative Bank* na navionya vyama vya ushirika visithubutu tena kutumia mikopo hii nje ya makusudio yake na wahakikishe wanailipa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni ufumbuzi wa muda mfupi tu wa matatizo ya mitaji. Ufumbuzi wa kudumu ni kujenga uwezo wa mitaji ndani ya vyama vyenyewe, vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa ni jibu la uhakika la tatizo la mitaji. Tumeweka mkazo mkubwa sana kwenye jambo hili na mafanikio yameanza kuonekana. Katika miaka miwili na nusu tu iliyopita vyama vya akiba na mikopo vimeongezeka kwa asilimia 57. Hisa na akiba kwenye vyama hivyo zimeongezeka kwa asilimia 83 na mikopo imeongezeka kwa asilimia 117. Huu ndiyo uwezeshaji wanyonge kimitaji. Na utawanufaisha walio tayari kushirikiana na wenzao. Wasiotaka kushirikiana watabaki kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaweka mkazo pia kwenye ukaguzi ili kuhakikisha kuwa mali na fedha za vyama vya ushirika zinatumika vizuri kwa ufanisi na kwa manufaa ya wanachama badala ya manufaa binafsi ya viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo wanaouliza faida ya mageuzi yetu ya kiuchumi ni nini kwa wananchi wa kawaida. Nasema utashi wa wazi wa kisiasa wa kuwasaidia wanyonge kupitia ushirika. Mapato ya Serikali yaliongezeka na kutuwezesha kugharamia uwezeshaji kwenye ushirika na mageuzi kwenye Sekta ya fedha yaliyowezesha vyama vya ushirika kukopeshwa ni faida za wazi kwa wanyonge na uwezeshaji wao katika uchumi wa soko na utandawazi. *(Makofi)*

Lakini ili wafaidike wanyonge lazima wajiunge kwenye ushirika. Lazima wasimamie vizuri ushirika wao. Lazima wawe wajasiriamali, wabunifu na wenye kuthubutu na kujiamini. Sifa hizo zinatokana na wananchi wenyewe. Serikali haiwezi kuzishurutisha kwao. Waheshimiwa Wabunge mnayo nafasi nzuri na ni wajibu wenu kujenga sifa hizo miongoni mwa wananchi kwenye kila jimbo la uchaguzi na ni vema muwaambie ukweli huu.

Mheshimiwa Spika, unajua wasiotupenda wanadai kuwa sisi wanasiasa ni walaghai, wasiosema ukweli wote. Si sifa nzuri hata kidogo na inaweza kuwa na madhara baadaye. Siku moja basi lililojaa wanasiasa liliacha njia na kugonga mti kwenye shamba la mkulima mmoja mzee. Mzee yule akaenda kuchunguza, kisha akachimba kaburi na kuwazika wanasiasa wote. *(Kicheko)*

Siku chache baadaye akaja askari polisi, akamwuliza yule Mzee, je, wote walikufa? Mzee akajibu: "Ah!, wengine walisema hawajafa. Lakini unajua tena jinsi wanasiasa walivyo hodari wa kudanganya." *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulimwengu kupitia Umoja wa Mataifa, ulijiwekea malengo nane ya kufikiwa ifikapo mwaka 2015 ili kupunguza umaskini kwa nusu duniani yanaitwa malengo ya maendeleo ya *millennium, millennium development goals.*

Lengo la pili kwenye orodha hiyo linahusu elimu kwamba ifikapo mwaka 2015 kila mtoto wa kike na wa kiume apate elimu kamili ya msingi. Benki ya Dunia inasema ifuatavyo kuhusu lengo hilo:-

Nanukuu. “Elimu ni maendeleo, inawapa watu uwezo wa kuchagua na inawapa fursa. Inawapunguzia mizigo miwili ya umaskini na maradhi na inampa mwenye nayo kauli nzito zaidi kwenye jamii. Inafanya nchi ziwe na nguvu kazi yenye elimumwendo *(dynamic)* na raia waelewa wanaoweza kushindana na kushirikiana na wengine duniani ikifungua milango ya mafanikio ya kiuchumi na kisiasa.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana sana na kauli hiyo. Ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Tatu imeweka mkazo mkubwa sana kwenye elimu ya msingi na tukaona kuwa mwaka 2015 ni mbali mno kufikia lengo muhimu kama hili.

Tukabuni mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(MMEM)* 2002-2006, kuhakikisha lengo hili linafikiwa ifikapo mwaka 2006. Yapo mafanikio mengi ya mpango huu katika miaka yake miwili ya kwanza. Nitataja machache tu. *(Makofi)*

Na nimewaandikia viongozi wa nchi hisani waliotufadhili katika mradi huu na kuorodhesha machache haya haya. Walionijibu wameridhika sana na matumizi ya fadhila zao na wametupongeza kwa mafanikio yetu. Machache gani hayo? *(Makofi)*

Kwanza, tumefikia usawa wa kijinsia kwenye shule za msingi; pili, idadi ya wanafunzi kwenye shule za msingi imeongezeka kwa asilimia 50.

Tatu, tumeongeza uwiano wa watoto wanaoandikishwa shule kwa rika ya wanaopaswa kuwepo shuleni kutoka asilimia 77.6% mpango ulipoanza hadi 105.2% hivi sasa.

Nne, tumeongeza kiasi cha wanafunzi wanaobakia shuleni mpaka mwisho kutoka asilimia 58.8% tulipoanza hadi asilimia 88.5% hivi sasa, tano, tumejenga madarasa 31,825 na nyumba za walimu 7,530 kwa kushirikiana na wananchi na sita, tumejenga shule mpya za msingi 1,081.

Saba, walimu wapya 17,851 wameajiriwa, na 14,852 kupatiwa mafunzo ya kujenga uwezo wao wa kujiendeleza, nane, upatikanaji wa vitabu umeongezeka kutoka uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi wanane katika madarasa ya I-IV hadi kufikia 1:3, na katika madarasa ya 5-7 kutoka 1:10 hadi 1:6 na tisa, kiwango cha kufaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi kimeongezeka kutoka asilimia 22% mwaka 2000 hadi asilimia 40 mwaka 2003. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tusione kwamba *glass* imejaa nusu tuone kwamba *glass* inaendelea kujaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya *MMEM* yameonyesha usahihi wa mwelekeo ambao tunaamini ndiyo njia pekee ya kufikia malengo ya maendeleo ya milenia. Mimi ninaamini kuwa malengo hayo yatafikiwa iwapo tu kuna ushirikiano wa Kimataifa unaozingatia mambo matatu yafuatayo, ushirikiano wa Kimataifa:-

Kwanza, utashi wa kisiasa na utawala bora katika nchi maskini na pili, mipango shirikishi kwenye kila jamii.

Tatu, mazingira ya nje yanayosaidia jitihada za nchi maskini kama vile kusamehe madeni, kuongeza misaada badala ya mikopo na kutoa fursa za uwekezaji na biashara. *(Makofi)*

Haya mambo matatu ndiyo yametuwezesha kupata mafanikio yetu na kutupa matumaini kuwa malengo ya elimu ambayo dunia ilifikiri yatafikiwa mwaka 2015 sisi tutayafikia mwaka 2006 yaani miaka 9 kabla ya tarehe iliyowekwa na Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Lakini narudia kibwagizo changu. Ni mageuzi yetu ya uchumi ndiyo yaliyosaidia kukua kwa uchumi na kuongezeka kwa mapato ya Serikali na hivyo kutuwezesha kufuta ada kwenye shule za msingi. Ni mageuzi yetu ndiyo yaliyotufanya tuwe na mahusiano mazuri na wahisani na kusamehewa kiasi fulani cha madeni ya nje na kuelekeza unafuu tulioupata kwenye sekta muhimu kwenye vita dhidi ya umaskini

kama ilivyo elimu. Ni mageuzi yetu ndiyo yametufanya tuaminiwe na wahisani na kupewa misaada zaidi na mikopo ya masharti nafuu. Na ni utashi wa kisiasa uliotuwezesha kuongeza sehemu ya Bajeti ya Serikali iendayo kwenye sekta za kipaumbele kwenye vita dhidi ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi yametupa uzoefu na dhamira ya kuwa na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari utakaoongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari kutoka asilimia 22 ya waliomaliza elimu ya msingi mwaka 2003 hadi asilimia 50 ya watakaomaliza elimu hiyo mwaka 2009, tena kwa kuzingatia jinsia na mtawanyiko kijiografia ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote haya yamewezekana na yataendelea kuwezekana kutokana na mafanikio ya mageuzi yetu, ili mradi tusirudi nyuma wala kupunguza kasi. Mageuzi yanafungua milango na fursa kwa wengi, ukianzia na hawa wanaopata elimu. Baadhi yao wamefanya vizuri sana katika shule zetu za Serikali na za binafsi na kututia moyo.

Leo mbele yenu, Waheshimiwa Wabunge napenda niwatambulishe vijana wetu wanafunzi, mmoja wa kike na mwingine wa kiume, waliofanya vizuri sana kuliko wenzao wote Tanzania kwenye mitihani iliyopita ya Darasa la Saba, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita. *(Makofi)*

**SPIKA:** *Sergeant-At-Arms* fungua mlango waingie vijana aliowataja Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

*(Hapa Vijana Waliotajwa na Rais waliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Katika mtihani uliofanyika Septemba, 2003 wa kumaliza Elimu ya Msingi, binti wa Kitanzania, Mbuke Solomoka, aliyekuwa anasoma Shule ya Kanawa, Wilaya ya Shinyanga Vijijini alikuwa msichana wa kwanza. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Jitambulishe kwa kunyoosha mkono.

*(Hapa Kijana Mbuke Solomoka alinyosha mkono juu)*

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Na kijana wa Kitanzania, Kesy Fulano kutoka Shule ya Bumanji, Wilaya ya Geita, naye alikuwa wa kwanza kwa upande wa wavulana. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Kijana Kesy Fulano alinyosha mkono juu)*

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Katika mitihani wa Kidato cha Nne, uliofanyika Oktoba, 2002, binti mwingine wa Kitanzania, Sara Cheche, aliibuka cheche kweli kweli na kuwa wa kwanza kwa upande wa wasichana Tanzania nzima. *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Huyu hakuweza kufika.

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Yeye alikuwa anasoma *St. Mary,* Mazinde Juu. *(Makofi)*

Kwa upande wa wavulana, kijana wa Kitanzania, Mosses Mwizarubi, aliyekuwa anasoma Ilboru alikuwa wa kwanza. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Kijana Mosses Mwizarubi alinyosha mkono juu)*

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Katika mitihani wa kumaliza Kidato cha Sita uliofanyika mwezi Mei, 2003, binti wa Kitanzania Alice Edward kutoka *St. Mary,* Mazinde Juu alikuwa msichana wa kwanza. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Kijana Alice Edward alinyosha mkono juu)*

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Na kijana Emil Patrick, aliyekuwa anasoma Mzumbe alikuwa wa kwanza. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Kijana Emil Patrick alinyosha mkono juu)*

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Vijana hawa wanastahili pongezi zetu, naomba tuwapigie makofi wanayostahili. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Mnaweza kurudi kwenye nafasi zenu vijana. *(Makofi)*

*(Hapa Vijana Waliotajwa na Rais walitoka ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Naliomba Bunge liwatambue, maana hawa na wenzao wengi ndio tumaini la Tanzania ya kesho. *(Makofi)*

Uendelevu na ustawi wa Tanzania unawategemea hawa lazima kama wazazi na kama Taifa tuwekeze sana kwenye vijana wetu kama hawa. Dunia ijayo ni ya ushindani mkubwa sana walioelimika vizuri ndio wenye uhakika wa kuhimili ushindani huo iwe kwenye ajira au kwenye biashara.

Kwa kupitia vijana hawa, napeleka ujumbe kwa wenzao wote wa Kitanzania, ujumbe wangu ni mfupi sana tutafanya kila tuwezalo kuwapeni elimu lakini uamuzi wa kutumia elimu hiyo ni wenu. Tambueni kuwa upo mzigo mkubwa wa kuendesha nchi hii ambao unawasubiri, jiandaeni vizuri, someni kwa makini, msituangushe na zaidi sana msipate Ukimwi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya mageuzi ya uchumi yametuwezesha pia kupanua Elimu ya Juu kwa kushirikiana na sekta binafsi na mashirika ya dini. Matokeo yake, katika miaka minne iliyopita idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Ufundi, Vyuo Vikuu binafsi na Vyuo Vikuu vya Umma iliongezeka kwa asilimia 62.5. *(Makofi)*

Cha kutia moyo zaidi ni kuwa ongezeko kubwa lilikuwa ni la wanafunzi wa kike ambao wameongezeka kwa asilimia 160.7. Miaka minne tu iliyopita wanawake walikuwa asilimia 20.7 ya wanafunzi wote kwenye vyuo hivi leo wapo asilimia 33. Nawapongeza sana wanawake waliojitokeza kutafuta Elimu ya Juu maana Serikali inaweza kutoa fursa lakini uamuzi wa kutumia fursa hizo ni wa mtu binafsi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji kwa njia ya elimu ni sehemu muhimu ya mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na changamoto za utandawazi. Bado tunayo kazi kubwa ya kufanya. Lengo la Serikali ni kuwa ifikapo mwaka 2008 wawepo wanafunzi 55,000 katika Vyuo vya Ufundi, vyuo vingine vya Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Mambo matatu ni muhimu sana ili tufikie hapo. Kwanza, Bunge hili liendeleze utashi wa kisiasa wa mkakati huu. Pili, uchumi ukue kwa kasi zaidi na kuipa Serikali mapato ya kutekeleza mipango yetu na Bunge hili lichochee ukuaji huo wa uchumi. Tatu, Elimu ya Sekondari ipanuke na iboreke kupitia mpango ambao nimeuzungumzia ili tupate wahitimu bora wa kutosha kudahiliwa kwenye vyuo vyetu. *(Makofi)*

Napenda nilishukuru Bunge hili Tukufu kwa kukubali kupitisha Sheria Na.8 ya mwaka 2001 iliyoanzisha Mfuko wa Elimu ambao kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge watakumbuka una malengo matatu makuu.

Kwanza, kuhakikisha elimu yetu katika ngazi zote ni bora zaidi. Pili, kuhakikisha upo mfumo endelevu wa kugharamia elimu nchini na tatu kuhakikisha mfumo wa elimu unatoa fursa sawa kwa wote bila ubaguzi wowote. *(Makofi)*

Mfuko umeanza kazi na tayari mamlaka ya Elimu Tanzania unayousimamia umetoa shilingi 3.4 bilioni kwa Vyuo vya Ufundi na Vyuo Vikuu vya Umma Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na Vyuo Vikuu binafsi na vya Mashirika ya Dini. *(Makofi)*

Narudia, mfuko huu ni kuwezesha elimu kwa Watanzania wote bila ubaguzi. Popote Mtanzania anapopata elimu ujumla wake ni ongezeko la wasomi nchini ambayo ni hazina ya Taifa. Tutaendeleza ushirikiano huu kati ya Serikali zetu mbili ya Muungano na ya Zanzibar na taasisi binafsi za elimu nchini kwa lengo moja la kuongeza idadi na ubora wa nguvu kazi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya ni muhimu sana katika vita dhidi ya umaskini lakini ni wazi pia kuwa mafanikio yake hayategemei utashi na maamuzi ya Serikali peke yake. Hatimaye afya ya mtu ina gharama ambayo mwenyewe lazima awe tayari kuibeba. Ipo gharama ya kuzuia usiumwe kwa kula chakula bora, kwa kuweka mazingira ya pale unapoishi na kufanya kazi kuwa safi, kwa Waheshimiwa Wanasiasa kufanya mazoezi, kwa kuzuia magonjwa kwa chanjo pale palipo na chanjo au kwa kuepuka kuambukizwa magonjwa kama Ukimwi yasiyo na chanjo na kwa kuchangia gharama za matibabu. *(Makofi/Kicheko).*

Mafanikio ya mageuzi yetu na mahusiano mazuri na wahisani na sekta binafsi yote yametusaidia kuleta mabadiliko makubwa ya mfumo wa huduma za afya, ukarabati wa taasisi za afya na upatikanaji wa chanjo. Bajeti ya afya imekuwa ikiongezeka kwa miaka mitatu mfululizo. Hili nalo limewezekana kwa sababu ya mafanikio ya mageuzi yetu ya kiuchumi. Hali ya chanzo imeboreka na kufikia asilimia 83 kuzidi kiwango cha asilimia 80 ambacho Kimataifa kimekubaliwa kuwa ni kiwango kizuri. *(Makofi)*

Hivi sasa tumeanza kutoa chanjo ya *Hepatitis* ambayo imechanganywa na chanjo iliyopo ya *DPTT* bila malipo ya ziada. Hii itasaidia kuokoa maisha kati ya 20,000-25,000 yanayopotea kwa mwaka hivi sasa.

Tanzania ipo mstari wa mbele duniani katika vita dhidi ya malaria lakini tunaomba uelewa na ushirikiano wa wananchi. Tumefuta kodi kwenye vyandarua na bidhaa zinazosaidia vita dhidi ya malaria. Tumepata msaada wa Mfuko wa Kimataifa wa Kudhibiti Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria hivyo tumeweza kufidia baadhi ya gharama za vyandarua vilivyotiwa dawa ambavyo imedhihirika vinasaidia sana kupungua maambukizo ya malaria hasa kwa akina mama wajawazito na watoto wachanga. Lakini jitihada zetu hizo ni bure iwapo wananchi hawatatumia utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, duniani kote Bima ya Afya ndio kinga thabiti hasa kwa wanyonge ya kukabiliana na gharama za tiba. Kwa wananchi wa kawaida tumeanzisha Mifuko ya Afya ya Jamii. Pale ambapo Mifuko hii inafanya kazi yapo mafanikio makubwa ambayo siri yake ni ushirikiano mzuri kati ya Serikali na wananchi. Mifuko hiyo imewapunguzia mzigo na hofu wananchi na kuzipatia hospitali uwezo wa kujiendesha. Tunataka mifuko hii ianzishwe katika Wilaya zote zilizobaki katika miaka michache ijayo. *(Makofi)*

Kwa wafanyakazi wa sekta ya umma tumeanzisha Bima ya Afya ambayo huchangiwa kati ya mfanyakazi na mwajiri. Matatizo mengi ya awali kutokana na uchanga wa mfuko yamepatiwa ufumbuzi na kazi iliyo mbele yetu ni kuimarisha Mfuko huo na kuboresha taratibu zake.

Pia tumeendelea na ukarabati mkubwa wa vituo vya huduma za afya kuanzia Hospitali ya Taifa Muhimbili ambapo kazi inaendelea mpaka hospitali za Wilaya. Kwa mfano, kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi tayari tumefunga mashine za *X-Ray* na mashine nyingine katika hospitali za Wilaya, Mikoa na Rufaa. Changamoto iliyo mbele yetu ni kuvitumia vifaa hivyo vizuri na kuvitunza ili viendelee kutumika kwa miaka mingi ijayo na kuboresha uwezo wa Madaktari kutibu wagonjwa kwa usahihi na uhakika zaidi. *(Makofi)*

Pia tumeendelea na mageuzi ya Sekta ya Afya *(Heath Sector Reform),* Wilaya zote sasa zinatekeleza mageuzi hayo yanayohusu pamoja na mengine kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi katika kuamua kinachofanyika katika vituo vyetu. Hiki ni kielelezo kingine cha kuimarika kwa demokrasia kwenye eneo muhimu kama hili la vita dhidi ya umaskini. Nawasihi wananchi wachukue nafasi hii kuboresha huduma zinazotolewa kwenye vituo vya Huduma ya Afya kupitia Bodi na Kamati za Huduma za

Afya. Ningependa katika muda mfupi iwezekanavyo Bodi na Kamati hizo ziwe zimeanzishwa nchini kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Desemba, 1999, nilitangaza kuwa Ukimwi ni janga la Taifa. Niliwasihi wananchi wote, viongozi wa Serikali, siasa, dini na wa kiraia na asasi zisizokuwa za Kiserikali kuchukua hatua mpya na za ziada ili kuliandaa Taifa kupambana na Ukimwi. Zipo dalili za ongezeko la mwamko katika jamii kuhusu Ukimwi. Kila siku kuna taarifa kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu kuhusu jitihada za kudhibiti Ukimwi. Leo Ukimwi unazungumzwa kwa uwazi zaidi kuliko miaka iliyopita.

Taarifa za awali zinaonyesha dalili za kupungua kwa maambukizo ya virusi vya Ukimwi miongoni mwa wanawake wajawazito katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Ili kupata taarifa sahihi za mwelekeo wa janga hili utafiti unafanywa kujua kiwango halisi cha maambukizo ya virusi vya Ukimwi. Pamoja na ufinyu wa Bajeti, Serikali imeamua kutoa dawa za kurefusha maisha bure kwa waishio na virusi vya Ukimwi kwa kadri ya uwezo wetu na msaada wa wahisani mbalimbali. Tunashukuru wahisani wote wanaotusaidia na kushirikiana nasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya Ukimwi ni ngumu na ya muda mrefu. Inahitaji ushiriki wa kila mmoja wetu na hususan viongozi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Hatua inayofuata sasa ni kuhakikisha kila Mtanzania anaongozwa na kanuni tatu kuu za maisha zifuatazo:-

Kama hujaambukizwa hakikisha huambukizwi. Kama umeambukizwa hakikisha humwambukizi mwingine na ujitunze ili uishi muda mrefu iwezekanavyo na unyanyapaa uwe mwiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya kero za wananchi na kikwazo katika njia yao ya kujiendeleza ni maji safi na salama. Ndio maana maji ni miongoni mwa vipaumbele katika mkakati wa Taifa wa kupiga vita umaskini. Mageuzi yetu ya uchumi na usahihi wa sera zetu kwa pamoja vimesaidia kuleta mafanikio ya kutia moyo. Kwa mfano, idadi ya wakazi wa mijini wanaopata huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka asilimia 68 mwaka 1998 hadi asilimia 73 hivi sasa. Idadi ya wananchi vijijini wanaopata maji safi imeongezeka kutoka asilimia 48 mwaka 1995 hadi asilimia 53 hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yana maelezo yake. Kwanza ni utashi mkubwa kisiasa kupambana na umaskini kiashiria kimojawapo cha umaskini kikiwa kero ya maji. Pili ni usahihi na Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 1991 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002 ambayo inasisitiza ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi ya maji vijijini. *(Makofi)*

Katika utaratibu huu, miradi ya maji inamilikiwa na wananchi wenyewe na Serikali na wafadhili wanachangia nguvu zao katika utekelezaji. Kwa utaratibu huu, wananchi wengi wameanzisha Kamati na Mifuko ya Maji yenye thamani ya shilingi 1.3 bilioni. *(Makofi)*

Kwa maneno mengine, Sera hii inasema kuwa kero ya maji itamalizwa kwa ubia kati ya Serikali na wananchi. Hakuna tena wananchi kukunja mikono wakingoja Serikali au wahisani walete maji na wananchi watoe shukrani. *(Kicheko)*

Sasa ni ubia, asiyetaka ubia, anayetaka kusubiri Serikali atabakia kwenye lindi la umaskini. Kwa mijini, ubia huo ni wajibu wa kulipia huduma ya maji ili Mamlaka za Maji zijiendeshe bila kutegemea ruzuku ya Serikali na zimudu gharama za utunzaji na ukarabati wa miundo mbinu ya maji. Lakini pia tunao utaratibu wa bei nafuu kwa wenye kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuwa matunda ya Sera hii yameanza kuonekana. Makusanyo ya maduhuli ya matumizi ya maji yameongezeka mara 34 kati ya mwaka 1995 na 2003 na kuzifanya Mamlaka za Arusha, Tanga, Moshi, Mwanza, Morogoro, Mbeya, Tabora na Dodoma kujitegemea kwa gharama zote za uendeshaji na kuchangia katika ukarabati na upanuzi wa miundo mbinu yake. Lengo sasa ni kuhakikisha Mamlaka zote zinajitegemea kikamilifu ifikapo mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya tatu kwa nini tumefanikiwa ni usahihi wa, na matunda ya mageuzi yetu ya kiuchumi kama nilivyoelezea awali. Matokeo yake tumeweza kuongeza sana uwekezaji kwenye

miradi ya maji mijini na vijijini. Hadi sasa miradi ya maji safi yenye thamani ya shilingi 20.4 bilioni katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Tabora, Arusha, Kilimanjaro na Tanga na miradi yenye thamani ya shilingi 11.4 bilioni ya uondoaji maji taka katika Mikoa ya Morogoro, Tabora, Mwanza, Iringa, Arusha, Moshi na Mwanza imekamilika. Tunawashukuru sana wahisani kwenye sekta ya maji ambao ni pamoja na *KfW,* Benki ya Dunia, *European Union, African Development Bank, BADEA* na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo hadithi ya mlevi mmoja aliyepiga simu Polisi akidai wezi wameingia kwenye gari lake na kuiba kila kitu. "Wameniibia *dashboard,* usukani, *break,* redio na hata kichapuzi," akasema kwa uchungu. Lakini kabla Polisi hawajaanza uchunguzi wakapokea simu nyingine kutoka kwa mlevi yule yule. "Oh! msijali sana," akasema huku akikatishwa na kwikwi. "Kumbe niliingia kwenye kiti cha nyuma kwa bahati mbaya." *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kuwa wanaolalamikia mageuzi yetu ni wale ambao kwa bahati mbaya wanatafuta mafanikio yake mahali ambapo sipo. Naomba niwarejeshe kwenye kiti cha mbele ili leo tumalize ubishi wa iwapo mageuzi yetu ya uchumi yana faida kwa mwananchi wa kawaida au la. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kama yupo anayengoja Serikali iweke fedha mfukoni mwake huyo atasubiri sana na siku zote ataona mageuzi haya hayana faida kwake yeye binafsi na pengine atahisi anaibiwa. Lakini hili ni Bunge, Bunge la maskini na nawaomba muwe na upeo mpana zaidi ya yule anayengoja Serikali iweke fedha mkononi mwake. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa miaka mingi tumetamani na kuwania kuwaletea wananchi wa Mkoa wa Shinyanga maji kutoka Ziwa Victoria. Haikuwezekana kwa vile tulipanga kwa kutegemea fedha za wengine. Tulikazania kutafuta wahisani. Ufumbuzi umepatikana baada tu ya mageuzi yetu ya kiuchumi yaliyoongezea uwekezaji nchini, yaliyofufua uzalishaji na huduma na yaliyoongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Matokeo yake juzi hapa hapa Dodoma umetiwa saini mkataba wa ujenzi wa awamu ya kwanza ya mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya miji ya Kahama na Shinyanga. Ujenzi utaanza mwezi Mei, 2004 na awamu ya kwanza imepangwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2005. Gharama kwa awamu zote za mradi ni shilingi 85.1 bilioni ambazo zitakuwa fedha zetu wenyewe. *(Makofi)*

Sasa mimi nauliza ninaposema anayedai mageuzi ya uchumi hayana faida kwa wananchi wa kawaida kafumba macho, ninakosea? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie kidogo tatizo la maji Jijini Dar es Salaam na ufumbuzi wake kama kielelezo kingine cha usahihi wa sera zetu na mafanikio ya mageuzi yetu ya kiuchumi. Sisi wote hapa ni viongozi, zipo sifa za kiongozi bora, upeo mpana, uwezo wa kupima na kuamua, ujasiri wa kutenda na zipo sifa za kiongozi asiye bora, upeo finyu, uwezo mdogo wa kupima na kuamua na woga na mashaka katika kutenda. *(Kicheko)*

Mimi ni muwazi na mkweli, naomba Bunge hili Tukufu, Bunge ambalo ni tumaini la Watanzania liniunge mkono ili kwa pamoja tuwe na upeo mpana zaidi tuimarishe zaidi uwezo wetu wa kupima na kuamua na hasa tuwe jasiri zaidi kwa vitendo. Kubabaika hata pale ambapo sera ni nzuri eti kwa vile kuna vikwazo au mapungufu madogo hapa na pale huleta picha ya watu na viongozi ambao hawajaamua kwa dhati wanakwenda hatua mbele na hatua nyuma.

Uamuzi wa kubinafsisha huduma za maji safi na maji taka Jijini Dar es Salaam haukuwa rahisi hata kidogo. Lakini ilibidi tuamue baada ya kupima faida na hasara zake. Cha kushangaza ni kuwa hata kabla ya miezi sita ya ukodishaji huo haijaisha wapo wanaoanza kukosa subira wakitaka matatizo yaishe mara moja, haiwezekani. Matatizo haya tumekaa nayo, tumeyalea kwa miaka chungu nzima tunathubutuje kutaka *City Water* iyamalize katika miezi sita?

Ukodishaji huo umeiwezesha Serikali kupata mkopo wa shilingi 164.6 bilioni kutoka Benki ya Dunia *(IDA),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Benki ya Rasilimali ya Ulaya *(AfDB).* Mkopo huo utatumika kuboresha huduma ya maji Jijini Dar es Salaam pamoja na maeneo ya Kibaha na Bagamoyo.

Kazi ya kukarabati mifumo ya maji safi na uondoaji maji taka inatarajiwa kuanza hivi karibuni. Ukarabati muhimu na wa haraka wa mitambo ya maji na mabomba ya maji yaletayo maji Jijini umeanza na ukarabati mkubwa wa mitambo ya kusafisha maji ya Mtoni, Ruvu Juu na Ruvu Chini inatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2004 na kazi nyingine nyingi zitaanza mwaka huu huu. *(Makofi)*

Baada ya kazi hizi kukamilika huduma ya maji safi na uondoaji maji taka katika Jiji la Dar es Salaam itaboreshwa kwa kiasi kikubwa na muhimu zaidi uwekezaji katika kuboresha huduma ya maji hautategemea tena fedha kutoka Serikalini bali itakuwa ni mapato yanayotokana na huduma yenyewe. Maana kila huduma ina gharama yake inayopaswa kubebwa na anayeitumia isipokuwa kwa wasiojiweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka kumi iliyopita kilimo kimekuwa kikikua kwa wastani wa asilimia 3.1 kwa mwaka ikilinganishwa na ukuaji wa idadi ya watu unaokisiwa kuwa asilimia 2.9 kwa mwaka katika kipindi hicho. Ukuaji huu wa kilimo bado ni mdogo sana na hautawezesha kuondoa umaskini na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Ndio maana tumeweka mkazo mpya kwenye kilimo. Mwaka 2002 kilimo kilikua kwa asilimia tano mwaka huu tulitarajia tufike asilimia sita lakini kutokana na ukame unaoendelea kuikumba nchi yetu lengo hili halitafikiwa.

Kati ya miaka miwili iliyopita uzalishaji wa pamba, tumbaku, sukari, mkonge, chai na pareto umeongezeka. Lakini uzalishaji wa korosho na kahawa ulishuka kutokana na wakulima kukosa fedha za kununulia pembejeo baada ya bei za mazao hayo kushuka. *(Makofi)*

Eneo lililolimwa maua limeongezeka zaidi ya mara tatu tangu 1995 hadi leo na vikonyo vya maua vilivyouzwa nje vimeongezeka zaidi ya mara nne. Serikali imehamasisha sekta binafsi ambayo imeanza kuuza matunda na mboga mboga mbalimbali nje ya nchi.

Ubinafsishaji na uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya biashara hususan chai na sukari umeonyesha mafanikio. Uzalishaji sukari umeongezeka mara mbili tangu 1998. Kiwanda cha Sukari cha Kagera kitaanza tena uzalishaji msimu wa 2003/2004 na kinatarajia kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka wa kwanza. Kufufuliwa kwa viwanda vya sukari kumeongeza ajira na mapato ya Watanzania na kuwezesha wakulima wengi kuingia katika kilimo cha mkataba *(out-growers).* Kama yupo asiyekuwa na uhakika wa faida za ubinafsishaji akawaulize wakulima wadogo wa mkataba *(out-growers)* jirani na viwanda vya sukari vya Mtibwa, Kilombero na baadaye mwaka huu Kagera. *(Makofi)*

Serikali katika Awamu ya Tatu imeongeza uwekezaji katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani hususan katika ujenzi na ukarabati wa scheme ndogo za umwagiliaji maji mashamba.

Narudia, wanaodhani Serikali haikazanii kilimo cha umwagiliaji, wanisikilize vizuri. Tangu mwaka 2002/2003, mwaka juzi, jumla ya shilingi 3.16 bilioni zimetumika katika miradi ya umwagiliaji maji mashambani. Ifikapo Juni, 2004 eneo litakalokuwa limeendelezwa kwa umwagiliaji litafikia zaidi ya hekta 230,000. *(Makofi)*

Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA)* imekamilisha maandalizi ya sehemu ya kwanza ya mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Uchunguzi uliofanywa umeonyesha kwamba kuna hekta milioni 2.3 zenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa. Kwa jumla, Taifa lina hekta milioni 29.4 zinazofaa kuendelezwa kwa umwagiliaji maji mashambani.

Wakulima wanaoshiriki katika *scheme* ndogo za umwagiliaji sasa wanaweza kulima eneo moja hadi mara tatu kwa mwaka na uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 kwa hekta moja mpaka tani 5 kwa hekta na unatarajiwa kuongezeka hadi tani 6-8. Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuingiza nchini zana bora kwa ajili ya kuendeleza kilimo. Hatua hii ilichangia kuingiza

matrekta 1080 kati ya mwaka 2001-2003 ikilinganishwa na matrekta 50 yaliyoingizwa nchini mwaka 1999-2000.

Aidha, mwaka 1999-2000 yaliingizwa matrekta madogo ya mkono 60 yaliyouzwa kwa bei nafuu na kwa mkopo. Serikali inaendelea kutoa mikopo ya kukarabati matrekta machakavu na kununua matrekta mapya. Mpaka sasa waombaji 272 wamepitishiwa maombi yao. *(Makofi)*

Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa vituo vyake 17 vya utafiti wa kilimo kati ya 22 uliohusu maabara, ofisi, nyumba za watumishi na miundo mbinu ya mashamba ya majaribio. Aidha, vituo vyote 22 vimepatiwa vitendea kazi kama vile magari, matrekta, pikipiki na kompyuta. Jumla ya wataalam 97 kati ya wataalam 350 wamepatiwa mafunzo ya Shahada za Juu *(MSc* na *Ph.D)* katika kipindi hiki na hivyo kuwaimarisha kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, narudia utashi wa kisiasa wa Serikali hii kukuza kilimo ni mkubwa na yote yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika yanawezekana kutokana na mafanikio ya mageuzi ya uchumi nchini. Hatuna muujiza wa kumaliza matatizo yote siku moja lakini usahihi wa sera na mwelekeo wetu upo dhahiri sambamba na utashi wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji ni sehemu ya mageuzi ya uchumi tunayoyafanya na ambayo yanatoa fursa kwa Watanzania kujiendeleza na kumiliki uchumi wa Taifa lao.

Ningependa nitumie mfano wa ubinafsishaji wa mashamba makubwa ya mifugo na *Ranch* za Taifa kuelezea dhana hii na jitihada za Serikali kuwawezesha wananchi kutumia fursa hii. Mwezi Februari, 2002, Serikali kwa makusudi iliamua kuwa ubinafsishaji wa mashamba makubwa ya mifugo na *Ranch* za Taifa utumike kuwawezesha Watanzania kuingia kwenye ufugaji wa kisasa, ufugaji wa kibiashara. Katika mkakati huo *Ranch* saba za *NARCO* ambazo ni *Kikulula Complex,* Kitengule, Mkata, Missenyi, Kalambo, *West Kilimanjaro* na Mzeri, kila moja itatenga eneo la hekta 20,000 ambalo litaendelezwa kama *Ranch* ya mfano chini ya *NARCO.* Maeneo ya *Ranch* hizi yanayobaki pamoja na maeneo yote ya ranch za Usangu na Uvinza yatagawanywa katika maeneo ya *Ranch* ndogo za ukubwa wa hekta 2,000 kila moja ambazo zitamilikishwa Watanzania wenye nia na uwezo wa kufuga kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, *Ranch* za Kongwa na Ruvu zitabaki kuwa maeneo yasiyo na magonjwa ili kuiwezesha nchi yetu kuwa na mifugo inayokubalika kwenye soko la nje. Utaratibu wa kugawa *Ranch* ambao utakamilika mwezi Juni mwaka huu utahusisha jumla ya hekta 400,000 ambazo zitagawanywa ili kupata ranch ndogo zipatazo 100 zitakazoendelezwa na wawekezaji binafsi wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mashamba ya ng'ombe wa maziwa ya Serikali yaliyokuwa chini ya *DAFCO* nayo yaliingizwa kwenye utaratibu huu wa kubinafsishwa kwa wananchi. Hadi sasa mashamba yaliyobinafsishwa kwa wawekezaji wananchi ni Utegi (Tarime), Ruvu (Pwani), Ihimbu (Iringa) na kwa shamba la maziwa la Rongai ubinafsishaji kwa mwekezaji Mtanzania upo katika hatua za mwisho. Shamba la ngombe wa maziwa la Malonje litagawanywa katika maeneo madogo ya hekta hamsini kila moja na kumilikishwa Watanzania wenye nia na uwezo wa kufuga kibiashara. Matumaini yangu ni kuwa ubinafsishaji huu wa makusudi ya kusaidia na kuwawezesha wananchi utakuwa na mafanikio makubwa kuliko ule tulioufanya kwenye mashirika ya biashara. Naomba wajitokeze Watanzania wenye nia, mipango mizuri na uwezo na sisi Serikali tutawaunga mkono na kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miundombinu bora ya kiuchumi ni ya lazima ikiwa tunataka kuvutia wawekezaji na kuwawezesha wananchi kushiriki uchumi wa soko. Kazi kubwa imefanyika kwenye eneo hili, lakini nitatoa mifano mitatu tu, barabara, simu na bandari.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya miundombinu muhimu kwa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kijamii, pamoja na kuchochea uzalishaji na biashara ni barabara. Uchumi wa soko ndani na nje ya nchi hauwezi kutengemaa bila barabara nzuri zinazowezesha watu, mazao, bidhaa na huduma kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Tatu iliamua tangu mwanzo kuendeleza kazi ya ujenzi wa barabara iliyoanza kwenye Serikali zilizotangulia. Kwa ushirikiano na Bunge hili tumefanya kazi kubwa ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko.

Mheshimiwa Spika, katika miaka nane iliyopita tumekamilisha miradi ifuatayo:-

Tumekarabati na kupanua barabara zenye urefu wa kilomita 68, tumejenga barabara za lami kiasi cha kilomita 194, tumejenga Daraja la Mto Rufiji na madaraja mengine 22, tumekamilisha upembuzi yakinifu wa barabara ya Mtwara -Songea-*Mbamba Bay* na tumenunua vivuko vya Kilombero na Ukara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ni miradi iliyokamilika. Lakini ipo mingine mingi iliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwemo, ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 961, ukarabati wa kilomita 197 za barabara za lami, upembuzi yakinifu wa barabara zenye urefu wa kilomita 943 na usanifu wa kina wa barabara wa kilomita 367. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo pia miradi ambayo maandalizi yake ya ujenzi na ukarabati wa kilomita 587 yanaendelea. Miradi ya barabara na madaraja ni mingi, siwezi kuiorodhesha yote hapa. Napenda nikushukuruni, Waheshimiwa Wabunge, kwa kuunga mkono Serikali katika mkazo huu tuliouweka kwenye miundombinu na hususan barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee mradi wa ujenzi wa barabara kwa fedha zetu wenyewe kama kielelezi kingine cha mafanikio ya mageuzi yetu ya kiuchumi na dhamira ya Serikali kuwawezesha wananchi kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi miradi muhimu ya barabara ilichelewa kwa vile tulikuwa tunawategemea mno wahisani. Wakati mwingine walisema hawana fedha, wakati mwingine fedha zilichelewa na kusababisha gharama za ujenzi kupanda, wakati mwingine masharti ya kupewa msaada au mkopo yaligeuka kuwa kero.

Mheshimiwa Spika, kwa kadri mapato ya Serikali yalivyoongezeka, tulipata ujasiri wa kujenga barabara kwa haraka zaidi kwa kutumia fedha zetu wenyewe. Tukaamua kila mwezi kutenga shilingi 1.84 bilioni kwa lengo hilo. Katika kipindi cha miaka mitano 2001 mpaka 2005, barabara zifuatazo zitajengwa kwa kiwango cha lami kwa utaratibu huu:-

(a) Barabara ya Somanga-Masaninga na daraja la Matandu.

(b) Barabara ya Nangurukuru-Mbwemkulu.

(c) Barabara ya Mbwemkulu-Mingoyo.

(d) Barabara ya Dodoma-Manyoni.

(e) Barabara ya Manyoni-Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia, asemaye mageuzi yetu hayamsaidii mwananchi amefumba macho kwa hiari yake. Bila mageuzi tusingepata mapato ya kutupa ujasiri huu wa kujitegemea ambao ni uwezeshaji wa kweli wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kushiriki fursa za utandawazi bila ya matumizi ya teknolojia ya mawasiliano, kuanzia simu za kawaida, simu za mkononi, kompyuta, tovuti, intaneti, satelaiti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa mitambo ya simu umeongezeka kutoka njia 125,000 mwaka 1993 hadi njia 242,000 mwaka 2002. Hivi sasa zipo njia za simu za mkononi zaidi ya milioni moja na nashukuru Waheshimiwa Wabunge wamezima zao hapa ili tusikilizane vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huduma hii si tu imechangia kurahisisha mawasiliano ya kibiashara, kijamii na kifamilia, bali pia kwa ujumla wao makampuni ya simu sasa huchangia sana mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, yapo maendeleo ya kutia moyo pia kwenye mifumo na matumizi ya intaneti inayoweza kurahisisha sana upatikanaji wa elimu, habari na ufanyaji biashara kwa gharama nafuu. Hivi sasa Mikoa karibu yote ina vituo vinavyotoa huduma ya intaneti, kasoro Lindi, Rukwa na Ruvuma. Matarajio yetu ni kuwa Mikoa hii nayo itapata vituo hivi kabla ya mwisho wa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo moja lenye uwezo wa kuongeza mapato ya Taifa kwa haraka ni bandari. Nchi yetu imebahatika kuwa katika eneo zuri sana kijiografia. Bandari zetu zinahudumia nchi jirani sita. Ni wajibu wetu kutoa huduma bora bandarini na hivyo kuhimili ushidnani wa bandari nyingine kwenye mwambao wa bahari ya Hindi. Ili kufikia lengo hili, tumepanua na kuboresha Lango la Bandari kule Dar es Salaam, tumejenga eneo la kuhudumia makontena, tumenunua vifaa vya kuhudumia mizigo kwa bandari zote, tumepanua eneo la bandari ya Mtwara, tumejenga kituo cha kuongozea meli Dar es Salaam na kuboresha eneo la matishari kwenye bandari ya Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kubinafsisha huduma za Kitengo cha Makontena, ufanisi wake umeboreka sana na leo kimekuwa cha kwanza kwa ufanisi Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Bandari ya Dar es Salaam imeongeza idadi ya mizigo iliyoshughulikiwa kutoka tani 3.5 milioni mwaka 1998 hadi tani 4.5 milioni mwaka 2002. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo Watanzania lazima tuelezane ukweli. Haiwezekani kwa nchi yetu kuendelea kwa heshima, kwa kujitegemea, bila kuongeza ukubwa na thamani ya mauzo yetu nchi za nje. Ni kweli kumekuwepo na ongezeko kubwa la mauzo ya nje katika miaka michache iliyopita kutoka *USD* 682 milioni mwaka 1995 hadi *USD* 877 milioni mwaka 2002. Lakini ukweli ni kuwa ongezeko hilo limechangiwa zaidi na mauzo ya madini, hususa dhahabu.

Sasa si jambo zuri hata kidogo kutegemea mno mauzo ya madini. Maana kwanza bei yake ina hulka ya kubadilika badilika kila mara na pili, madini yanakwisha. Tunahitaji kujenga uchumi wetu kwa mauzo ya nje ya nchi ambayo yanatokana na uzalishaji viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajivunia pia akiba kubwa ya fedha za kigeni na leo nimerudia majivuno hayo. Lakini ningefurahi zaidi iwapo fedha hizo zingekuwa za Watanzania waliouza nje bidhaa na huduma. Hivi sasa kiasi fulani cha akiba hiyo kinatokana na fedha za mikopo na wahisani. Si jambo zuri hata kidogo. Kwa nini Watanzania hawauzi nje ya nchi? Kinachotushinda ni nini? Hayo ndiyo maswali ya msingi kujiuliza. Kwa nini tunasita kuvutia wawekezaji kwenye viwanda ili kuongeza uwezo wetu wa kuuza nje bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi, huku wananchi wakipata ajira? Lakini nikihimiza uwekezaji huo, naambiwa Mkapa anauza nchi. Tutaamka lini na kuelewa hali halisi ya dunia na mwelekeo wake ndani ya utandawazi?

Mheshimiwa Spika, niwape mifano. Jamhuri ya Dominika *(Dominican Republic)* ina ukubwa wa kilometa 48,072 za mraba ambazo ni asilimia tano ya eneo la Tanzania na watu 8.7 milioni ambao ni asilimia 25 tu ya Watanzania. Hawana kitu cha zaidi kuliko sisi, uchumi wao unategemea sukari, kahawa, tumbaku, saruji na madini kidogo. Katika miaka ya karibuni sekta ya huduma, hususan utalii na maeneo huru ya biashara *(EPZ),* imezidi kilimo kama mchangiaji mkubwa wa uchumi. Mwaka 2000 waliuza nje bidhaa, za *USD* 5.7 bilioni (mara nane ya kwetu kwa mwaka huo) na huduma za *USD* 3.2 bilioni (mara tano ya kwetu kwa mwaka huo). Haya ndiyo maswali ya msingi ya Watanzania kujiuliza. Tunashindwaje na nchi ndogo kama Jamhuri ya Dominika kuu za nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, mwezi Agosti, tulizindua Sera ya Taifa ya Biashara, ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kuiwezesha Tanzania kupiga vita umaskini kwa kufanya biashara ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nalishukuru Bunge hili Tukufu kwa kupitisha Sheria ya Maeneo Maalum kwa Mauzo Nje *(EPZ)* ili kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha bidhaa kwa soko la nje. Tayari viwanda viwili vimeanzishwa na vinauza nje kwa utaratibu huu. Lakini kasi hii bado ni ndogo sana. Ni aibu kubwa kwamba mimi niko mstari wa mbele kudai nchi tajiri zifungue milango kwa bidhaa zetu, wakati ambapo bado Tanzania haina bidhaa za kutosha za kuuza!! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiulizwa kipi hasa ninashindwa kuuza nitasemaje? Nikiulizwa wauzaji nje makini wako wangapi nitajibu nini? Hodari wa kelele, dhaifu wa vitendo. Ndio sisi Watanzania, nitaambiwa! Nitaambiwa hivyo na kwa kweli nimeambiwa na kiongozi wa *European Union* maana nilimwandikia. Haki yetu ya kuuza Marekani kwa masharti nafuu chini ya utaratibu wa *AGOA* bado hatuitumii kikamilifu. Jirani zetu Kenya wako mbali. Haki yetu ya kuuza katika nchi za Umoja wa Ulaya zinazoturuhusu kuuza karibu kila kitu isipokuwa silaha, nayo hatuitumii kikamilifu pamoja na vikwazo wanavyoweka. Lakini ninapokaribisha wawekezaji kuharakisha kujenga uwezo wetu kuuza nje na wakati huo huo kuleta ajira, wanaibuka wale wanaosema mkubwa Mkapa anauza nchi. Watu wa ajabu sana hawa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi bado naamini kuwa tukijituma zaidi tunaweza kufanya mambo mengi makubwa. Mwaka jana, kwa mfano, Wizara ya Ushirika na Masoko ilihamasisha na kuwawezesha wakulima na wafanyabiashara wa mbogamboga, maua, matunda na viungo vya vyakula kushiriki Maonyesho ya Kimataifa ya bidhaa hizo kule Rostock, Ujerumani. Walipata mafanikio makubwa, ambapo Tanzania ilipata Nishani ya Heshima na washiriki kutoka Tanzania walipata jumla ya medali 33, zikiwemo 12 za dhahabu, 14 za fedha na saba za shaba. Medali hizo hata hivyo hazitakuwa na maana kama hatutauza hizo mbogamboga, hivyo vituo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema inawezekana iwapo tutajituma zaidi na kutumia vizuri fursa na uwezeshaji unaofanywa na Serikali. Kwa taarifa tu Jamhuri ya Dominika inauza nje bidhaa hizo hizo za matunda tulizopewa sisi medali za dhahabu, wanauza bidhaa hizo hizo za matunda na mbogamboga zenye thamani ya *USD* 104.2 kwa mwaka. Sisi, pamoja na nchi kubwa kama hii aliyotupa Mwenyezi Mungu tunashindwaje hasa baada ya mafanikio ya Maonyesho ya Rostock?

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Tano wa Mawaziri wa Biashara Duniani ulivunjika kule Cancun mwezi Septemba, 2003 bila makubaliano kufikiwa kuhusu mwenendo wa biashara duniani. Ulivunjika pia bila kuendeleza mbele ajenda iliyoanza kule Doha ya kuhusisha biashara na maendeleo ya nchi maskini. Kuvunjika kwa Mkutano huo ilikuwa pigo kubwa kwa maendeleo ya nchi kama zetu na kwa utaratibu bora wa utawala duniani wa mashauriano badala ya kila nchi moja au kundi la nchi kujiamulia wenyewe bila kuzingatia athari za maamuzi yao kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, chanzo hasa cha Mkutano kuvunjika ni kuwa ahadi nyingi zilizowekwa kule Doha hazikutekelezwa na nchi maskini zilionyesha wazi kukataa kuendelea na hadaa za Mataifa makubwa. Karibu kila nchi hata zile tajiri inakiri kuwa ruzuku zinazotolewa kwa wakulima na wafugaji katika nchi tajiri zikiwemo ruzuku za uzalishaji na za kuuza nje ya nchi zao, zimeathiri sana uwezo wa wakulima na wafugaji katika nchi maskini ambao wao hawapati ruzuku za kushindana na bidhaa za wenzao wanaopata ruzuku katika nchi tajiri. *(Makofi)*

Isitoshe nchi hizo zina vikwazo vya aina mbalimbali vinavyozuia wakulima na wafugaji katika nchi maskini kuuza kwao, hasa kwa kadri bidhaa hizo zinavyoongezewa thamani kwa kusindikwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kujivunia kwa nchi maskini na zinazoendelea, ni kuwa kule Cancun tuliungana na kuwa kitu kimoja, tukakataa kuendelea kuburuzwa kwenye suala la ruzuku kwa wakulima na wafugaji katika nchi tajiri na pia suala la wakubwa kutuharakisha mno kuzungumzia mambo yaitwayo "Masuala ya Singapore," masuala ambayo dhahiri yanawaongezea wao na kutupunguzia sisi, fursa na tija katika biashara na uwekezaji. Umoja na uimara wa nchi maskini na zinazoendelea kwa upande mmoja na kwa upande mwingine kushindwa kwa nchi tajiri kutoa majibu muafaka kwa madai ya nchi zinazoendelea, ndiyo mambo yaliyosababisha mkutano uvunjike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa juhudi zinaendelea kujaribu kufufua duru ya mazungumzo ya biashara duniani, duru ambayo kule Doha tulikubaliana iitwe "Duru ya Maendeleo". Lakini ni wazi duru hiyo haiwezi kuwa ya maendeleo bila makubaliano juu ya kupunguza na hatimaye kufuta zile ruzuku kwenye kilimo na ufugaji zinazofanya kusiwe na usawa wala haki kwenye biashara. Tunaziomba sana nchi tajiri wasiishie kwenye kukiri kwamba ruzuku zao zinatuumiza bali wachukue hatua mapema ya kuzirekebisha na hatimaye kuzifuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatoa wito kwa nchi zote duniani tuanze tena mazungumzo, lakini kwa kuelewana kuwa Cancun ilikuwa mwanzo wa mfumo mpya wa majadiliano, mfumo unaozingatia kwa dhati kuwa maskini nao wana haki, wanastahili kusikilizwa na wanastahili kusaidiwa ili kutumia biashara kujiendeleza, badala ya kuzidi kutegemea misaada ya wahisani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nahutubia Bunge lako Tukufu, tarehe 30 Januari, 2002, ndiyo nilitoka tu kupewa heshima na Shirika la Kazi Duniani kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Kimataifa Kuhusu Masuala ya Kijamii katika Utandawazi. Tume hiyo niliyoiongoza na Mwenyekiti-Mwenza, Mheshimiwa Tarja Halonen, Rais wa Finland, imemaliza kazi zake na tunatarajia kuzindua Ripoti yake Mjini Geneva na London tarehe 23 na 24 Februari, 2004 baadaye wiki mbili zijazo. Aidha, natarajiwa kuikabidhi Ripoti hiyo rasmi kwenye Baraza la Utendaji la Shirika la Kazi Duniani baadaye mwezi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya msingi ya Tume ilikuwa kujaribu kuanzisha mjadala wa kiungwana kuhusu utandawazi, hususan athari zake katika masuala ya kijamii. Tume imezibainisha athari hizo, ikiwemo kwenye maeneo ya kiuchumi na kimaendeleo. Aidha, imesisitiza nafasi kubwa ya utandawazi, ukiongozwa vizuri, huwa nguzo kuu ya maendeleo ya jamii zote duniani. Tume inaonya kwamba pamoja na kwamba utandawazi waweza kuwa wa manufaa makubwa kwa jamii zote duniani, sasa hivi hofu na hasira kubwa kutokana na jinsi utandawazi unavyoendelea inajengeka. Hii ni hatari, si tu kwa jamii inayoathirika, bali kwa jamii nzima ya Kimataifa. Ipo methali ya Kichina isemayo "Moto hauwezi kufunikwa kwa karatasi." Ujumbe wetu wa Tume ni kuwa: "Moto wa chuki inayojengeka dhidi ya utandawazi haiwezi tena kufunikwa kwa karatasi."

Mheshimiwa Spika, ili kuzikabili athari za utandawazi, tutahitaji kuungwa mkono na viongozi wa kisiasa na kibiashara katika ngazi zote, Kimataifa, Kikanda na Kitaifa. Lakini hatuwezi kuulaumu utandawazi kwa kila shida yetu na umaskini wetu. Kama Taifa, tunayo mengi ambayo hatuna budi kuyafanya ili kunufaika na utandawazi. Mojawapo, kama nilivyosema ni elimu. Vijana tunaowatayarisha kuongoza maendeleo ya Taifa letu hwana budi kuwa vijana wanaokidhi mahitaji ya maendeleo ya kisasa hasa katika uzalishaji na ajira.

Wakati tunajitahidi kujenga mazingira yatakayowezesha utandawazi kuwa wa manufaa kwa nchi zetu sharti tuelewe kwanza kwamba hatma ya nchi yetu ipo mikononi mwetu. Dunia iliyopo nje yetu inaweza kuendelea bila sisi. Lakini siamini kwamba sisi tunaweza kuendelea bila dunia hiyo. Tukishajiandaa vya kutosha ndani ya nchi yetu ndipo tutapata nguvu na uhalali kudai ziwepo sheria na taratibu zinazotabirika na zinazolinda maslahi ya wanyonge katika biashara na maendeleo duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote niliyoyasema yanatoa changamoto kubwa sana kwa sera yetu ya mambo ya nje. Lazima tujenge uwezo wa kutambua misukumo ya mabadiliko yanayokabili dunia na kubuni sera na mbinu zitakazotuwezesha kuyakabili na wakati huo huo kuendeleza amani, utulivu na maendeleo hapa nchini kwa majirani zetu, bara letu na duniani kote.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu ukosefu wa amani katika nchi za jirani umekuwa ni mzigo mkubwa kwa Taifa letu, hasa kwa maana ya wakimbizi na uharibifu wa mazingira. Hatuwezi kupata suluhu ya kudumu ya matatizo kama haya kwa juhudi zetu peke yetu. Matatizo haya yanahitaji mtazamo mpana na wa pamoja kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nchini Burundi, Serikali ya mpito inaendelea vizuri, hivi sasa ikiongozwa na Rais Domitien Ndayizeye. Tunamshukuru yeye na Warundi wote kwa jitihada wanazozifanya ili amani ya kudumu ipatikane nchini kwao. Hivi karibuni vikundi vya waasi vimekubali kuweka chini silaha zao na kushiriki kutafuta suluhu ya matatizo yao. Tunaendelea kukihimiza kikundi kilichobakia cha *FNL* ili nao wajiunge na Warundi wenzao katika kujenga mustakabali wa nchi yao kwa amani. Kama kawaida tutakuwa tayari kusaidia jitihada hizo.

Mheshimiwa Spika, katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo jitihada za Wakongo chini ya Rais Joseph Kabila zinaendelea kuleta matumaini kwa amani ya nchi hiyo iliyoteseka sana na hata katika eneo lote la Maziwa Makuu. Tunawashukuru sana Rais Thabo Mbeki wa Afrika Kusini na Makamu wake

Bwana Jacob Zuma, kwa jitihada zao. Tunawashukuru viongozi wengine wa Ukanda wa Maziwa Makuu ambao wametoa mchango mkubwa katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuelewa umuhimu huu, Jumuiya ya Kimataifa ikiongozwa na Umoja wa Mataifa ipo mbioni kutayarisha Mkutano wa Kimataifa kuhusu eneo la Maziwa Makuu. Nchi yetu imepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa mkutano huu unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusudi la mkutano huo ni kutafuta mkakati wa Kimataifa utakaoziunga mkono juhudi za nchi zetu kukabili vyanzo vya vita, kuainisha misaada ya maendeleo na kujenga uwezo wetu wa kuzuia vita na kulinda amani.

Kwa muda mrefu eneo letu limefahamika kama eneo la vita. Hali hii imetunyima nafasi ya kutumia umoja wetu na maliasili zetu kwa manufaa ya nchi zetu na watu wake. Sura hii haitoi mtazamo wa maendeleo na sio kivutio cha mitaji wala wawekezaji katika eneo letu. Tanzania itashiriki kikamilifu katika jitihada zote za kufanya eneo la Maziwa Makuu liwe na amani ya kudumu na maendeleo endelevu na ligeuke kuwa ukanda wa amani.

Mheshimiwa Spika, sababu mojawapo ya kuhamishia majukumu ya uzalishaji na biashara kutoka Serikalini kwenda sekta binafsi, ni kuipa Serikali fursa kushughulikia vizuri zaidi majukumu asilia ya dola ikiwemo ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, majukumu hayo yanatekelezeka tu iwapo Serikali ina uwezo wa mapato, uwezo ambao kwetu sisi tumechangiwa sana na mafanikio ya mageuzi yetu ya uchumi. Ninafurahi kulijulisha Bunge hili Tukufu kuwa ongezeko kubwa la mapato ya Serikali limetuwezesha kuhudumia majeshi yetu vizuri zaidi na kuyawezesha kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi. Nitataja machache tu tuliyoweza kuyafanya.

La kwanza, kwa umuhimu, ni kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeweza kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha upo ulinzi imara kwa nchi nzima ili wananchi wafanye kazi zao na kuishi bila hofu. Sera yetu ya ulinzi inaweka mkazo mkubwa kwenye ulinzi wa mgambo. Hali nzuri ya kifedha imetuwezesha kuendeleza mafunzo ya mgambo na matunda ya kuimarika kwa ulinzi wa mgambo yameanza kuonekana hasa sehemu za mipakani. *(Makofi)*

Sera yetu pia ni ya kuwa na jeshi dogo la kitaalam, lililoiva kwa ujuzi, uwezo, uhodari, nidhamu na utii. Mafunzo ya Jeshi la aina hiyo ni ghali, lakini ni muhimu sana. Kwa sasa hivi tumeweka kufanya mazoezi ya kijeshi sisi wenyewe na pia kwa kushirikiana na nchi jirani. *(Makofi)*

Mafanikio ya mageuzi yetu ya uchumi yametuwezesha pia kukidhi baadhi ya huduma muhimu kwa Maafisa na Askari wa JWTZ na JKT. Kwa mfano:-

- Hospitali za Jeshi, ikiwemo Hospitali Kuu ya Lugalo na hospitali za Kanda za Mbeya na Mwanza zimekarabatiwa na kupatiwa vifaa ili kuhudumia Maafisa na Askari na wananchi. *(Makofi)*

- Upatikanaji na ubora wa chakula kwa wanajeshi umeboreka sana na Mabwalo vikosini yameimarishwa.

- Maduka ya bei nafuu yamefunguliwa kwenye vikosi vingi.

- Zimenunuliwa ndege mbili kubwa za usafirishaji ambazo pia zinaweza kutumika wakati wa maafa.

- Jeshi limenunua sare mpya za kutosha Maafisa na Askari wote.

- Tatizo la malazi kwa Askari wapya na kwenye vyuo limeondolewa na wanapata vifaa vya kutosheleza.

- Tumeweza pia kukamilisha ujenzi wa nyumba ambazokwa miaka mingi zilikuwa hazijakamilika kule Monduli, Arusha na hapa Ihumwa, Dodoma.

- Tumeweza kuanza mradi wa kuboresha utawala na utoaji maamuzi kwa kuweka kompyuta kwa awamu.

- Uwajibikaji na usimamizi kuhusu matumizi ya fedha za Serikali umeboreka sana. Hakuna tena malimbikizo makubwa ya madeni na hoja za ukaguzi zimepungua.

- Mishahara na posho za chakula vimeboreshwa kiasi na ucheleweshaji malipo haupo tena.

- Tumefufua utaratibu wa kupeleka vijana JKT.

- Tumekarabati makambi ya JKT ya Ruvu, Makutupora, Oljoro na Mafinga na mengine yanaendelea kukarabatiwa.

- Tumeweza kujenga ofisi mpya za Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa yenye hadhi inayostahili.

- Tumeweza pia kuboresha hali kwenye majeshi yetu ya Polisi na Magereza.

- Bajeti ya Jeshi la Polisi imeongezeka kwa asilimia 176 kwa miaka miwili tu na Jeshi la Magereza kwa asilimia 135. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeweza kuendelea na kuendelea. Niliyosema yanatosha kuonyesha kuwa anayesema haoni faida ya mageuzi yetu ya uchumi basi ama amekaa kiti cha nyuma au amefumba macho! Nasema, tukumbuke tulikotoka. Na kwa kweli natoa shukrani zangu kwa uvumilivu wa Wakuu, Maafisa na Askari wa Majeshi yetu yote ya ulinzi na usalama tulipokuwa tunakusanya nguvu na kurekebisha uchumi, kulikoambatana na kufunga mikanda. Nawapongeza wote pia kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa niaba ya Taifa lao. Najua matatizo hayajaisha, lakini tumeanza vizuri na tutaendelea kwa kadri uchumi unavyokua. *(Makofi/Kicheko)*

Serikali imeanza kuviimarisha vikosa vya Zimamoto na Uokoaji katika Halmashauri. Kwa kuanzia tayari Serikali Kuu imetoa shilingi 1.5 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa magari mapya kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam na shilingi 600 milioni kwa ajili ya Jiji la Mwanza. Halmashauri za Mikoa mingine saba zitafaidika na mpango huu katika mwaka ujao wa fedha na hapa napenda niwapongeze wote walioshiriki kwa namna na kwa viwango, tofauti katika kuzima moto uliotokea tarehe 22 Januari, 2004 kwenye matanki ya mafuta kwenye kituo cha *TANESCO* Ubungo, kule Dar es Salaam.

Kwa namna ya pekee kabisa nawapongeza sana na kuwashukuru Askari Zimamoto wa Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam, Mratibu Mpemba Mputa Magogo na Sajini Fadhili Mtola, ambao ujasiri wao wa kupigiwa mfano ulioepusha hasara kubwa na maisha ya raia wenzao wengi waliokuwa hatarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nimekumbuka sana hadithi za walevi. Walevi wawili walikuwa wanatembea usiku. Mmoja akaangalia juu, akamwambia mwenziwe: "Usiku wa leo ni mzuri kweli, hebu ona mwezi ulivyopendeza!" Mwenziwe akasimama, akapepesuka kidogo, kisha akajibu: "Wewe vipi, umelewa nini, huo sio mwezi, hilo ni jua." Wakabishana kwa muda mpaka walipomwona mtu wa tatu akipitia karibu yao. Kumbe naye mlevi. Wakamwuliza: "Samahani bwana, hebu tusaidie. Lile ni jua au mwezi?" Mlevi wa tatu akasimama, akafinya macho, kisha akajibu: "Sijui bwana, mimi ni mgeni hapa!" *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sitarajii Mtanzania akiulizwa kuhusu uzuri wa uwazi wa kazi iliyofanyika katika nchi yetu ajibu kuwa yeye hajui kwa vile haishi hapa. Sote tunaishi hapa na tunajua tulikotoka. Nawaomba Watanzania wakumbuke tulikotoka na wasione haya kukiri kuwa tumepiga hatua kubwa. Najua si hulka yetu kujisifu, lakini dunia ya leo inahitaji kujisifu. Tusiwaachie wageni tu ndio kila mara wanaimba sifa zetu, wakati wenyewe tunakuwa kama hatuhusiki na hatuoni. *(Makofi/Kicheko)*

Na wote hawa wanaotusifu, pamoja na wawekezaji wakubwa wa Kimataifa, wanauliza kwa nini Watanzania wenyewe hawajitangazi na kueneza habari njema ya mafanikio yao zaidi. Jibu langu siku zote limekuwa kwamba kwa asili na hulka yetu Watanzania, hatupendi kujisifu. Na wao hunikumbusha kuwa dunia imebadilika na itabadilika zaidi. Haitoshi tena kufanya jambo jema tu. Lazima pia watu na dunia wajue jema ulilolifanya. Ushindani uliopo na ujao unahitaji nchi kujitangaza na kutambulika zaidi. Dunia sasa imekuwa ya wawamba ngozi, ambapo kila mtu anavutia kwake. Siku hizi hata nchi zinajitangaza kama bidhaa na hivyo hujipachika rajamu *(brand),* yaani alama ya biashara. Nasi Watanzania, muda umefika tutambulike kwa sababu au sifa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tusifiche kasoro na mapungufu yetu hasa miongoni mwetu wenyewe. Lakini tusionee haya, wala kupuuza mafanikio tuliyoyapata. Mwanga wa Kitaifa umulike zaidi mafanikio, na tuyainue juu ili kila mwananchi ayaone na watu wa nje nao wajue kuwa hii ni nchi ya watu makini walioamua kwa dhati kulinda heshima na utu wao kwa kutafuta maendeleo. Si heshima kujidharau mwenyewe, kujipuuza mwenyewe. Sifa ya nchi si sifa ya mtu au sifa ya chama au sifa ya Serikali, ni sifa ya nchi. Hivyo hivyo, aibu ya nchi si ya mtu au chama au Serikali, ni aibu ya nchi na Watanzania wote. Kosoa kwa uadilifu panapostahili kukosolewa na sifu kwa bidii zote panapostahili sifa. Nitatoa mifano michache. *(Makofi)*

Kwa kutumia misingi imara waliyotuachia Waasisi wetu, Baba wa Taifa, Marehemu Julius Nyerere na mzee wetu Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume, tumeweza kujenga taasisi za kisiasa ambazo ni nyumbulifu na endelevu zinazoweza kuhimili matatizo ya aina mbalimbali. Kielelezo kimojawapo ni Mwafaka. Kasi ya kupatikana kwa ufumbuzi wa matatizo ya kisiasa Zanzibar, hasa baada ya kuushughulikia sisi wenyewe, peke yetu, iliwashangaza wengi. Maana, Barani Afrika, lakini pia hata katika baadhi ya nchi za wakubwa, ipo migogoro ya kisiasa ambayo imechukua miongo na miongo bila kupata mwafaka ulio murua na endelevu kama wa kwetu. Sisi tumeweza, na pande zote mbili zimeonyesha ukomavu wa kisiasa wa kuheshimu muafaka na utekelezaji wake. Mwafaka wetu sasa ni mfano kwa wengine na sitashangaa wakija wasomi kutoka mbali wakautafiti na kujipatia Shahada za Udaktari wa Falsafa. Lakini ni kama vile sisi wenyewe hatuoni kuwa hilo ni jambo kubwa sana la kujivunia na kuwa mwafaka wetu ni kielelezo cha ukomavu, unyumbulifu na uendelevu wa taasisi zetu za kisiasa. *(Makofi)*

Mfano wa pili wa kisiasa, ni kipindi cha mwezi mzima ambao nilikuwa nje ya nchi kwa matibabu. Mimi sijui ni nchi ngapi Barani Afrika zingeweza kutulia kisiasa kama Watanzania walivyotulia katika kipindi chote hicho ambacho sikuwepo nchini. Ni sifa kwa Watanzania, lakini pia ni kielelezo cha ukomavu, unyumbulifu na uendelevu wa taasisi zetu za kisiasa na za ndola. Tusione aibu kujisifu. *(Makofi)*

Kiuchumi hali kadhalika, kwa vigezo vyovyote vile, Tanzania sasa imejijengea misingi imara ya uchumi na hivyo kuufanya uchumi wetu uanze kuwa nyumbulifu na endelevu. Kama nilivyosema kuwa nyumbulifu na endelevu kwa Kiingereza *resilient and sustainable.*

Kama nilivyosema, tunao ukame msimu huu kwenye sehemu kubwa ya nchi yetu. Ingekuwa zamani tungekuwa tunahaha kweli kweli. Lakini leo ninaposema wananchi wasiwe na wasiwasi, nasema hivyo kwa kujiamini, maana tunayo akiba ya kutosha ya fedha za kigeni na tunayo mahusiano mazuri na nchi wahisani ambao tunashukuru wanaunga mkono juhudi za Serikali kuhakikisha kinakuwepo chakula cha kutosha kwenye pembe zote za nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa upande wa kijamii nako tunayo mengi ya kujivunia na kutangaza. Umoja wa Kitaifa, heshima kwa watu wote, mafanikio katika vita dhidi ya ubaguzi wa dini, madhehebu ya dini, rangi na kabila yote yanasifiwa duniani kote. Sisi tumeyazoea, tunayaona ni ya kawiada. Lakini si mambo haya

kawaida barani Afrika. Tumefika mahali ambapo hakuna mwanasiasa makini atakayethubutu hadharani kueneza mambo ya udini au ukabila. Akifanya, ni kwa kujificha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunayo mengi ya kujisifu na kujitangaza nayo. Tusidhani ni sifa kujidharau au kujibeza wenyewe. Busara ni kujijengea heshima kwa kuhakikisha mafanikio yako yanajulikana.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imekuwa ndefu mno, lazima sasa niihitimishe. Tumepiga hatua kubwa. Katika Bunge hili wapo waliotoa mchango wao mkubwa sana katika mafanikio hayo.

Kwa niaba ya Watanzania wote nawashukuru na kuwapongeza sana. Ombi langu tusirudi nyuma, wala kupunguza kasi. Tanzania hapa ilipo ni kama ndege iliyo kwenye njia ya kurukia *(Runway)* . Inakwenda mbele, inaelekea mahali panapostahili, tulipowaelezea kwenye *version* yetu, lakini bado ipo ardhini, haijanyanyuka na kupaa. Kwa ajili ya watoto wetu, na hatma ya Taifa letu katika utandawazi, lazima sasa tupae. Uchumi wetu unahitaji nguvu mpya, msukumo mpya ili upae. Na nguvu hiyo na msukumo huo si mwingine ila uwekezaji mkubwa zaidi, utakaotoa nafasi nyingi zaidi za ajira, utakaotuwezesha kuuza nje kwa wingi zaidi na utakaoimarisha uchumi wetu na kutoa fursa nyingi zaidi za kila raia aliye tayari ajiendeleze. Tuwe jasiri na tuwe makini. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu akipenda ninayo miezi 20 ya kuongoza nchi yetu. Tusaidianeni ili niache uongozi Tanzania ikiwa inapaa, si ikiwa bado kwenye njia ya kurukia. Inawezekana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waheshimiwa Wabunge mmeisikia hotuba ya Mheshimiwa Rais na Watanzania wote ambao walikuwa wamefungua Redio zao wameisikia kwa sababu ilikuwa inatoka moja kwa moja.

Hali kadhalika Mheshimiwa Rais, amenijulisha kwamba hotuba hii kama haijawekwa tayari itawekwa kwenye *Website* ya Serikali ili Watanzania walioko nchi za nje waweze nao kujua yaliyomo. Kwetu sisi pamoja na kuwa kwenye *Hansard,* lakini vitabu vya hotuba tumekwishakabidhiwa tutawagawia Waheshimiwa Wabunge sasa hivi, ili muweze kuanza kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Ile hotuba yake alipozungumza mara ya mwisho mwaka 2002 nilipomshukuru kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge nilitumia neno la Kiingereza kwamba *it was a powerful speech.* Hii hotuba ya leo ningependa kuieleza kwa maneno yafuatayo kwamba, *it was authoritative, comprehensive and inspiring.* *(Makofi)*

- Upatikanaji na ubora wa chakula kwa wanajeshi umeboreka sana na Mabwalo vikosini yameimarishwa.

- Maduka ya bei nafuu yamefunguliwa kwenye vikosi vingi.

- Zimenunuliwa ndege mbili kubwa za usafirishaji ambazo pia zinaweza kutumika wakati wa maafa.

- Jeshi limenunua sare mpya za kutosha Maafisa na Askari wote.

- Tatizo la malazi kwa Askari wapya na kwenye vyuo limeondolewa na wanapata vifaa vya kutosheleza.

- Tumeweza pia kukamilisha ujenzi wa nyumba ambazo kwa miaka mingi zilikuwa hazijakamilika kule Monduli, Arusha na hapa Ihumwa, Dodoma.

- Tumeweza kuanza mradi wa kuboresha utawala na utoaji maamuzi kwa kuweka kompyuta kwa awamu.

- Uwajibikaji na usimamizi kuhusu matumizi ya fedha za Serikali umeboreka sana. Hakuna tena malimbikizo makubwa ya madeni na hoja za ukaguzi zimepungua.

- Mishahara na posho za chakula vimeboreshwa kiasi na ucheleweshaji malipo haupo tena.

- Tumefufua utaratibu wa kupeleka vijana JKT.

- Tumekarabati makambi ya JKT ya Ruvu, Makutupora, Oljoro na Mafinga na mengine yanaendelea kukarabatiwa.

- Tumeweza kujenga ofisi mpya za Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa yenye hadhi inayostahili.

- Tumeweza pia kuboresha hali kwenye majeshi yetu ya Polisi na Magereza.

- Bajeti ya Jeshi la Polisi imeongezeka kwa asilimia 176 kwa miaka miwili tu na Jeshi la Magereza kwa asilimia 135. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeweza kuendelea na kuendelea. Niliyosema yanatosha kuonyesha kuwa anayesema haoni faida ya mageuzi yetu ya uchumi basi ama amekaa kiti cha nyuma au amefumba macho! Nasema, tukumbuke tulikotoka. Na kwa kweli natoa shukrani zangu kwa uvumilivu wa Wakuu, Maafisa na Askari wa Majeshi yetu yote ya ulinzi na usalama tulipokuwa tunakusanya nguvu na kurekebisha uchumi, kulikoambatana na kufunga mikanda. Nawapongeza wote pia kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa niaba ya Taifa lao. Najua matatizo hayajaisha, lakini tumeanza vizuri na tutaendelea kwa kadri uchumi unavyokua. *(Makofi/Kicheko)*

Serikali imeanza kuviimarisha vikosa vya Zimamoto na Uokoaji katika Halmashauri. Kwa kuanzia tayari Serikali Kuu imetoa shilingi 1.5 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa magari mapya kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam na shilingi 600 milioni kwa ajili ya Jiji la Mwanza. Halmashauri za Mikoa mingine saba zitafaidika na mpango huu katika mwaka ujao wa fedha na hapa napenda niwapongeze wote walioshiriki kwa namna na kwa viwango, tofauti katika kuzima moto uliotokea tarehe 22 Januari, 2004 kwenye matanki ya mafuta kwenye kituo cha *TANESCO* Ubungo, kule Dar es Salaam.

Kwa namna ya pekee kabisa nawapongeza sana na kuwashukuru Askari Zimamoto wa Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam, Mratibu Mpemba Mputa Magogo na Sajini Fadhili Mtola, ambao ujasiri wao wa kupigiwa mfano ulioepusha hasara kubwa na maisha ya raia wenzao wengi waliokuwa hatarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nimekumbuka sana hadithi za walevi. Walevi wawili walikuwa wanatembea usiku. Mmoja akaangalia juu, akamwambia mwenziwe: “Usiku wa leo ni mzuri kweli, hebu ona mwezi ulivyopendeza!” Mwenziwe akasimama, akapepesuka kidogo, kisha akajibu: “Wewe vipi, umelewa nini, huo sio mwezi, hilo ni jua.” Wakabishana kwa muda mpaka walipomwona mtu wa tatu akipitia karibu yao. Kumbe naye mlevi. Wakamwuliza: “Samahani bwana, hebu tusaidie. Lile ni jua au mwezi?” Mlevi wa tatu akasimama, akafinya macho, kisha akajibu: “Sijui bwana, mimi ni mgeni hapa!” *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sitarajii Mtanzania akiulizwa kuhusu uzuri wa uwazi wa kazi iliyofanyika katika nchi yetu ajibu kuwa yeye hajui kwa vile haishi hapa. Sote tunaishi hapa na tunajua tulikotoka. Nawaomba Watanzania wakumbuke tulikotoka na wasione haya kukiri kuwa tumepiga hatua kubwa. Najua si hulka yetu kujisifu, lakini dunia ya leo inahitaji kujisifu. Tusiwaachie wageni tu ndio kila mara wanaimba sifa zetu, wakati wenyewe tunakuwa kama hatuhusiki na hatuoni. *(Makofi/Kicheko)*

Na wote hawa wanaotusifu, pamoja na wawekezaji wakubwa wa Kimataifa, wanauliza kwa nini Watanzania wenyewe hawajitangazi na kueneza habari njema ya mafanikio yao zaidi. Jibu langu siku zote limekuwa kwamba kwa asili na hulka yetu Watanzania, hatupendi kujisifu. Na wao hunikumbusha kuwa dunia imebadilika na itabadilika zaidi. Haitoshi tena kufanya jambo jema tu. Lazima pia watu na dunia wajue jema ulilolifanya. Ushindani uliopo na ujao unahitaji nchi kujitangaza na kutambulika zaidi. Dunia sasa imekuwa ya wawamba ngozi, ambapo kila mtu anavutia kwake. Siku hizi hata nchi zinajitangaza kama bidhaa na hivyo hujipachika rajamu *(brand),* yaani alama ya biashara. Nasi Watanzania, muda umefika tutambulike kwa sababu au sifa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tusifiche kasoro na mapungufu yetu hasa miongoni mwetu wenyewe. Lakini tusionee haya, wala kupuuza mafanikio tuliyoyapata. Mwanga wa Kitaifa umulike zaidi mafanikio, na tuyainue juu ili kila mwananchi ayaone na watu wa nje nao wajue kuwa hii ni nchi ya watu makini walioamua kwa dhati kulinda heshima na utu wao kwa kutafuta maendeleo. Si heshima kujidharau mwenyewe, kujipuuza mwenyewe. Sifa ya nchi si sifa ya mtu au sifa ya chama au sifa ya Serikali, ni sifa ya nchi. Hivyo hivyo, aibu ya nchi si ya mtu au chama au Serikali, ni aibu ya nchi na Watanzania wote. Kosoa kwa uadilifu panapostahili kukosolewa na sifu kwa bidii zote panapostahili sifa. Nitatoa mifano michache. *(Makofi)*

Kwa kutumia misingi imara waliyotuachia Waasisi wetu, Baba wa Taifa, Marehemu Julius Nyerere na mzee wetu Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume, tumeweza kujenga taasisi za kisiasa ambazo ni nyumbulifu na endelevu zinazoweza kuhimili matatizo ya aina mbalimbali. Kielelezo kimojawapo ni Mwafaka. Kasi ya kupatikana kwa ufumbuzi wa matatizo ya kisiasa Zanzibar, hasa baada ya kuushughulikia sisi wenyewe, peke yetu, iliwashangaza wengi. Maana, Barani Afrika, lakini pia hata katika baadhi ya nchi za wakubwa, ipo migogoro ya kisiasa ambayo imechukua miongo na miongo bila kupata mwafaka ulio murua na endelevu kama wa kwetu. Sisi tumeweza, na pande zote mbili zimeonyesha ukomavu wa kisiasa wa kuheshimu muafaka na utekelezaji wake. Mwafaka wetu sasa ni mfano kwa wengine na sitashangaa wakija wasomi kutoka mbali wakautafiti na kujipatia Shahada za Udaktari wa Falsafa. Lakini ni kama vile sisi wenyewe hatuoni kuwa hilo ni jambo kubwa sana la kujivunia na kuwa mwafaka wetu ni kielelezo cha ukomavu, unyumbulifu na uendelevu wa taasisi zetu za kisiasa. *(Makofi)*

Mfano wa pili wa kisiasa, ni kipindi cha mwezi mzima ambao nilikuwa nje ya nchi kwa matibabu. Mimi sijui ni nchi ngapi Barani Afrika zingeweza kutulia kisiasa kama Watanzania walivyotulia katika kipindi chote hicho ambacho sikuwepo nchini. Ni sifa kwa Watanzania, lakini pia ni kielelezo cha ukomavu, unyumbulifu na uendelevu wa taasisi zetu za kisiasa na za ndola. Tusione aibu kujisifu. *(Makofi)*

Kiuchumi hali kadhalika, kwa vigezo vyovyote vile, Tanzania sasa imejijengea misingi imara ya uchumi na hivyo kuufanya uchumi wetu uanze kuwa nyumbulifu na endelevu. Kama nilivyosema kuwa nyumbulifu na endelevu kwa Kiingereza *resilient and sustainable.*

Kama nilivyosema, tunao ukame msimu huu kwenye sehemu kubwa ya nchi yetu. Ingekuwa zamani tungekuwa tunahaha kweli kweli. Lakini leo ninaposema wananchi wasiwe na wasiwasi, nasema hivyo kwa kujiamini, maana tunayo akiba ya kutosha ya fedha za kigeni na tunayo mahusiano mazuri na nchi wahisani ambao tunashukuru wanaunga mkono juhudi za Serikali kuhakikisha kinakuwepo chakula cha kutosha kwenye pembe zote za nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa upande wa kijamii nako tunayo mengi ya kujivunia na kutangaza. Umoja wa Kitaifa, heshima kwa watu wote, mafanikio katika vita dhidi ya ubaguzi wa dini, madhehebu ya dini, rangi na kabila yote yanasifiwa duniani kote. Sisi tumeyazoea, tunayaona ni ya kawiada. Lakini si mambo haya kawaida barani Afrika. Tumefika mahali ambapo hakuna mwanasiasa makini atakayethubutu hadharani kueneza mambo ya udini au ukabila. Akifanya, ni kwa kujificha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunayo mengi ya kujisifu na kujitangaza nayo. Tusidhani ni sifa kujidharau au kujibeza wenyewe. Busara ni kujijengea heshima kwa kuhakikisha mafanikio yako yanajulikana.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imekuwa ndefu mno, lazima sasa niihitimishe. Tumepiga hatua kubwa. Katika Bunge hili wapo waliotoa mchango wao mkubwa sana katika mafanikio hayo.

Kwa niaba ya Watanzania wote nawashukuru na kuwapongeza sana. Ombi langu tusirudi nyuma, wala kupunguza kasi. Tanzania hapa ilipo ni kama ndege iliyo kwenye njia ya kurukia *(Runway)* . Inakwenda mbele, inaelekea mahali panapostahili, tulipowaelezea kwenye *version* yetu, lakini bado ipo ardhini, haijanyanyuka na kupaa. Kwa ajili ya watoto wetu, na hatma ya Taifa letu katika utandawazi, lazima sasa tupae. Uchumi wetu unahitaji nguvu mpya, msukumo mpya ili upae. Na nguvu hiyo na msukumo huo si mwingine ila uwekezaji mkubwa zaidi, utakaotoa nafasi nyingi zaidi za ajira, utakaotuwezesha kuuza nje kwa wingi zaidi na utakaoimarisha uchumi wetu na kutoa fursa nyingi zaidi za kila raia aliye tayari ajiendeleze. Tuwe jasiri na tuwe makini. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu akipenda ninayo miezi 20 ya kuongoza nchi yetu. Tusaidianeni ili niache uongozi Tanzania ikiwa inapaa, si ikiwa bado kwenye njia ya kurukia. Inawezekana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waheshimiwa Wabunge mmeisikia hotuba ya Mheshimiwa Rais na Watanzania wote ambao walikuwa wamefungua Redio zao wameisikia kwa sababu ilikuwa inatoka moja kwa moja.

Hali kadhalika Mheshimiwa Rais, amenijulisha kwamba hotuba hii kama haijawekwa tayari itawekwa kwenye *Website* ya Serikali ili Watanzania walioko nchi za nje waweze nao kujua yaliyomo. Kwetu sisi pamoja na kuwa kwenye *Hansard,* lakini vitabu vya hotuba tumekwishakabidhiwa tutawagawia Waheshimiwa Wabunge sasa hivi, ili muweze kuanza kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Ile hotuba yake alipozungumza mara ya mwisho mwaka 2002 nilipomshukuru kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge nilitumia neno la Kiingereza kwamba *it was a powerful speech.* Hii hotuba ya leo ningependa kuieleza kwa maneno yafuatayo kwamba, *it was authoritative, comprehensive and inspiring. (Makofi)*

Mheshimiwa Rais, kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote nikushukuru sana kwa kutenga siku ya leo kuzungumza na sisi na kupitia kwetu na Watanzania wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tumefikia mwisho wa hotuba ya Mheshimiwa Rais. Sasa nitamwomba Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Upinzani, wawasindikize Viongozi wetu waende katika *Speaker's Lounge* wakati mimi naendelea kutoa maelezo mengine. *(Makofi)*

*(Hapa Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliondoka ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitakapositisha shughuli za Bunge hadi jioni, naomba Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge wabaki ndani. Ningeomba Wenyeviti wa Vyama vya Siasa pamoja Katibu Mkuu wa Chama Tawala wabaki hapo walipo nina maelezo ya kuwapa baadaye na ninaomba viongozi wa dini wa madhehebu yale walioalikwa na wao wabaki hapo walipo nina maelezo ya kuwapa baada ya kumaliza shughuli za hapa.

Waheshimiwa Wabunge, niseme tu kwamba kuna wachache miongoni mwetu lakini wengi kidogo waliokuwa wameomba ruksa ya Spika wasiwepo hapa katika Vikao vya Bunge ili waende kuhiji. Sasa nafurahi wote wamesharudi salama wako pamoja nasi tunawakaribisha. *(Makofi)*

*(Hapa Mahujaji husika walisimama)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. Vitabu vitagawiwa pale nje tunapogawia *Order Paper* kwa kawaida, kwa hiyo, tusiwasumbue kubaki ndani ya ukumbi.

**WABUNGE FULANI:** Hapa hapa!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, basi msafara wa Spika ukishatoka subirini hapa hapa mtapewa vitabu vya hotuba ya Mheshimiwa Rais.

*(Saa 06.18 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2003 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2003)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii mchana huu ili niweze kuwasilisha hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Nafarijika sana kwa kufanya hivyo hasa baada ya hotuba nzuri, makini na yenye kutoa matumaini aliyoitoa asubuhi hii Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunampongeza sana ameyasema yote mazuri kwa niaba ya Watanzania na kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2003 yaani *The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 2) Bill, 2003,* sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya mabadiliko katika sheria mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya kwanza ni Sheria ya Mchezo wa Bahati Nasibu ya mwaka 2003 yaani *The Gaming Act (No.4) of 2003.* Sheria ya pili ni Sheria ya Milipuko ya mwaka 1963 yaani *Explosives Act 1963.* Sheria ya tatu ni *The Penal Code* sura namba 16 ya sheria za Tanzania yaani Sheria ya Kanuni za Adhabu. Sheria ya nne ni Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai ya Mwaka 1985. Sheria ya tano ni Sheria ya Mahakama ya Mahakimu ya Mwaka 1984 yaani *The Magistrate Courts Act.* Sheria ya sita ni Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa yaani *The Political Services Retirement Benefits Act of 1999.* Sheria ya saba ni Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma yaani *The Public Service Retirement Benefits Act of 1999* na Sheria ya nane ni Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 yaani *The Mining Act No. 20 of 1998.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria nyingine katika Muswada huu ni zile zinazokusudiwa kufutwa ambazo ni kama ifuatavyo:-

Sheria ya Baraza la Taifa la Tija ya Mwaka 1981 yaani *The National Protectivity Council Act of 1981.* Sheria ya Chuo cha Uandishi wa Habari ya Mwaka 1981 *(The Tanzania School of Journalism Act of 1981)* na mwisho ni Sheria ya Shirika la Ukaguzi wa Hesabu Tanzania yaani *The Tanzania Audit Corporation Act of 1968.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya kwanza inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Michezo ya Bahati Nasibu ya Mwaka 2003. Sheria hii baada ya kupitishwa na Bunge lako Tukufu imegundulika kwamba kuna sheria nyingine ya Bahati Nasibu ambayo bado haijafutwa. Hii ni Sheria ya

Michezo ya Kamari ya Mwaka 1923 yaani *The Gumbling Ordinance of 1923.* Hivyo marekebisho haya yanapendekeza kufutwa kwa sheria hiyo ya mwaka 1923 kupitia kifungu cha 86 cha Sheria ya Michezo ya Bahati Nasibu ya mwaka 2003 ili michezo yote pamoja na hii michezo ya Kamari isimamiwe na sheria moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya pili inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Milipuko ya mwaka 1963 yaani *The Explosives Act of 1963.* Sheria hii inafanyiwa marekebisho ili kuweka utaratibu madhubuti wa kudhibiti na kusimamia matumizi ya milipuko inayoingizwa nchini. Ili kukidhi hitaji hili kifungu cha 16 kinachomtaja mwingizaji wa milipuko nchini kufanya marejesho pale ambapo ametakiwa kufanya hivyo na Kamishna wa Madini kinafanyiwa marekebisho katika kifungu kidogo cha 4 (c) ili muingizaji wa milipuko awajibike kufanya marejesho ya matumizi ya milipuko kila mwezi badala ya kungojea utashi wa Kamishna wa Madini kama ilivyo katika sheria hivi sasa. Utaratibu huu utasaidia kufuatilia kwa karibu milipuko inayoingizwa nchini na pia matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya tatu inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Kanuni za Adhabu sura ya 16 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano. Katika kutekeleza sheria hii inayotoa ufafanuzi na vigezo vya makosa mbalimbali ya jinai imeonekana kwamba makosa ya ujambazi wa kutumia silaha yaani *(Armed robbery)* na makosa ya kujaribu kutenda kosa la ujambazi kwa kutumia silaha yaani *(Attempted armed robbering)* haijapewa tafsiri au vigezo dhahiri. Hali hii imesababisha utata kuhusu vigezo vinavyotumika katika kuthibitisha makosa haya dhidi ya mshtakiwa Mahakamani. Hivyo ili kuondoa utata huu inapendekezwa kuongeza vifungu vipya vya 287(a) na 287(b) ili kutoa tafsiri ya kosa la ujambazi kwa kutumia silaha pamoja na kujaribu kutenda kosa la ujambazi kwa kutumia silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya 4 inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ya mwaka 1985. Sheria hii inafanyiwa marekebisho katika jedwali la kwanza ambalo pamoja na mambo mengine linaainisha makosa mbalimbali na Mahakama zinazohusika kwa ajili ya makosa hayo. Katika utekelezaji wa sheria hii imegundulika kwamba yapo makosa ya kawaida ambayo yangeweza kusikilizwa na Mahakama za chini japo kwa sasa makosa hayo yameainishwa kusikilizwa na Mahakama Kuu.

Hali hii imekuwa ikichangia katika mlundikano wa kesi usio wa lazima katika Mahakama Kuu. Ili kupunguza mlundikano huu inapendekezwa jedwali la kwanza la sheria hii ifanyiwe marekebisho ili makosa yaliyoainishwa katika Muswada huu yakiwemo makosa ya kutishia kuua *(sending written of rights to murder),* makosa ya kujamiiana kwa maharimu *(incent by male and incent by females)* na kujaribu kuua *(attempting murder)* yawezwe kusikilizwa na Mahakama za chini badala ya Mahakama Kuu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya tano inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria za Mahakama za Mahakimu ya mwaka 1984. Sheria hii inafanyiwa marekebisho ili kuweka mipaka ya Mamlaka ya Mahakama za Mahakimu katika kushughulikia Mashauri ya Biashara. Sheria hii itakumbukwa kwamba ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2002 yaani *The Written Laws Miscellaneous Amendments Act No. 25 of 2002.* Ili kuongeza wigo wa Mamlaka *(jurisdiction)* ya Mahakama hizo. Kwa mujibu wa marekebisho hayo Mahakama za Mahakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya zinazoongozwa Mahakimu Wakazi zimepewa mamlaka kushughulikia kesi zote ambazo thamani ya mali zinazohamishika yaani *immoveable properties* haizidi shilingi 100,000,000 na kesi nyingine ambazo thamani ya mali zisizohamishika yaani *moveable properties* haizidi shilingi 150,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba mwaka 1999 Mahakama ya Biashara ilianzishwa chini ya Kanuni za Mahakama Kuu yaani *The High Courts Registries Amendments Rules 1999* ili kushughulikia kesi zote za biashara. Marekebisho yaliyofanyika mwaka 2002 kwenye Sheria ya Mahakama za Mahakimu imeziwezesha Mahakama za Mahakimu Wakazi kushughulikia kesi nyingi za biashara jambo ambalo linaanza kuonekana linaipunguzia sana kazi Mahakama ya Biashara na hivyo kuiathiri Mahakama hiyo kimapato kinyume kabisa na madhumuni ya Serikali ya kuanzisha Mahakama ya Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na hali hii inapendekezwa Sheria ya Mahakimu ya Mwaka 1984 ifanyiwe marekebisho kama ifuatavyo:-

Katika kifungu cha 2 kinachotoa tafsiri ya maneno yanayotumika katika sheria hiyo inapendekezwa kuingiza tafsiri mpya ya maneno kesi ya biashara *(commercial cases)* ndani ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu ya mwaka 1984. Pia inapendekezwa katika kifungu cha 40 cha sheria hiyo kinachofafanua mamlaka za Mahakama za Mahakimu Wakazi ili kuongeza kipengele kitakachopunguza wigo wa mamlaka za Mahakama hizo katika kushughulikia kesi za biashara.

Kwa mujibu wa mapendekezo haya Mahakama za Mahakimu Wakazi zitakuwa na mamlaka za kushughulikia fedha za biashara zinazohusu mali inayohamishika yenye thamani isiyozidi shilingi 30,000,000 badala ya shilingi 100,000,000 na kesi za biashara zinazohusu mali isiyohamishika yenye thamani isiyozidi shilingi 50,000,000 badala ya shilingi 150,000,000. Hata hivyo ili kuzuia mlundikano wa kesi katika Mahakama ya Biashara inapendekezwa rufaa za kesi za biashara kutoka Mahakama za Wilaya ziendelee kusikilizwa na Mahakama Kuu kama ilivyo hivi sasa. Kwa maneno mengine Mahakama ya Biashara kwa sasa haitakuwa na *appelate jurisdiction* yaani mamlaka ya kusikiliza Rufaa zinazohusu kesi za biashara kutoka Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya sita inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999. Hali ilivyo sasa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanatambuliwa kisheria kama Viongozi wa Kisiasa chini ya Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya Mwaka 1999 *(The Political Service Retirement Benefits Acts of 1999)* ambayo imetoa tafsiri ya neno Kiongozi *(Leader)* kwa kujumuisha Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

Pamoja na kutambuliwa kama Viongozi wa Kisiasa Sheria hii ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa haikuweka utaratibu wa mafao yao kama ilivyofanya kwa viongozi wengine wa kisiasa na badala yake inatamka bayana kuwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya walipwe mafao yao ya hitimisho la kazi chini ya Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 1999 yaani *The Public Service Retirement Beneficts Acts of 1999.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imekuwa ikileta utata na malalamiko kuhusu hadhi halisi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya chini ya sheria hizi mbili. Ili kuondoa utata huu inapendekezwa Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya Mwaka 1999 ifanyiwe marekebisho kwa kufuta kifungu cha 23 kinachoweka utaratibu wa mafao ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya chini ya Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 na kuweka kifungu kipya kinachoweka utaratibu mpya wa ulipaji wa mafao kwa viongozi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya utaratibu unaopendekezwa kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa marekebisho haya Wakuu wa Mikoa au Wakuu wa Wilaya watakapostaafu au kuacha kazi kama Wakuu wa Mikoa au Wakuu wa Wilaya kama ilivyo kwa viongozi wengine wa kisiasa walipwe mafao yao chini ya Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999.

Hata hivyo Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya aliyekuwa mtumishi wa umma kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya atahesabiwa kuwa amechukua likizo bila malipo kama mtumishi wa umma na pindi atakapokuwa amestaafu au kuacha kazi ya Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya kabla hajafikia umri wa kustaafu na wala hakusudii kurudi tena kwa mwajiri wake au atakayefikia umri wa kustaafu kwa lazima.

Basi Mkuu huyu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya atalipwa mafao yake chini ya Sheria ya Mafao ya Utumishi wa Umma au sheria nyingine inayotawala ajira yake kama Mtumishi wa Umma na kipindi alichofanya kazi kama Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya kitazingatiwa katika kuandaa mafao yake yaani kipindi alichotumikia katika wadhifa huo wa uongozi kitaunganishwa na kipindi chake cha utumishi wa huko nyuma kwa madhumuni ya kupiga mahesabu ya mafao yake. Utaratibu huu umeainishwa bayana katika kifungu cha 7 kama kilivyorekebishwa mwaka 2000 cha Sheria ya Mafao ya Viongozi ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, inapendekezwa kuwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya waliokuwa kazini kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa marekebisho haya mara baada ya tarehe ya kutumika kwa marekebisho haya watalipwa mafao yao kwa utumishi wao wa nyuma hadi tarehe hiyo chini ya Sheria ya Mafao ya Viongozi wa mwaka 1981 kwa kuzingatia mazingira ya ajira kama ifuatavyo:-

(a) Mkuu wa Mkoa aliyekuwa Mtumishi wa Umma kabla ya kuteuliwa kwake kuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa kWilaya atalipwa mafao ya ama pensheni au *gratuity* yatakayoandaliwa chini ya Sheria ya Mafao ya Viongozi ya mwaka 1981 kwa kipindi alichofanya kazi kama Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya mpaka tarehe ya kuanza kutumika kwa marekebisho haya na mshahara wake kama Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya tarehe hiyo yaani tarehe ya marekebisho hayo kuanza kutumika utatumika katika kuandaa mafao yake chini ya sheria hiyo kwa kipindi cha nyuma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Mkoa aliyekuwa kazini kabla ya tarehe ya kuanza kutumika kwa marekebisho haya na ambaye hakuwahi kuwa Mtumishi wa Umma mafao yake kwa kipindi cha nyuma alichokuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya mpaka tarehe ya kuanzia kutumika kwa marekebisho haya yatalipwa chini ya Sheria ya Mafao ya Viongozi ya mwaka 1981 na mshahara wake kwa tarehe hiyo kama Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya utazingatiwa katika kuandaa mafao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya saba ni Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 yaani *The Public Service Retirement Benefits Acts of 1999.* Sheria hiyo inafanyiwa marekebisho sambamba na marekebisho yaliyopendekezwa katika Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya Mwaka 1999 kifungu cha 20(7) kinachoweka masharti ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya chini ya sheria hii kinafutwa ili mafao ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya yashughulikiwe kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa chini ya Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya Mwaka 1999 badala ya kushughulikiwa kama ilivyo hivi sasa chini ya Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya nane inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Madini ya mwaka 1998 *(The Mining Act of 1998).* Sheria hii inafanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji mbalimbali yaliyojitokeza katika utekelezaji wa sheria hii. Mahitaji haya ni pamoja na yale yanayohusu udhibiti wa shughuli za madini. Adhabu kwa atakayeshindwa kulipa malipo ya mrahaba *(royalty),* Kuundwa kwa Bodi ya Ushauri ya Madini ya Vito *(The Gemstones Board),* kiwango cha malipo ya mrahaba kwa madini ya vito na ufafanuzi wa maneno mbalimbali ni baadhi tu ya mambo muhimu yanayopendekezwa katika Muswada huu. Kwa ujumla mapendekezo haya yanajitokeza katika vifungu mbalimbali kama ifuatavyo.

Kwanza, kifungu cha 4 cha Sheria ya Madini kimefanyiwa marekebisho ili kujumuisha fafanuzi mbalimbali za maneno yatakayotumika kwa mujibu wa mapendekezo haya.

Pili, kifungu cha 9 kinachohusu kuhamisha haki ya madini *(Mineral Rights)* kinafanyiwa marekebisho kuongeza kifungu kidogo cha 6 kinachoweka utaratibu wa maombi kwa ajili ya kuhamisha leseni za uchimbaji *(The Primary Mining Licenses).* Kwa mujibu wa mapendekezo haya maombi haya yatafanyika katika fomu maalum zitakazoandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini.

Tatu, inapendekezwa kuongezwa kifungu kipya cha 14(a) kwa madhumuni ya kumwezesha Waziri mwenye dhamana ya madini kuteua aina yoyote ya vito ili madini hayo yaweze kusanifiwa pale ambapo wataona kwamba kufanya hivyo kutakuwa ni kwa manufaa ya maendeleo ya viwanda vya vito nchini.

Nne, kifungu cha 15 kinachohusu makosa yanayohusu biashara ya madini kinafanyiwa marekebisho ili makosa hayo yahusu madini ya aina zote badala ya kutaja madini ya dhahabu na vito peke yake kama ilivyo kwenye sheria hivi sasa. Aidha, kifungu kidogo cha 5 kinachompa mamlaka Waziri kuongeza aina ya madini yatakayohusika na makosa chini ya kifungu hiki kinafutwa maana hakihitajiki tena baada ya kupendekezwa kuwa makosa hayao yahusu madini ya aina zote.

Tano, kifungu cha 16 kinachohusu uteuzi wa Kamishna wa Madini kinafanyiwa marekebisho katika kifungu kidogo cha 4 ili kuongeza uteuzi wa kada mpya ya watendaji wakiwa chini ya sheria hiyo. Watendaji hawa watafahamika kama Maafisa wa Madini wa Mikoa *(Residents Mines*

*Officers).* Kwa mujibu wa mapendekezo haya mbali na Maafisa Madini wa Kanda kutakuwepo Maafisa Madini wa Mkoa.

Sita, kifungu cha 18 kinachohusu huduma za miamba *(Geological services)* kinafanyiwa marekebisho katika maneno ya awali ili utekelezaji chini ya kifungu hiki umhusu na mtu mwingine atakayeteuliwa na Waziri badala ya kuwa Kamishna wa Madini peke yake kama ilivyo kwenye sheria ya hivi sasa. Mapendekezo haya yanakusudia kurahisisha utekelezaji wa majukumu haya pale ambapo Kamishna wa Madini atakuwa hayupo.

Saba, kifungu kipya cha 20(a) kinapendekezwa ili kuunda Bodi ya Ushauri Kuhusu Madini ya Vito *(The Gemstones Board)* itakayomshauri Waziri juu ya mambo yote yanayohusu shughuli za madini ya vito nchini.

Nane, kifungu cha 28 kinafanyiwa marekebisho madogo ili kusahihisha makosa ya uchapishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, kifungu cha 29 cha Sheria ya Madini kinachohusu utoaji, muda wa leseni na maombi ya kuhuisha leseni *(The Grant of Licenses, Duration and Renewal Prospecting Licences)* kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha 1(a) kitakachoweka utaratibu wa kuwasilisha maombi ya leseni chini ya kifungu hiki. Chini ya mapendekezo haya mtu mwenye leseni iliyokwisha muda wake atatakiwa kuwasilisha maombi ya leseni katika kipindi cha miezi mitatu kabla ya tarehe ya kumalizika kwa muda wa leseni aliokuwa nayo.

Aidha, kifungu hiki kinafanyiwa marekebisho kwa madhumuni ya kuongeza kifungu kidogo kipya cha 3(a) kinachoweka utaratibu wa kutangaza maeneo yaliyoachwa yaani *relinquished areas* ili yatolewe upya.

Kwa mujibu wa mapendekezo haya maeneo yaliyoachwa yatatangazwa kila mwezi na kuwekwa kwenye ubao wa matangazo yaani notice board kwa Makao Makuu ya Wizara ya Madini, Ofisi za Madini za Kanda na Ofisi za Madini za Mkoa ili kila mtu ajue kwamba kuna maeneo yaliyo wazi ambayo yanaweza yakaombewa leseni. Utaratibu huu utawezeshwa wahusika kujua maeneo yaliyoachwa.

Kumi, kifungu cha 30 cha Sheria ya Madini kinachohusu utoaji wa taarifa wa leseni zinazotolewa kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta vipengele vidogo katika kifungu kidogo cha kwanza na kuweka vipengele vipya vinavyoweka muda maalum wa utoaji taarifa chini ya kifungu hiki. Hivyo mwombaji aliyepata taarifa kuhusu kupewa kwake leseni atatakiwa kutoa taarifa ya kukubali leseni aliyopewa na kuilipia ndani ya muda wa wiki nne. Utaratibu huu utasaidia kuondoa waombaji wanaochelewa kulipia leseni au wanaoshikilia maeneo bila ya kuyafanyia kazi iliyokusudiwa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na moja, kifungu cha 57 kinachohusu kusitisha na kufuta haki ya madini *(Suspension and Cancellation of Mineral Rights)* kinafanyiwa marekebisho kwa kuondoa kipengele cha (a) kinachohusu kosa la kushindwa kulipa malipo ya mrahaba ili sasa makosa hayo yashughulikiwa kipekee chini ya kifungu kipya cha 57(a).

Kumi na mbili, Sheria hii inafanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 57(a) kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho. Chini ya kifungu hiki mwenye leseni ya kuchimba madini atakayeshindwa kulipa mrahaba atatakiwa kulipa malipo ya adhabu mbali na malipo ya mrahaba anayodaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tatu, kifungu cha 72 kinachohusu kufutwa *Primary Prospecting Licence* kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya 2, 3 na 4 vinavyoweka utaratibu utakaozingatiwa kabla ya Kamishna wa Madini kufikia uamuzi wa kufuta leseni chini ya kifungu hiki pamoja na haki ya rufaa dhidi ya uamuzi uliotolewa.

Chini ya utaratibu huu, mwenye leseni atapelekewa ilani ya kusudio la kufutwa kwa leseni na atatakiwa kujibu ilani hiyo katika muda uliopangwa. Lengo ni kuhakikisha yamefanyika mawasiliano na wenye leseni kabla ya leseni yake kufutwa. Kifungu kidogo cha nne ambacho kiko kwenye jedwali la

marekebisho kinamwezesha mtu asiyeridhika na uamuzi wa Kamishna wa kumfutia leseni kuwasilisha rufaa yake kwa Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rekebisho la 15, sehemu ya 5 ya sheria hii inafanyiwa marekebisho kwenye kichwa cha habari kwa kuondoa maneno yanayotamka baadhi ya madini na kuweka maneno yanayojumuisha madini ya aina zote. Marekebisho hayo yatawezesha sehemu hii kushughulikia madini ya aina zote badala ya kushughulikia baadhi tu ya madini yaani dhahabu na vito. Mapendekezo hayo yako kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rekebisho la 16, kifungu cha 73 kinachohusu maombi ya *dealer's licence* kinafanyiwa marekebisho ili kuliondoa jukumu la kupokea maombi ya leseni za aina hiyo kutoka kwa Waziri wa Madini na badala yake kuhamishia shughuli hizo kwa Kamishna wa Madini kupitia kwa Maafisa wa Kanda au wa Mikoa. Kifungu kidogo cha pili kimeondolewa na kuweka kifungu kipya ili kumwezesha mwombaji wa leseni ataje aina ya madini yatakayohusika chini ya leseni yake. Aidha, kifungu kidogo kipya cha tatu kimependekezwa ili kumtaka mwombaji wa leseni ya kujihusisha na vito kuonyesha uwezo wake wa kusanifisha vito *(capacity to undertake lapidary).* Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha leseni zinatolewa kwa kuzingatia aina ya madini inayohusika na uwezo wa mwombaji katika kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 17 ni kwenye kifungu cha 75 cha Sheria ya mMadini kinachohusu muda wa maombi ya leseni *(duration and renewal of dealer's licence).* Kifungu hiki kinafanyiwa marekebisho ili kupunguza muda wa ukomo na uhuishaji wa leseni za namna hiyo *(dealer's licence).* Mapendekezo haya ambayo yanaonekana katika kifungu kidogo cha kwanza, cha tatu na cha nne yanapunguza muda huo kutoka miezi 15 kwenda miezi 12, kutoka miezi 12 kwenda miezi 10 na kutoka miezi 15 kwa kuhuisha na kuwa miezi 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya 18 ni kifungu cha 76 kuhusu haki za mwenye *dealer's licence* kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu kidogo cha pili kwani kifungu hiki kidogo hakihitajiwi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya 19 ni kwamba, kifungu cha 78 kinachoweka kiwango cha marejesho kinafanyiwa marekebisho kwa kupunguza muda wa kufanya marejesho kutoka miaka mitatu kwenda miaka miwili kwani muda huo unaonekana ni mrefu mno kwa mwenye leseni kutowasilisha taarifa za ununuzi wa madini. Hivyo, mtu yeyote aliyepewa *dealer's licence* atakayeshindwa kufanya marejesho katika kipindi cha miaka miwili mfululizo chini ya mapendekezo haya hataruhusiwa kupata leseni mpya baada ya leseni yake kuisha muda wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rekebisho la 20, kifungu cha 86 cha Sheria ya Madini kinachohusu mrahaba kinafanyiwa marekebisho kwa kuongezwa vipengele vipya vya (b) na (c) katika kifungu kidogo cha kwanza, vinavyoweka viwango vya malipo ya mrahaba kwa madini ya aina ya vito yanayosafishwa kwenda nje ya nchi.

Tozo la asilimia 5 linapendekezwa kwa vito vinavyosafirishwa nje ya nchi ambavyo havijasanifiwa *(Unpolished Gemstones).* Inapendekezwa vito vilivyosanifiwa *(polished gems)* vitakavyouzwa nje ya nchi visitozwe mrahaba. Ni imani ya Serikali kwamba, hatua hii itakuwa chachu ya kusanifu madini ya *Tanzanite* na aina nyingine ya vito hapa nchini na hivyo kuwezesha madini hayo kuhimili ushindani katika soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la kwanza katika Sheria ya Madini linalohusu Kamati ya Ushauri ya Madini linafanyiwa marekebisho ili kuhakikisha Waziri wa Madini anapotumia madaraka yake ateue Mtaalam wa Madini katika Kamati hiyo *(Mining Advisory Committee).*

Mheshimiwa Naibu Spika, rekebisho la mwisho kwenye sheria hii, jedwali la tatu linalohusu taarifa, nalo linafanyiwa marekebisho kwa kufuta kipengele cha (b) na kuweka kipengele kipya kitakachomtaka mwenye leseni kuwasilisha taarifa katika muda unaoonyeshwa kwenye jedwali la marekebisho yaani mwezi wa kwanza wa kila robo mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, sheria nyingine katika Muswada huu ni zile zinazokusudiwa kufutwa kama ifuatavyo: -

Kwanza, Sheria ya Baraza la Tija ya Mwaka 1981 *(The National Productivity Council of 1981).* Inapendekezwa kufutwa kwa kuwa sheria hii haihitajiki tena baada ya kuonekana kwamba shughuli chini ya sheria hii zinatekelezwa na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Pili ni Sheria ya Chuo cha Uandishi wa Habari *(The School of Journalism Act of 1981).* Inapendekezwa ifutwe maana nayo haihitajiki tena baada ya Chuo hicho kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sheria ya tatu na ya mwisho ni Sheria ya Shirika la Ukaguzi wa Hesabu Tanzania *(The Tanzania Audit Cooperations Act of 1968)* iliyoanzisha Shirika la Ukaguzi wa Hesabu *(Tanzania Audit Cooperation)* nayo inapendekezwa kufutwa.

Kufuatia Sera ya Taifa ya Ubinafsishaji, Shirika hilo lilibinafsishwa ili kuondoa ukiritimba uliokuwepo na kuleta ushindani katika huduma ya ukaguzi wa hesabu hapa nchini. Baada ya shughuli za Shirika hili kuchukuliwa na Chombo kingine cha Wataalam wa Hesabu *(TAC Associates)* sheria hii iliyounda Shirika la Ukaguzi wa Hesabu haihitajiki tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Naibu wake na mtani wangu, Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo, kwa uchambuzi wao wa kina na ushauri mzuri waliotoa kuhusu maudhui ya Muswada huu. Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kutambua mchango na ushauri mzuri uliotolewa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, katika eneo la Muswada huu linalohusu Sheria ya Madini hususan ushauri wake wa kuiomba Serikali iweke utaratibu mzuri na masharti yatakayohakikisha ukataji na uuzaji wa madini ya vito hapa nchini kwa lengo la kuongeza Pato la Taifa kutokana na madini hayo kuwa yamesanifiwa kabla ya kusafirishwa kwenda nchi za nje. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu na kuupitisha pamoja na marekebisho kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho yanayoendana na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia napenda nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa leo asubuhi. Hotuba ambayo imetukumbusha majukumu yetu kama wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, sasa napenda niwasilishe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2003 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2003).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, napenda kushukuru kwa kutupatia fursa ya kuchangia kwenye Muswada huu kuwa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2003 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2003).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unalenga kufanya marekebisho katika sheria zifuatazo: -

(i) Sheria ya Michezo ya Bahati Nasibu ya Mwaka 2003 *(The Gaming Act, 2003);*

(ii) Sheria ya Milipuko ya Mwaka 1963 *(The Explosive Act, 1963);*

(iii) Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 *(The Penal Code Cap. 16);*

(iv) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ya Mwaka 1985 *(The Criminal Procedure Act, 1985);*

(v) Sheria ya Mahakama ya Mahakimu ya Mwaka 1985 *(The Magistrates Court Act, 1985);*

(vi) Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya Mwaka 1999 *(The Political service Retirement Benefits Act, 1999);*

(vii) Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 1999 *(The Public Service Retirement Benefits Act, 1999);*

(viii) Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 *(The Mining Act, 1998);*

(ix) Kufutwa kwa Sheria ya Baraza la Tija ya Mwaka 1981 *(The National Productivity Council Act, 1981);*

(x) Sheria ya Chuo cha Uandishi wa Habari ya Mwaka 1981 *(The Tanzania School of Journalism, 1981);* na

(xi) Sheria ya Shirika la Ukaguzi wa Hesabu Tanzania ya 1968 *(The Tanzania Audit Cooperation Act, 1968).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imetekeleza kazi hiyo na sasa kwa mujibu wa Kanuni namba 70, kifungu cha pili cha Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2003, naomba kutoa maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

Katika Muswada wa Sheria ya Milipuko, Kamati imekubaliana na mapendekezo yanayotolewa ili kuweka utaratibu mpya wa kudhibiti na kusimamia uuzaji na matumizi ya milipuko inayoingizwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Muswada wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Kamati yangu inakubaliana na mapendekezo yanayotolewa kwa kuweka tafsiri ya ujambazi kwa kutumia silaha ili kuondoa utata uliokuwa ukijitokeza kwa kukosekana kwa tafsiri hiyo katika sheria kama ilivyo sasa.

Hata hivyo, Kamati imepata wasiwasi wa mapendekezo ya adhabu kwa kosa la jaribio la ujambazi kwa kutumia silaha miaka 15 wakati jaribio hilo likifanikiwa ni adhabu ya miaka 30. Kwa upande mwingine, Kamati haioni umuhimu wa kuongeza adhabu ya viboko kwa makosa hayo yaliyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufafanuzi wa kina kutoka kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati iliafikiana na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Mwenendo wa Mashauri wa Jinai, Kamati inapongeza mapendekezo yanayotolewa kwa kuwezesha Mahakama za Chini kushughulikia baadhi ya kesi ambazo zilikuwa zinashughulikiwa Mahakama Kuu pekee. Kamati inatoa pongezi hizo kutokana na ukweli kwamba Mahakama Kuu zimekuwa na kesi nyingi hivyo kusababisha ucheleweshwaji katika kukamilishwa kwa kesi hizo, hivyo kusababisha mlundikano wa mahabusu katika magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada wa Sheria ya Mahakama ya Mahakimu, marekebisho yanafanyika kupunguza wigo wa Mahakama hizo katika kushughulikia kesi za biashara, Kamati yangu inaafiki mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sheria ilivyo sasa, kesi zote za madai ambazo thamani ya mali zinazohamishika hazizidi shilingi milioni 100 na mali zisizohamishika thamani isiyozidi shilingi milioni 150 zimekuwa zikishughulikiwa na Mahakama hizi, hivyo imebainika kwamba Mahakama ya Biashara haipati kesi za kutosha na mapato yake yanazidi kupungua. Hata hivyo, Kamati yangu inashauri kuwa, sheria itoe uhuru *(flexibility)* ya mtu kuamua kupeleka kesi yake Mahakama ya Kawaida au Mahakama ya Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatokana na ukweli kuwa Mahakama ya Biashara iko Dar es Salaam tu, hivyo utekelezaji wa sheria hii usiongeze gharama kwa Wananchi na kusababisha washindwe kufuatilia haki zao. Aidha, tahadhari ichukuliwe ili utekelezaji wa marekebisho haya usihamishie mlundikano wa kesi kutoka Mahakama za Kawaida kwenda Mahakama ya Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada wa Sheria ya Madini, Kamati yangu kimsingi inakubaliana na mapendekezo yanayotolewa na Serikali, isipokuwa lile lililopo katika kipengele (c) cha Muswada huo. Kipengele hiki kinafuta kifungu cha 12 (2) cha Sheria ya Madini kuweka kifungu kipya. Kifungu hiki kipya kinaondoa Mamlaka ya Waziri kutumia busara zake katika kuamua nani apewe kipaumbele pale inapotokea maombi zaidi ya moja ya kibali cha uchimbaji wa madini yamepokelewa kwa wakati mmoja. Badala yake yanatolewa mapendekezo kuwa, inapotokea hali kama hiyo, maamuzi yatolewe kwa kufuata bahati nasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu haiamini kuwa tumefikia hatua hiyo ya kukosa imani kwa Mawaziri wetu hadi tuingize michezo ya bahati nasibu. Hivyo, Kamati haiafiki mapendekezo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele (r) cha Muswada kinahusu mrahaba kwa aina mbalimbali za madini. Kamati inaona kuwa, viwango vinavyotozwa kama mrahaba ni vidogo ukilinganisha na faida inayopatikana. Aidha, Kamati inashauri utafiti ufanyike kwa nchi nyingine kuhusu suala hili la viwango vya mrahaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada wa Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa inapendekezwa kuwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wahamishiwe katika sheria hii ili walipwe mafao kama Viongozi wa Kisiasa *(Political Leaders)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu haina kipingamizi kwa mafao ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kushughulikiwa namna ya Viongozi wa Kisiasa kwa mujibu wa sheria husika *(Political Service Retirement Benefits Act, 1999)* kwani hata tafsiri ya Viongozi wa Kisiasa chini ya sheria hii inawahusisha wao pia.

Hata hivyo, Kamati haikubaliani na mapendekezo yanayotolewa katika kifungu kipya cha 23(2) ambacho kinaeleza kwamba: "Mtumishi wa umma anayeteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya inapofikia wakati anakoma kuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya atakuwa na uhuru wa kuchagua kama mafao yake yashughulikiwe kama watumishi wengine wa umma *(The Public Servants)* au kama Kiongozi wa Kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu haioni mantiki ya kutoa *option* ya namna hiyo. Sheria ni lazima iwe na mwelekeo. Kama ni Kiongozi wa Kisiasa ni vema masuala yote yafuate kanuni, sheria na taratibu za Viongozi wa Kisiasa. Hivyo, Kamati inashauri kuwa, kifungu hicho kifanyiwe marekebisho ili suala la *option* lisiwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekubaliana na ushauri huu wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru tena wewe kwa kunipatia nafasi hii na pia nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake kwa ushirikiano, maelekezo na ufafanuzi mzuri alioutoa kwa Kamati yangu wakati wa kujadili Muswada huu. *(Makofi)*

Aidha, kwa namna ya pekee, niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa michango yao ya kina iliyowawezesha kuboresha Muswada huu na napenda niwatambue Wajumbe wa Kamati hii, nao ni Mheshimiwa Athumani Janguo - Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombare-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mwanne Mchemba na Mheshimiwa Rosemary Nyerere. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ramadhan Khalfan, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimiwa Ruth Msafiri. *(Makofi)*

Michango yao ya kina ndiyo imesaidia kuboresha Muswada huu. Kwa hiyo, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru na kuwapongeza Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Nenelwa Mwihambi, Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Charles Mloka, kwa kazi nzuri ya kuihudumia Kamati hii ikiwa ni pamoja na uandishi sahihi wa maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA - MSEMAJI WA KAMBI UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi zangu na za Kambi ya Upinzani kwako pamoja na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kumaliza mwaka wa 2003 na kuteuliwa na Mwenyezi Mungu kuingia katika mwaka huu wa 2004 kwa kishindo na kwa afya njema. Ninawatakia nyote baraka na fanaka tele kwa yote mtakayoyafanya katika mwaka huu wa 2004 hasa katika kazi kubwa na ngumu ya kuwahudumia wapigakura wetu katika maeneo yetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nazungumza pia kwa niaba ya Kambi, baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake. Nisingependa kusema kwa saa hizi kama ninaiunga mkono, lakini labda nitoe ombi na nitegemee kwamba hotuba ya Rais katika uzito wake mkubwa bila shaka itapangiwa nafasi ya kujadiliwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam za Kambi ya Upinzani, naomba sasa nichukue fursa hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada ulio mbele yetu yaani Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali. Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni yake katika maeneo machache kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 *(The Penal Code Cap. 16),* Kambi ya Upinzani inaelewa nia na lengo la kuongeza kipengele kipya cha 287 (a) na 287 (b) kinachotoa ufafanuzi na vigezo vya kosa la ujambazi kwa kutumia silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa vipengele hivi ni muhimu kuondoa utata kuhusu vigezo vinavyotumika kuthibitisha kosa la ujambazi wa kutumia silaha *(armed robbery)* pamoja na *attempted robbery.* Vipengele hivi pia ni muhimu kutokana na hali iliyojitokeza hivi karibuni ya ujambazi na hasa ujambazi wa kutumia silaha na hivyo kuondoa mazingira ya amani, usalama wa Wananchi na mali zao. Hivyo, kwa hili tunaipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kambi ya Upinzani inatoa tahadhari kubwa kuwa ni vyema vipengele hivi vikatumika kwa uangalifu mkubwa sana kwani kwa upande mmoja tuna lengo na nia ya kutaka kuondoa tatizo la msingi, lakini bila vyombo vyetu husika kutumia uangalifu na busara katika matumizi ya vipengele hivi tutahalalisha Wananchi wengi wasio na kosa wakati wa msukosuko bila sababu. Tunazo taarifa nyingi za kesi za matumizi ya silaha ambazo zimebambikizwa na Wananchi wasio na makosa wakapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, kesi ya namna hiyo imetokea Mkoani Arusha kwa mfano mmoja tu ninaoutoa kwa bwana anayeitwa Juma Galle, ambaye ametungiwa kesi ya silaha, akakamatwa na kuwekwa rumande mara tatu na kila wakati kukaa ndani kwa zaidi ya siku 60 na hatimaye kwa kila mara kuachiwa na Mahakama kwa kuwa upande wa mashtaka haukuwasilisha ushahidi Mahakamani. Hakuna ukaguzi wa nyumba uliofanyika na hata *parade* iliyotakiwa kufanyika ilifanywa na watu waliopandikizwa. Hatimaye imegunduliwa kuwa mhusika amebambikiziwa kesi hii kwa mlalamikaji kula njama na Polisi kwa vile tu mlalamikaji amegombania mwanamke na mtuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lisiloeleweka wala lisilo na mantiki kwa mwananchi asiye na kosa kukaa rumande kwa siku zaidi ya 180 katika vipindi vitatu tofauti na hatimaye kuachiwa. Mheshimiwa Waziri ana taarifa ya kesi hiyo. Malalamiko ya aina hiyo pia yametokea sehemu mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo Tarime, Serengeti na sehemu nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukubalika rekebisho hilo, ni vema mazingira ya kumkamata mtuhumiwa, taratibu zinazotakiwa yaani upekuzi wa nyumba au mazingira husika na *parade* ya utambuzi yakaangaliwa vizuri. Pia, ni vema maadili ya Maaskari wetu ambao wengi kimsingi wanafanya kazi nzuri yakawekwa vizuri ili wachache wasipate nafasi ya kutumia kipengele hiki vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe, tafsiri ya maneno *dangerous or offensive weapon* haiko wazi kwani panga, kisu kikali na mikuki, vyote ni silaha za hatari na taratibu za mila zetu zinajulikana na baadhi ya silaha hizo zinatumika pia kwa matumizi mazuri ikiwa ni pamoja na matumizi ya nyumbani. Ni imani yetu kuwa matumizi sahihi yatatumika vinginevyo ukimbambikiziwa kesi ya aina hiyo na ulikuwa na sime tu ukaishia kufungwa kifungo kisicho chini ya miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inapenda kutoa maoni yake katika Marekebisho ya Sheria Namba 3 ya 1999 *(The Political Service Retirement Benefits Act, 1999).* Katika kipengele hiki, kimsingi tunakubaliana na wenzetu wa Kamati kwa sababu na sisi ni Wajumbe, lakini tungependa kutoa pia tahadhari zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele hiki ambacho kinapendekeza Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya wapate maslahi kama walivyo Viongozi wa Kisiasa, Kambi ya Upinzani inaona si vema Viongozi hao ambao kimsingi si wa kuchaguliwa kuingizwa katika kundi la Viongozi wa Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wa siasa ni wale wenye dhamana kutokana na kuchaguliwa na Wananchi na Viongozi wa Kuteuliwa si vema wakawa kwenye ulingo mmoja na Viongozi wa Kuchaguliwa. Wakuu wa Mikoa ni walinzi wa amani katika maeneo yao na ndiyo Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama. Hivyo, wanatakiwa wasiwe na upande wowote kisiasa na wasiwe na upendeleo wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani daima inasisitiza na itaendelea kusisitiza kuwa, ili tuwe na utawala bora kwa matendo ni vema Viongozi hao wabaki kuwa Watendaji Wakuu wa Serikali katika maeneo yao badala ya kuwa Wanasiasa ili waweze kusimamia vizuri utawala wa sheria na utawala bora bila mtazamo au mlengo wa kisiasa wa upande wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vyote katika Mkoa viko katika malezi ya Mkuu wa Mkoa na katika Wilaya viko katika malezi ya Mkuu wa Wilaya. Hivyo, si vema wakatambulika Wakuu hao moja kwa moja kuwa Viongozi wa Kisiasa na kuegemea upande mmoja wa Chama kinachohusika. Hivyo, tungependekeza sheria ile iliyowaweka katika *category* ya Viongozi wa Siasa irekebishwe na wageuzwe kuwa Viongozi wa Watumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa marekebisho haya yanahalalisha mambo ambayo katika utawala bora hayakubaliki na yanajenga dhahiri mazingira ya upendeleo wa wazi. Kimsingi *RC* na *DC* ni watumishi wanaoteuliwa na Rais, kama tulivyosema, hivyo hawana sifa za kuitwa viongozi wa kisiasa kwa vile hawapigiwi kura kama Wabunge na Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kada za *RC* na *DC* ni mabaki ya ukoloni ambapo walitumiwa ili kurahisisha utawala wa kikoloni. Hivyo hatuna budi kubadilisha na kuzifuta kabisa kada hizo. Vinginevyo kama ilivyo kwa nchi nyingine nyingi nao waingie kwenye ulingo wa siasa na wachaguliwe kupitia Vyama vya Siasa, jambo ambalo litaweka wazi kabisa na kuwa kwa mamlaka na madaraka ya wananchi watakaokuwa wamewaweka kwenye utawala watakuwa wakitetea maslahi ya chama kilichoshinda katika eneo hilo. Hali ya sasa ni kukataa dhahiri mazingira kuwa wakati chama kimoja kikishinda ngazi ya taifa chama kingine kinaweza kushinda katika ngazi ya Serikali za Mitaa, jambo ambalo haliko Tanzania tu limedhihirishwa na sehemu mbalimbali duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu imedhamiria kupeleka madaraka mikoani kwa kuwaachia wananchi kujiamulia mambo yao wenyewe na kwa kuwa kada za Makatiba Tawala na Katibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Manispaa wa Miji, Jiji na Halmashauri ni Watendaji Wakuu na kimsingi wanaiwakilisha Serikali ni vizuri kazi za *RC* na *DC* kama zilivyoainishwa katika Sheria ya *Regional Administration* yaani wanakuwa *facilitators* zifanywe na *RAC* na *DAC* ambazo kimsingi ni watalaam wakisaidiana na Wakurugenzi husika. Kwa sasa kazi za *DC* zimechanganyikana na kazi za Wakurungezi na kunakuingiliana sana kwa vile mipaka ya kazi ya *DC* haikuwekwa wazi katika sheria niliyotaja juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali basi kuleta Muswada wa kufuta kada za *RC* na *DC* badala ya kuwabadilisha utumishi kuwa *political leaders*. Kuwalipa mafao kwa kodi na jasho la wananchi wote wakati wanaegemea upande mmoja, kimsingi haikubaliki. Kwa mahesabu ya haraka tu Wakuu wa Mikoa 26 na Wakuu wa Wilaya zaidi ya 130, wanatumia fedha nyingi mathalani kwa magari zaidi ya bilioni 6.5 kila miaka 3 kununua magari mapya. Lakini kwa fedha hizo tungeliweza kufuta kabisa matatizo ya zahanati katika kata zaidi ya 60 katika nchi hii. Ni lazima tukubaliane kuwa ni lazima tuweke fedha zetu kwenye vipaumbele na hasa tuiweke pale ambapo tutapata manufaa makubwa zaidi. Matokeo ya kutokuwa na mipaka iliyowazi kati ya Ma - *DC* na Wakurugenzi ni kuwa Wakurugenzi ambao ndiyo watendaji wakuu na wenye watalaam chini yao wamekuwa na migongano na badala yake sasa wengi wao wamebaki maofisini na Ma- *DC* ndiyo wanaozunguka vijijini ambako hawana utalaam nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho yanayohusu sheria ya madini Kambi ya Upinzani inapenda kutoa mapungufu yafuatayo; kuna tatizo la msingi katika kifungu cha 4 (a) (2) kinachotoa tafsiri ya *lawful occupies* yaani kinachoelezwa mmiliki halali wa eneo liliko madini. Kambi inaamini kwamba kifungu cha sasa kinapendekeza kuwa mmiliki awe kama ilivyo kwenye Sheria ya Ardhi Namba 4 ya 1999. Kwa bahati mbaya sheria Namba 4 ya Mwaka 1999 haitoi tafsiri ya *lawful occupier* ukiangalia sehemu ya *definition* hutapata tafsiri yoyote ya *lawful occupier.* Tafsiri pekee inaweza kupatikana katika kifungu cha 95 ambayo kimsingi lengo lake ni kuweka vizingiti kwa wawekezaji na cha 96 ambacho kilikuwa kinataka kibali cha maandishi cha mmiliki iwapo mwekezaji atawekeza na mmiliki aliyekuwepo yeye kupata madhara *effective actual occupier.*

Vile vile kifungu cha 29 kinaeleza aina mbalimbali za namna ya kupata ardhi kwa mfano anayepata kwa *lease* au kwa kitu kilichoitwa *derivative right* au Mheshimiwa Rais anapogawa ardhi ya jumla. Tatizo la msingi sasa ni kuwa kuweka kifungu hiki kipya sheria yetu kwa dhati na kwa uwazi kabisa inamlinda mwekezaji bila wakati huo huo kuweka *(protection)* kinga yoyote kwa mwananchi au wananchi wanaomiliki maeneo ya aina hiyo. Kinga iliyotolewa na sheria Namba 4 sasa imeondolewa kwa kifungu hiki. Kifungu cha 19 (2) kinaeleza sababu moja ya kutoa ardhi kwa wageni yaani uwekezaji. Lakini ardhi kwa msingi huo inaweza kumilikiwa kwa njia ya *lease* kwa miaka 98 na siku 355 yaani pungufu kidogo ya miaka 99 ambayo ndiyo *lease* nyingi za sasa zilivyo jambo ambalo linaweza kuleta utata mkubwa, watu kuweza kubadilisha ardhi kwa kinyemele. Tafsiri hii lengo na matokeo yake ni kuwalinda wawekezaji bila kinga ya kutosha pia kwa wananchi wa kawaida. Kifungu cha 4 (a) (3) nacho kinatia wasiwasi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kinaleta tafsiri mpya kwa kuondoa maneno *below the ground* na kuweka *all vertically below the ground within horizontal boundaries of the license* bila kusoma kwa makini kifungu hiki kinaonekana hakina madhara yoyote. Lakini mtu yoyote anayechambua maana halisi ya kifungu hiki atagundua kuwa kifungu hiki kwa makusudi mazima kinalenga kuwaondoa wachimbaji wadogo na mathalani wa *Tanzanite* kule Mererani. Hali halisi kwa mfano Mererani ilikuwa wakati wa wawekezaji wakubwa kwa mfano *AFGEM* wamemilikishwa maeneo *block* zenye *square km 8* wakati huo huo wachimbaji wadogo wadogo wamepewa *block* za mita 50 kwa 50 ambayo kwa vyovyote haiwezekani kwenda *vertical* bila kuchimba pia wakati huo huo *horizontally.*

Kambi ya Upinzani, inadhani si namna nzuri ya kulinda maslahi ya wananchi kwani marekebisho haya sasa yataondoa kabisa katika shughuli za uchimbaji kwani itakuwa vigumu kwa wachimbaji wadogo kwenda chini tu, isitoshe hawana vifaa vya kutosha. Ni vema Serikali ikaangalia upya suala hili ama sivyo kutatokea mgongano mkubwa kwani eneo hili tayari ni la matatizo ambayo hayapatiwi ufumbuzi na wananchi wanapigwa risasi kutokana na mgogoro huu huu wa uchimbaji. Aidha kwenda *vertical* au kwenda *horizontal* hasa Mererani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine katika Muswada huu ambayo Kambi ya Upinzani, ina tatizo ni kipengele cha (m) ambacho kinafanyiwa marekebisho kifungu cha 72 cha Sheria Mama. Marekebisho hayo yanatoa uwezo mkubwa kwa Kamishna yaani kifungu cha pili. Kinatamka kufuta kitu kilichoitwa *Primary prospective licenses all primary mining license.*

Kwa taarifa ya Waheshimiwa Wabunge leseni hizi zote zinazopendekezwa kufutwa zinatolewa kwa wachimbaji wadogo wadogo tu. Wachimbaji wakubwa wote wanapewa leseni za aina tatu yaani *special license* ambayo kwa sheria inadumu miaka 50, *mining license* ambayo uhai wake ni miaka 20 na *gemstone* ambayo pia uhai wake ni miaka 20. Ni dhahiri basi kwa mtindo huu wachimbaji wadogo watakuwa wameonewa kwani ni wao tu ndiyo watakaofutiwa leseni hizi. Tunaanza kuwa na sheria yenye ubaguzi tena tunawabagua wananchi wenye nchi katika mali yao. *(Makofi)*

Tunadhani haya marekebisho pia kipengele hiki kitoe vile vile hivyo hivyo na masharti hayo hayo kwa hao wakubwa ambao wanapewa kwa miaka 50 na miaka 20 ili kuwe na usawa na kuwe na *fair and level playing ground.* Tunadhani vile vile haya marekebisho yamelenga pia kuwafutia wachimbaji wadogo na kuwapendelea wakubwa na kama tunapenda uwekezaji basi ni vizuri tukawa na sheria inayotengeneza mazingira yanayofanana kwa wote. Isitoshe Kamishna ana madaraka ya kufuta hizo leseni na anafuta bila kuwa na chombo chochote kinachomwelekeza au kumsaidia na kumshauri. Tunadhani kazi ya kufuta iwekwe chini ya chombo na siyo mtu mmoja ambaye anaweza kutumia mamlaka yake anavyoona na vile vile tumeshtushwa na tafsiri iliyotolewa katika kifungu cha ardhi ambayo kwa msingi huo huo sasa wawekezaji wakubwa wakishakusafisha gemstone hawatokiwi kulipia ushuru tena. Hili ni jambo la hatari japo nia yake inaelekea kwamba ni kuvutia wawekezaji.

Lakini tukumbuke kwamba Waziri wa Nishati na Madini, alivyotoa katika hotuba yake ya bajeti mwaka 2003 alieleza kwamba watumishi wa kigeni katika maeneo ya madini walikuwa ni 12 tu mwaka 1997 na idadi hiyo ilipanda kufikia 1197 mwaka 2002 na hawa siyo watumishi wataalam ni watumishi wa kada za chini jambo ambalo pia linaondoa nafasi kwa wafanyakazi wazalendo na tusipoangalia tutaendelea kujenga nafasi za kazi kwa wageni na watu wetu wakaendelea kubaki bila nafasi za ajira. *(Makofi)*

Aidha marekebisho yanaruhusu pia kwa makubaliano ya Mheshimiwa Waziri au Kamishna wa Migodi na mmiliki wa leseni ya mgodi wanaweza kutumia uwezo wao kisheria kumbadilishia kiwango cha kodi iliyowekwa kisheria kama vile *royalties, taxes and fees* kama ilivyo katika kifungu cha 10 (2) (b).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nguvu na uwezo mkubwa aliopewa Mheshimiwa Waziri na Kamishna katika kuweka kanuni na kuingia makubaliano maalum na wenye migodi ya madini, bado sheria imetoa marupurupu ya kodi kwa mmiliki wa mgodi kitu ambacho badala ya kulinufaisha taifa na wananchi wake, manufaa yanakuwa ni makubwa mno kuliko kwa wanaomiliki migodi.

Mfano ni kodi na ushuru wa vitu, kama magari yanayotumika migodoni, *spare parts,* mafuta ya aina zote, makadirio ya kodi na ushuru wa ongezeka la thamani kuwa sifuri. Aidha hasara kama ni kweli

kama inavyodaiwa na wengi wa madini, hatuna njia ya kuelewa kama kuna hasara kweli inayotokana na teknolojia wanayotumia. Hasara kupelekwa mbele kwa kipindi ambacho hakikuainishwa jambo hili ni la hatari kwani makampuni yanaweza kudai yanafanya hasara kwa kipindi chote cha uchimbaji na Serikali kushindwa kukusanya hata huo mrahaba wa asilimia 3. Katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali *Williamson Diamond Mines* kwa mfano inaonyesha haijalipa Serikalini *royalties* zake, inaelekea tangu kuanzishwa kwa sababu eti ilikuwa inapata hasara. Ni vema tukapata maelezo ya kina kuhusu suala hili kama leo lakini wakati wa mjadala unaohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada pia kifungu cha 10 (2) (c) sheria inatakiwa ifanyiwe marekebisho makubwa kwenye utunzaji wa mazingira kwenye maeneo ambapo shughuli za uchimbaji zinafanyika, inatakiwa kuwekwa *environmentally acceptable standard* kama sheria ilivyo kwa miradi yote mingine na uchimbaji madini unatakiwa kuwa na mazingira haya haya, mazingira ya wananchi ni lazima yalindwe. Kwa njia hii kutakuwa hakuna kufanya kama hiari kitu kinachotokea sasa hivi na kusababisha madhara makubwa kwa jamii zinazoishi pembezoni mwa shughuli za uchimbaji. Tunashauri sheria ya madini iwekewe hizi *safe environmentally acceptable standards. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha kumi (2) (d) kinachohusu usuluhishi pindi kunapotokea kutokuelewana baina ya mchimbaji na Serikali au na jamii inayoishi pembezoni mwa shughuli za uchimbaji, badala ya kumtegemea msuluhishi wa kimataifa ni bora sheria iwekwe wazi na ieleze pia ikiwa kitu cha namna hiyo kitatokea nini kitafuata. Kutegemea wawakilishi wa nje ambako makampuni mengi yanatoka ni dhahiri kutendeka kwa haki kwa wakati wa muafaka ni vigumu na vile vile utaratibu utakofuatwa ni wa kuwanyima haki wananchi wa kawaida ambao kipato chao hakiruhusu. Tunaamini haya ndiyo yalikuwa marekebisho muhimu. Lakini kwa bahati mbaya hayakuwekwa katika sheria yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maoni hayo ni imani kuwa Serikali itayafanyia kazi na sasa naomba niwasilishe kwako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Wasemaji Wakuu kwa Muswada huu wameishia hapo. Sasa ninao wachangia watatu tu mpaka sasa sijapata wengine. Kwa hiyo, nitawaita mmoja mmoja. Wa kwanza ataanza Mheshimiwa Chief Abdallah Said Fundikira, atafuatiwa Mheshimiwa Edson M. Halinga, halafu na Mheshimiwa John Singo. Sasa namwita mheshimiwa Chief Abdallah Fundikira. *(Makofi)*

**MHE. *CHIEF* ABDALLAH S. FUNDIKIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi sijazungumza lolote katika kikao hiki tangu tumeanza, ningependa kuanza kwa kukutakia kheri wewe Mheshimiwa *Deputy Speaker* na *Speaker* wetu heri za mwaka mpya na kulitakiwa Bunge letu neema na kazi njema za mwaka huu 2004 tuliuanza*. (Makofi)*

Pili, tumekuwa na chaguzi kadhaa wa kadhaa hapa, wote waliofanikiwa kwa mfano wenzetu ambao tumewachagua waende katika Bunge la Afrika, nawatakiwa kheri na fanaka katika kazi hiyo. Sina shaka watatuwakilisha kikamilifu kabisa. *(Makofi)*

Pia ninayo furaha kumkabirisha na kumpongeza ambaye nina haki ya kumwita kwamba ni mwanangu naye huyu Charles Makongoro Nyerere kwa sababu zilizo wazi kwamba baba yake alikuwa mwenzangu kwa muda mrefu, si tu kwamba tulisoma wakati mmoja tupolikuwa Makerere, Uganda na tulianzisha mikakati yetu ya kisiasa ili kuitakia Tanganyika, iliyokuwa wakati ule ipate uhuru.

Kwa hiyo, baada ya kupata tumeshirikiana pamoja kwa muda mrefu. Lilikuwa ni jambo la simanzi kubwa sana kwangu mimi Mwenyezi Mungu alipomwondoa duniani. Kwa hiyo, vijana hawa watoto wa Baba wa Taifa, nawahesabu kwamba ni wanangu. Ninapoona wanachaguliwa ili kuitumikia nchi inanikumbusha kwamba wanaendeleza heshima ile ile aliyokuwa nayo baba yao katika kutumikia nchi hii ya Tanzania kwa ujumla. Basi mimi napata furaha kubwa kuwaona na *Inshallah* watendelea kutumikia nchi hii kwa kadri wa uwezo wao. *(Makofi)*

*Mr. Deputy Speaker,* sasa nakuja katika hoja yangu ya kuzungumza juu ya Muswada huu. Mimi sina maoni tofauti sana kuliko ya kamati ambayo mimi ni mjumbe wa kamati hiyo. Lakini nikirudi nyuma

katika miaka yangu ya mwanzo nilipata kutumika kama msimamizi wa *Local Government* nikiwa Chiefu wa nchi ya Unyanyembe na tulifanya kazi tulivyoweza.

Lakini tulikuwa na jambo moja ambalo hatukulipenda nalo lilikuwa wale watumishi wa mkoloni ambao walikuwa na *PC's Provincial Commissioners and DCs* ambao walichaguliwa na *Governor* kuja kufanya kazi katika *areas* zetu sisi za *Local Government* si kwa kutusaidia tu lakini zaidi ilikuwa ni kwa haja ya kuja kudhibiti. Kwa hiyo, kazi ya watu hawa nilikuwa na mashaka nayo siku zote wale sikuifurahia sana. Kwa hiyo, katika upande huo katika shughuli zetu za sasa za *Local Government* na Maendeleo ya Serikali za Mitaa nina wasiwasi mkubwa sana. Mimi binafsi sipendelei kuendelea na mpango huu wa *Regional Commissioners and DCs* kwa siku zote naona utadhoofisha sana maendeleo ya *Local Government. (Makofi)*

Mimi siwanyimi wala si shabaha yangu kupata mafao haya ya kupata *benefits* za ku-*retire* chini ya mpango uliowekwa kwa wafanyakazi za kisiasa wapate kila wanachoweza wakapewa. Lakini wasiwasi wangu ni kwamba kila wakizidi kuyaboresha haya mapato yao ya ku-*retire* yanawa- *entrench* watumishi hawa katika kuendelea siku zote na bila shaka shabaha ambayo wote wale vijana *particularly* ambao wana haja ya ku *make clear* wakiwa ni Ma-*Regional Commissioners or District Commissioners* watafanya kila linalowezekana si kwa sababu ya *benefits* hizo nzuri ambazo za wakati wa ku-*retire* lakini pia watataka kuonyesha kwamba wanafanya kazi ambayo ni muhimu sana katika nchi na ikubali kwamba ni kazi ya muhimu lakini kwa muda tu wakati tunalea hizi *Local Governments* zetu.

Hizi Halmashauri za kila mahali za Local Government. Lakini siwezi kuamini na nina wasiwasi kwamba kustawi kwa hawa ma-*Regional Commissioners* na Ma-*DCs* katika shughuli zao hakuwezi siyo kuwa *existent* pamoja na kustawi na kuendeleza mbele na *Local Government.* Wao bila shaka wanafanya kazi nzuri lakini sisi ambao tuliokwisha jitumbukiza na *mind* zetu zimekwenda katika kutaka utawala wowote uwe *democratic* kama iwezekanavyo tuna wasiwasi kwamba mafanikio ya hawa Ma- *Regional Commissioner and District Commissioners* yatakuwa *at the expense of development* ya *Local Government* katika nchi.

Mawazo yangu mimi ilikuwa ni kwamba *at some stage in the future we should abolish this posts* zisiweko kwa sababu *area* wanayofanyia kazi ni katika *competition* na *Local Government* na sisi haja yetu *Local Government* yote iwe *democratic* itakayoendeshwa na watu wa nchi hii hii, hawa hawa watu wetu katika Wilaya na katika kila mahali katika nchi yote katika shughuli zao za kuendesha kama ni madiwani, wanaochaguliwa kwa kura za watu. *(Makofi)*

Lakini tena ukiwa na watu ambao wana- *spire* nao ku-*make a career* katika *area* ile ile ambao wanachaguliwa kwa kuteuliwa kwamba fulani wewe utakuwa *Regional Commissioner* ama utakuwa *District Commissioner* hapa na pale naona kutadhoofisha na kutawiza maendeleo ya *Local Government* katika nchi. Vitu viwili hivi haviwezi kuwa *core existence* yaani *an efficient local authority* inayofanya kazi yake ambayo inaendeshwa na *elected councils* na watu kama hao haiwezi kuwa *core exist.* Kengele inapiga siyo?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**WABUNGE FULANI:** Bado dakika tano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, endelea ni kengele ya kwanza, bado dakika zako tano.

**MHE. CHIEF ABDALLAH S. FUNDIKIRA:** Hayatakuwa ni maendeleo mazuri. Sasa mimi matumaini yangu ilikuwa ni kwamba kwa siku hizi za mwanzo kuna shughuli nyingi na hasa *particularly* shughuli ya kuhifadhi amani, *security* nakadhalika. Labda *councils as councils* kwa sasa pengine itakuwa si rahisi wao kuhamia kazi hiyo kwa mara moja. Lakini nadhani *with passage of time this councilors and councils will attain a degree of development to able to assume these duties.*

*Therefore my believe is that if the Regional Commissioners and District Commissioners continue to operate in the same area is more less competion with a District Councils, then I am so regret to say*

*that the development of Local Government in the country will take a long time and in many respect to be retiring. I want to be clear and I don't want to be misunderstood, I don't gradual this Regional Commissioners and DCs. What benefits* wanazopewa na Serikali? *But certainly, I don't think it is right, what we want here is a democratic development, particularly of the Local Government which we feel that most of our people can make their contribution. (Applause)*

*But if our people who will act against the develoment of Local Government then, I'm sorry I don't think that will be right even the* Mheshimiwa Rais *when he was delivering this memorable speech today, this morning for which I congratulate that for him and I express my gratitude to him, he did have occasion to refer to the point where he hopes that most of these duties which councilors and their councils will perfom, will gradually grow so that in the future, they will be running Local Government where most of our people live. (Applause)*

*And therefore much as I will not like to vidner their provision of this generals retirement to benefits for Regional Commissioners and District Commissioners. But my believe is that in future they should phase out from this serving in that capacity. My believe is that, since this was designed, the provision of Regional Commissioners and DCs which in fact is the old PCs and DCs which was a colonial designed to control the Africans. I don't think we should allow it to continue as a later said of their colonial regime. (Laughter/Applause)*

*At some point of other in our development we should phase them out. That is all I have to say Mr. Deputy Speaker, I may have problems on thoughts of many people but this is what I believe myself and I think it is important for the developemnt of their working of our democracy in our country.*

*Mr. Deputy Speaker, I support the giving over this benefit to the Regional Commissioners and District Commissioner. But, I don't go beyond that. Thank you. (Applause)*

***DEPUTY SPEAKER:*** *Honorable members of Parliament that was a language in Parliament during those days of early days of Independent. (Laughter/Applause)*

Baada ya Mheshimiwa Chief Fundikira sasa namwita Mheshimiwa Edson M. Halinga atafuatiwa na Mheshimiwa John Singo halafu na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi pia ajiandae na Mheshimiwa Said Nkumba, pia yuko kwenye orodha.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii nina maoni machache katika sehemu kadhaa. Kwanza napenda niipongeze Serikali kwa kukubali kufuta baadhi ya vitu vingine ambavyo kwa kweli havitusaidii sana. Kama Baraza la Tija kwa kweli haya mambo mengine lazima tukubali kuyaweka yale tunayoona yatatuletea faida na yatatuletea tija.

Lakini kuweka kitu japo kinatamkika vizuri lakini hakina tija kwa nchi hakina maana yoyote. Kwa kweli Baraza hili tumeishi, tumedumu nalo lakini hakuna lolote lililofanyika.

Mimi ninaipongeza sana Serikali kufuta kitu kama hicho. Hata hawa *Tanzanian Audit Corporation* wanakagua mahesabu lakini ukaguzi wao ni wa kulinganisha tu mahesabu, si kushauri na kuzuia namna ya matumizi mabaya yaliyotokea. Hili hata kwenye Kamati yetu tuliliona na tuliwashauri sana kwamba kwa kweli kazi wanayoifanya haitatusaidia kugundua matumizi mabaya na upotevu wa fedha, maana hawatoi ushauri wowote ila wanalinganisha mahesabu tu na kutaja makosa bila kushauri yarekebishwe vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo langu kubwa liko kwenye madini. Tunapotunga sheria hizi, tunadhani madini yako porini. Madini hayako porini, yapo katika maisha ya watu. Watu wanaishi na madini. Nitawapeni mfano mmoja, huko kwetu wameanzisha kuchimba madini. Sasa maeneo yaliyo na madini watu walihamia tangu mwanzo wa dunia hii ilipoumbwa. Lakini wamekuja watu wameanza kuchimba, wanapotoka hatujui. Wanachimba, wanatumia nyenzo mbali mbali, wanaanza kuwafukuza wenyeji wa pale, wanaanza hata kuharibu mazao ya pale kama kahawa wanang'oa eti wanachimba dhahabu. Sasa vitu kama hivi kwa kweli tusipoangalia vitatuletea matatizo sana.

Kuna wakati tulizungumza hapa nadhani ni wakati wa Bajeti kwamba yule aliyepo katika eneo la madini, ama na yule anayepewa leseni ya kuchimba, basi awe na ubia wa mwenye eneo lile. Lakini suala hili hatukulititilia uzito. Kwa hiyo, watu wetu wakishaonekana wanaishi kwenye sehemu ya madini, wao ni kuondoka tu na umaskini wao kwenda kungoja kufa mahali pengine basi. *(Kicheko)*

Hii ukiangalia hata kule Buliyankhulu Kahama *(Kahama Gold Mine)* wale watu hawakugundua wala *STAMICO* haikugundua ile dhahabu kule Kahama. Ni wanakijiji ndio waliogundua ile dhahabu, lakini maskini wametupwa pembeni hawana kitu. Tulikwenda juzi juzi kule Kakola, mji wa Kakola ni mdogo na hakana kitu. Ila wale wanaofanya kazi kwenye mgodi sasa ndio wanaofaidika. Ndio wanaojengewa nyumba na barabara. Sasa tusipoangalia hili suala, kwa kweli tutajikuta tumebaki na umaskini katika maeneo ya dhahabu lakini utajiri wanauchukua.

Watu wanapokuja kuchimba yale maeneo ya dhahabu, wamepewa leseni huko, hawaijali Wilaya, hawajali Kijiji, wao ni ardhi tu kuchimbua na kutoa yale madini na kila wanapofanya, pale wako walanguzi wa madini wamejaa. La kushangaza, mimi nimekumbana na Munowe mmoja yuko huko eti ameungana na watu wengine wa kuchimba pale. Hajui Kijiji, yeye ni kuwaambia watu wachimbe mchanga anaotaka, ana vifaa vyake vya kupimia kuwa hapa dhahabu ipo, hapa ipo, chimbeni, wanachimba wanalipwa Sh.1,000/= kwa siku. Hivi kweli madini haya yatakuwa na faida gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda Ludewa, kuna madini yanachimbwa, dhahabu inachimbwa, lakini nenda uone wale wananchi pale, yaani wale watu ni mfano wa umaskini wa kutupa tunaouzungumza siku zote. Lakini watu wanaopata zile dhahabu haijulikani zinakwenda wapi? Watu hawapewi dhahabu zile wala haziingii katika mfuko wa Taifa, hazimo! Sasa tusipoangalia haya madini, tutajikuta tunaneemesha watu binafsi tu tena wageni, wala hatupati faida katika nchi hii, wala hatuwasaidii watu wetu kitu chochote. Ni lazima sheria ingeeleza pale itoe maelekezo juu ya fidia ya mtu ambaye aliyekutwa pale kwenye eneo lile lenye madini, anafidiwa nini yeye? Sheria haisemi lolote juu ya mtu huyu. Kwa hiyo, anakuwa ni mtu mkimbizi tu wa kukimbizwa hapa pana dhahabu toka, anakwenda huko na kuishia na umaskini wake. *(Makofi)*

Sasa hii mimi imeniuma sana kule kwangu wameng'oa kahawa na mazao menginen wanasema wewe unaweza kupingana na masuala ya ardhi? Kwa kweli hili ni suala ambalo linaleta uchungu sana ila tunaomba sheria hizi zieleweke. Sasa wamekwenda hata hawajali hawa *Zonal Mines Officers,* nao sio watu wa kuaminika maana mimi huyu nilipomsikia na kumwuliza na nilikuwa na *DC* na wenzangu tukamwuliza wewe umesemaje kuwa dhahabu iko kule? Akasema eh, nilichukua kiheseni. Kiheseni ni kigunia cha mchanga sehemu zile na nimechekecha dhahabu kweli ipo. Mkuu wa Wilaya, yule sasa ni mshauri wa Serikali au ni mshauri wa watu hawa walanguzi? Lazima apewe wajibu wake unaoeleweka na ambao kwa kweli hautatuletea madhara katika nchi hii na uchumi wetu.

Mimi nasema hapa ningewekwa na sheria na mamlaka ya Wilaya kwamba itakuwa na mamlaka gani juu ya hawa wachimbaji ili iweze nayo kufaidika, iweze kueleweka. Hatusemi walazimishe lakini ingeonyeshwa kisheria. Hata hii *royalty* inawezekana inatolewa Kitaifa ni sawa, lakini sasa hata kuonyesha kwamba watafanya nini katika eneo hilo, ingeoneshwa kisheria kwamba watashughulikia haya au watamwona nani, lakini hii ya kuingia tu kuanza kuchimba madini kwamba madini hayahitaji sheria na hakuna mtu wa kulalamika, hii kwa kweli mimi inanipa woga sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, hawa waliogundua madini haya, mimi huko kwangu waliogundua ni wazee. Ubena walikuwa wanachukua zile wanasafisha wanafunga halafu ndio ya kuchezea ngoma pale ikimeremeta inakuwa ndio sifa yake pale, basi. Walikuwa watu wanacheza na mali na hii ni ukosefu wa elimu.

Lakini sasa ni vizuri basi sheria hii ionyeshe basi kwamba wananchi tuelimishwe. Inaonekana madini tunayo mengi sana. Lakini watu hawajaelimishwa, wayaenzi vipi na wafuatie vipi na wayalinde vipi. Sasa tusipofanya hivi, nchi hii kwa kweli tutabaki tunazungumza tu wengine wanakula, wengine tunang'onga mifupa, basi ndio dunia itakuwa inakwenda hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema hilo, limeniuma sana, tena sana. Naomba kwa kweli, Waziri aeleze hayo machimbo walivyoruhusu na wanavyoyaweka kwa faida ya watu. Kama wale wanaokaa kule sio watu hawahitaji kupata faida yoyote na madini yale, basi tuelewe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN. E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu.

Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kutoa hotuba nzuri, nzito nzito na kutupa changamoto ya *legacy* kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza sana kwa hotuba nzuri. La pili, nimtakie uponyaji wa Mwenyezi Mungu ili aweze kupata ahueni mapema na haraka ili aweze kufanya majukumu yake ya kuongoza nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Tatu, nianze kwa kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea mabadiliko kwa wakati muafaka ya hoja hii iliyoko mbele yetu. Mimi namwunga mkono moja kwa moja na nitapenda kuchangia machache katika hoja hii. La kwanza ni kuhusu ile sehemu ya *Political Service Retirement Benefit Act,* ile ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Kumekuwa na hisia nyingi sana kwamba Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa hawana sababu kuwepo. Lakini kuna usemi mmoja unaosema, ukiua njia moja lazima utengeneze njia nyingine ya kupitia. Sasa kama hatutaki wawepo, tunataka nani awepo? *(Makofi)*

Mimi nafikiri tusifikie hatua tukapoteza dira yetu katika nchi yetu, tunahitaji Wakuu wa Wilaya na tunahitaji Wakuu wa Mikoa kwa nguvu kabisa. Kwa sababu sehemu yao katika nchi yetu ni muhimu. Tulikuwa na ule utaratibu wa madaraka Mikoani, sasa tukiwaondoa ndio tutakuwa tumefikisha madaraka kwa wananchi. Tunataka wananchi wetu wapate huduma kwa karibu. Kwa maana ya kumwondoa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ni kumwambia mwananchi aliyeko Wilayani au Kijijini apande *train* au apande gari au *bus* aende Dar es Salaam akamwone Waziri au Katibu Mkuu ama Rais. Kwa hiyo, nafikiri kazi wanayoifanya ni kubwa sana ya kuweza kufikisha uwakilishi wa Serikali yetu karibu na watu. Kwa hiyo, kuwepo kwao ni kwa muhimu sana. *(Makofi)*

Lingine lazima tubainishe tofauti kati ya viongozi wetu wa Halmashauri kwa maana ya maendeleo ya watu wetu. Wananchi wetu wote wanaishi katika Halmashauri kwa maana ya kupata huduma muhimu za maendeleo. Lakini vile vile wananchi wetu hawawezi kuishi kwa amani bila kuwa na utawala mzuri, utawala bora na utawala bora huu wataupata kwa Mkuu wa Wilaya na Mkoa. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba bado tunawahitaji, wale hawapo pale kwa ajili ya *structure* za kikoloni. Ile ni *network* ya Serikali Kuu na isipokuwepo maana yake hakuna Serikali Kuu mahali wananchi wetu waliko. Kwa hiyo, wao kuwepo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Sasa nije lile la *benefits.* Hapo ndio ninakuwa na mgogoro kidogo. Kwanza wao hawakuomba kazi ya Ukuu wa Wilaya, kazi ya Ukuu wa Wilaya na Ukuu wa Mkoa huombi. Unateuliwa na huyo anayekuteua anakuteua kwa mamlaka aliyopewa na Wapiga Kura wa nchi hii. Kwa hiyo kwa njia moja au nyingine na wewe ni kama umechaguliwa *indirectly.* Lakini wakati mtu ametoka katika utumishi wa umma halafu anakuwa *DC* au Mkuu wa Mkoa, mimi nafikiri ingekuwepo *option* kwamba wapi alikuwa na marupurupu makubwa yako wapi ili achague. Kama alikuwa na marupurupu makubwa kule kwenye *public service,* basi achague huko awe na *option* na kama ni huku kwenye siasa, basi achukue hiyo *option* ambayo anapenda na bila shaka ni kubwa zaidi. Nafikiri hilo lingekuwa zuri zaidi kuliko tukiwaamulia moja kwa moja.

Lakini pamoja na hilo la *political benefit,* kuna moja ambalo tunasema umefika wakati wa ku-*retire* lakini kuna kimoja tumekisahau. Maisha ya mtu yanaweza yasifikie *retirement.* Atapata ajali, atakatika miguu yote ama mkono, atapata kilema cha jicho ama akafa kabla ya *retirement.* Hili nalo haliwekwi hapa. Mimi mwaka 2002 Oktoba nilipata ajali karibu jicho hili litoke na nilifikiri limetoka. Lakini basi Mwenyezi Mungu akalibakiza. Sasa baada ya pale nikajiuliza hivi hili jicho lingetoka ingekuwaje? Nikamwuliza Mheshimiwa Mwanasheria pale, akasema sana ni kifuta machozi. Hii habari ya kifuta machozi Mwanasheria Mkuu tunataka isiwepo sio kwa *public service* tu, lakini hata kwa *political leaders.* Huyu mtu hajafikia *retirement* akafa hapo katikati.

Jana mama mmoja amenifuata hapa, mume wake amekufa akiwa katika *public service* ya Serikali za Mitaa. Anazungushwa kupata fedha za mumewe na hata watoto hawaendi Shule. Yule bwana alifariki kabla ya *retirement,* lakini sasa watoto wamebaki hawaendi Shule. Lazima pamoja na kuyaangalia haya, Serikali ikaangalie. Hawa watu wamejitoa kufanya kazi ya Serikali, ndio shamba letu, hatuna shamba lingine. Wakulima wana mashamba yao na kila siku wanafikiria kuyapanua na kuyaboresha, lakini ili sisi tuweze kufanya kazi za Serikali vizuri, hili ndio shamba letu tunalolifanya ya siasa ama ya Serikali. Serikali lazima imfikirie huyu mtu kabla hajafikia *retirement* akipata ajali akawa kilema miguu yote imekatika itakuwaje? Kwa sababu haya yanaweza kutupata tena wakati wowote. Katika maisha tunaishi na uhai na balaa iko hapo hapo jirani na hata kifo kipo hapo hapo jirani. Ukikatika miguu huwezi kutembea, mikono imekatika, jicho limetoka ulikuwa unaona sasa huoni, umekuwa kipofu ghafla. Je, hayo tunayafikiria? Ama tunafikiri tuna ahadi na Mwenyezi Mungu kwamba sisi tutaendelea kuwa Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na kadhalika mpaka tufikie *retirement,* tuna ahadi na Mwenyezi Mungu? *(Makofi)*

Ningeomba Mwanasheria Mkuu siku nyingine Mungu akijaalia *inshallah,* ukituletea tena *amendments* tungeomba hilo likaangaliwe. Habari ya kifuta machozi ni mambo yaliyopitwa na wakati. Nchi zilizoendelea kama sasa tumeingia kwenye utandawazi, ukimwambia mtu kifuta machozi hakuelewi. Kifuta machozi maana yake amesema bila shaka huyu mtu tumlipe kama Sh.50,000/= ndio maana ya kifuta machozi, ama alipwe laki moja kama wale ndugu zetu waliopata matatizo katika *train.* Lazima tuanze kufikiria mambo ya *insurance* (Bima), kama sio Bima utaratibu mwingine ambao sheria itaona unastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi hoja ya Wakuu wa Mikoa ninaiunga mkono kabisa na Wakuu wa Wilaya nasema ndio msingi wa *structure* ya Serikali Kuu kuwafikia wananchi Vijijini kwetu. Tukiuondoa na tukirudi kwa wananchi wetu tutasema wapeleke matatizo yao wapi? Suala la kusema wao sio wanasiasa, lakini wao kama Wakuu wa Wilaya ama Wakuu wa Mikoa, ndani katika Mikoa yao na Wilaya zao siasa inatembea. Wao kama watawala lazima wawe upande wa siasa kwa sababu siasa ndio inatawala. Kwa hiyo, lazima wawe upande wa siasa, hatuwezi kuwa na njia nyingine bila kuwaweka hapa. La pili nilipenda kuchangia kwenye *Mining Act.* Msemaji aliyepita Mheshimiwa Halinga ameongea kidogo sana kwa uchungu na mimi nitaongezea. Machimbo yaliyopo Tanzania yapo katika maeneo Watanzania wanapoishi na watu wa kwanza kujua hapa kuna madini ni Watanzania na watu wa kwanza kuhamishwa mahali madini yalipo ni Watanzania na watu wa kwanza kuachia nafasi ili machimbo yachimbwe ni Watanzania. Sasa wale ambao wanahusika kwa njia moja au nyingine katika uchimbaji, kuruhusu, kutoa nafasi ya madini yakachimbwe katika ugunduzi lazima tuwape nafasi yao.

Mimi ningeomba, kwa sababu haipo wakati huu, lakini katika ukurasa wa tisa kuna ile sehemu ya *establishment of a Gemstone Body.* Tuanze kufikiria suala la kisheria sio kama lile linalofanana na kifuta machozi na wagunduzi wetu wa madini. Katika bajeti iliyopita, baba mmoja anaitwa Jumanne Ngoma alikuja hapa akilalamika kwamba yeye ndiye mgunduzi wa *Tanzanite,* lakini anaendelea kuishi maisha ya umaskini wa kutupa. Mwaka 1984 naambiwa alilipwa Sh.300,000/= na Serikali inasema. Je, hizo laki tatu hashibi? *In Europe* wangeuliza, mimi nimegundua *I am suppose* kupata *arrears* kila siku ka-p*ercent* kidogo. Sisi tunawakatisha tamaa Watanzania kuanza kugundua madini. Kule kwenye Jimbo langu mzee mmoja wanasema ameona madini ya ajabu. Ukishika hayo madini, mkono unakufa ganzi. Namwambia nipeleke, anasema hapana mtanifanyia mambo yale yale ya Jumanne Ngoma, kwa sababu ninyi mkishapewa Serikali haitutambui.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali, sasa tuko kwenye utandawazi iache kufunga milango. Huu utandawazi ambao tunauongea umefungua milango kwa mambo ya namna hiyo lakini yule mtu amelipwa laki tatu kwa sababu wakati ule ulikuwa wakati wa ujamaa. Nilisoma barua yake ambayo Marehemu Mwalimu Nyerere alisaini kwamba apewe zawadi ya laki tatu. Mwalimu Julius akaandika pale nakubali, akaweka J.K. Sasa leo hatuko katika ujamaa kikamilifu, hawa watu wanakuja wanachimba madini wanapata faida kubwa, maskini Mtanzania wetu amebaki pale pale. Tunaomba sheria iangalie wagunduzi wa madini wanapewa nini ili watu wetu wachakarike porini. Hatuwezi tukayapata yale madini sisi tulioko humu ndani lakini walioko huko Vijijini watayapata na kwa kweli kuna madini mengi ya thamani watu wanayapata moja moja wanazungusha wanakaa kimya, wanafanya kama magendo,

wanaficha kwa sababu wanaogopa nikipeleka hii ni *gemstone* kwanza wataniona sina *PR,* sina hati na mimi yatanipata yale yale ya Jumanne Ngoma. Ningeomba sana Mwanasheria Mkuu aliangalie hili. Nina imani kabisa siku nyingine tukiletewa *amendment* bila shaka Serikali itazingatia haya ambayo tumeishauri, si kwa ajili ya maslahi yetu lakini kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu na maendeleo yake na uchumi wake. Mimi napenda nimpongeze Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea mabadiliko haya na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake na ningependekeza pengine labda washauri wake na Mheshimiwa Kingunge wangempitishia ujumbe kwamba angeanzisha utaratibu kwamba anapotoa hotuba nzuri kama hiyo atenge siku mbili akakaa hapo tukaijadili akiwepo na umma ukasikia kama walivyosikia ya kwake. *(Makofi)*

Baada ya kulisema hilo, nataka sasa kuchangia katika huu Muswada na hususan hii sheria inayoangalia mafao ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuwaweka katika kundi la viongozi wa kisiasa. Ama ziko hoja mbili hapa. Ya kwanza, kwamba mfumo ule uondolewe kabisa na ya pili kwamba usiondolewe lakini kama wanataka kuwa wa kisiasa zaidi ili waweze kufanya kazi ya kisiasa, basi wakachaguliwe kwenye maeneo yao. Ningelipendelea hilo li-*appear* zaidi kwamba kama watu hawa tunataka wawajibike na wafanye kazi vizuri na waulizwe, ingekuwa vizuri kama inaundwa Tume, basi ichunguze kwamba mfumo wa sasa uendelee kama ulivyo na hadidu za rejea ziwekwe kwamba viongozi wale wa Mikoa na Wilaya wachaguliwe na wananchi ili waweze kujibu.

Waheshimiwa Wabunge wote tulioko humu ndani tunajua kwa kweli unapofika mbele ya Wapiga kura unavyo-*behave* na unavyojibu na unavyojitahidi kwa kadri unavyoweza ndani ya Bunge na nje ya Bunge kuhakikisha kwamba maslahi ya wananchi wako waliokuchagua yanatekelezwa ipasavyo na unajua usipofanya hivyo kwamba miaka mitano ijayo utakwenda kujibu pale. Hili la Wakuu wa Mikoa jinsi tunavyoliweka hapa, nadhani Mheshimiwa Rais amesema kwamba kujaribu kuficha moto kwenye karatasi ni hatari lakini kujaribu kuchemsha maji au kimiminika chochote halafu unasiriba kile chombo unachochemshia ni hatari zaidi. Kwa sababu kinachofanyika hapa, hawa viongozi wa kisiasa ambao wanahudhuria kwenye Kamati Kuu ya Chama pale Wilayani au Mkoani na wakati huo huo wakiwa Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama na usalama wakati mwingine Chama kilichoko madarakani hakiwezi kukubali usalama wake ukatishiwa ovyo ovyo hivi, kwa hiyo hii ni hatari zaidi kwa demokrasia ndio maana inabidi tusimame tuseme hivyo hata kama hayo maneno kuna watu yanawaudhi na hatutaomba radhi kwa hilo. Kinachonishangaza ni kitu kimoja. Hivi sasa tumeanza, *DCs* na *RCs* tunawaweka pale, itafika mahali tutatafuta Makatibu Tarafa tutawaweka pale kwa sababu hakuna hoja ya msingi ya wao kutowawekwa pale kwa sababu ni Wasaidizi wa Wakuu wa Wilaya. Mwisho, kwa sababu tumesema Rais kwa njia moja au nyingine atamteua Afisa Mtendaji wa Kijiji kupitia kwa *DED* na Afisa wa Kata tutamweka pale na Afisa wa Kijiji tutamweka pale, sasa haya mambo yanapofikia hatua hiyo, nadhani umma utakuja kuangalia kama sisi tunajipendelea zaidi.

Kinachoshangaza katika sheria hii, unaangalia *RC na DC,* bado viongozi wa siasa wenyewe tunawapiga kumbo na kila siku majibu ya Serikali hapa Bungeni ni kwamba Serikali haina fedha. Diwani posho yake ni Sh.30,000/= kwa mwezi. Halafu tulisema Diwani kama unagombea uwe ni mtu unayejiweza. Sasa hiyo sheria kama sio ya ubaguzi, anajiweza kwani wewe Mbunge kwa nini usijiweze? Kwa nini unataka mshahara? Hapa Mkuu wa Mkoa aliyezungukia nchi hii kwa miaka 20 ana haki ya kupata kwa sababu na yeye labda hapa tungetafuta utaratibu mwingine lakini sio kumweka hapa kwenye hii ya kisiasa kwa sababu hawana nafasi hata ya kufanya biashara. Lakini huyu Diwani anafanya shughuli zote hizo halafu kiinua mgongo kama cha mtoto mdogo na sisi ni Wabunge tunajua kwa sababu tunakaa nao na sisi ni kama Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunasherehekea na kushangilia mafanikio ya mpango wa *MMEM.* Nina uhakika kwa uchambuzi wangu kama si mchango mkubwa uliotolewa na Madiwani kwenye Kata zao kujitolea kuhamasisha watu kubeba matofali, mpango huo usingefanikiwa kwa asilimia tuliyofanikiwa. Lakini wakati huo huo na Diwani kwa kweli siku anagombea ama Mbunge, anaulizwa sasa wewe Shule iko wapi, Zahanati iko wapi, lakini sijawahi kusikia wananchi wakimwuliza Mkuu wa Mkoa

kwamba hivi wewe Mkuu wa Mkoa umekaa hapa Tanga miaka kumi, hebu sema ulifanya wapi, Shule iko wapi? Hawawezi kumwuliza! *(Makofi)*

Nchi nyingine, kama Marekani, *Governor* unakwenda pale unagombea wanakuchagua useme sera, mtoza ushuru kama wale *Regional Officers* wa *TRA* unagombea ili uje ujibu ulipotoza ushuru kodi zile ulipeleka wapi, ujibu sio unakaa hapo tu! Sasa hapa kuna utaratibu ambapo mtu yuko pale ana madaraka makubwa ya kukukamata hata wewe Mbunge anakuweka ndani, anaamrisha Polisi wanakukamata, lakini hawezi kuulizwa hivi Shule ya Sekondari iko wapi? Wewe umekaa hapa miaka kumi, hawezi kuulizwa!

Lakini tunasema tumpe mafao mengi na tunampa nyenzo nyingi, gari kubwa lakini hawezi kuulizwa. Sasa hivi tukihoji hapo tunakuwa tunakufuru au tunataka kuhoji ili tuweze kuweka utaratibu mzuri? Kwamba Wilaya iwepo iwe na *DC* agombee tumpe nyenzo na kwa kweli wamwulize na ajibu. Tuweke utaratibu mzuri kwamba watawajibika kwa Rais kwa utaratibu tutakaouweka. Kwa sababu hata kwamba kama tuna Serikali mbili, sidhani kama kuna Rais wa Zanzibar anafanya ukorofi kwa mujibu wa Katiba hii kwamba sasa tukisema *RC* achaguliwe, *DC* achaguliwe atakuwa mkorofi dhidi ya Rais aliyewekwa, hawezi kuwa hivyo. Lakini ninachotaka hapa ni kwamba watu hawa wanawajibika. Kwa sababu kinyume chake kama hawawajibiki kwa umma, wanawajibika kwa mtu mmoja, anaweza kuwa-*mislead*. Najua kuna watu waliambiwa hapa, wewe *DC* umekuja hapa ukisema kuna njaa, utanitambua.

Sasa ilikuwepo njaa. Kuna wakati Wabunge walikuwa wanagombana kwamba lakini wewe mbona unatoa taarifa kidogo, sasa mtu anatetemeka nikitaja hivi watanirukia, utafikiria wewe ndio umeleta ukame. Wanakurukia wewe utafikiri umepewa hela za kilimo ndio umeziiba! Tuweke mfumo ambao watu wote wanawajibika kwa umma na ndio utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kuyasema hayo, nilikuwa naomba kwamba wakati tunaiweka hivyo, tungeitafutia namna nyingine na tukumbuke hawa wengine Madiwani, vinginevyo tukiiweka hii na hatuwaweki kwenye Chama wagombee hatakuwa na faida yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalisema kwa sababu nina ushahidi mkiutaka maana Mbunge huwezi kusimamia hapa unazungumza ovyo ovyo. Yuko Mkuu mmoja wa Wilaya alikuwa anapiga kampeni kwenye Uchaguzi wa Madiwani, kwenye Mkutano wa Chama anahutubia anasema mimi nitahakikisha tunashinda na kama hatushindi mtanitambua.

Anaitwa Rugusha pale Bukoba. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba umma wa pale ulisema mlikatakata baiskeli zetu, tunawakomesha na waliwakomesha kweli. *(Makofi)*

Sasa ikifika mahali Mheshimiwa Naibu Spika, *DC* unaacha shughuli zako za kiutendaji na kuwa kama mlezi wa vyama vyote vilivyoko pale, wewe unapokonya madaraka, unahutubia pale na wengine wanasema mimi nimeletwa kuhakikisha upinzani unazima. Wewe unauzima, kwanza unavunja Katibu ya nchi. Kwa sababu suala la kuwepo kwa vyama vya upinzani liko katika Katiba ya nchi, sasa kwa kusema hivyo una maana gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kwamba Wachina wana methali wanasema uzuri wa maua ya mti fulani si ishara kwamba matunda ya mti ule yatakuwa matamu. Sasa sisi tunauona huu mfumo tunaouweka na tunadhani unapendekeza. Lakini pengine ungelirekebishwa, pengine ungeliweza kusaidia katika harakati zetu za kutaka kupinga maendeleo ya kiuchumi na jamii haraka sana kuliko hivi sasa tunavyoweza kufikiri kwa maslahi binafsi ya kiitikadi.

Baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa sababu nasimama kwa mara ya kwanza, napenda nichukue nafasi hii vile vile kuwatakiwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kheri ya mwaka mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesimama siku nzuri sana, Mheshimiwa Rais leo ametoa hotuba nzuri iliyojaa mafanikio ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Na hii ni ishara ya kutosha

kabisa tunapoelekea kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa pamoja na Serikali Kuu, Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005, Inadhihirisha kabisa kabisa kwamba mafanikio haya ni silaha ya kutosha kwa chama na Serikali ambavyo viko madarakani. *(Makofi)*

Nitasema kwa ufupi sana Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza moja kwa moja kwenye marekebisho yanayotaka kuwafanya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kupata mafao ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatofautiana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao kwa maelezo yao hayakuwa yanaonyesha umuhimu wa kazi nzuri zinazofanywa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za Wakuu wa Mikoa na kazi za Wakuu wa Wilaya zinajidhihirisha wazi wazi katika kusimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi. Sasa hatuzungumzii kwa sababu Chama Cha Mapinduzi kinatawala. Hili liko kwenye suala la Katiba kwamba lazima awepo mtu anayezungumzia suala la utekelezaji wa ilani wa Chama kinachotawala. *(Makofi)*

Nalisema hili kwa sababu Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tufike mahali tupishane lugha. Lugha anayokwenda kuzungumza na wananchi katika suala la kuhamasisha maendeleo anayokwenda nayo Mbunge lazima itakuwa tofauti na mtu anayeongoza Serikali. Kwa hiyo, kazi ya Mbunge utakwenda utahamasisha, kama ni Diwani utahamasisha. Anakuwepo mtu anayesimamia kazi ile. *(Makofi)*

Sasa mimi natambua kwa kweli mchango mkubwa ambao Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wameufanya katika kusuma maendeleo ya nchi yetu. Na hili si suala la kusema haya ni mabaki ya ukoloni. Hii si dhana ya mabaki ya ukoloni. Kwani Wabunge hawakuwepo wakati wa ukoloni? Nao walikuwepo. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, tunachukua yale mambo mazuri yaliyokuwepo wakati wa ukoloni tunayafanyia kazi sasa katika kusukuma maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, naunga mkono kwa kweli marekebisho haya yatawapa nafasi hawa wenzetu wakaribiane karibiane na Waheshimiwa Wabunge wawe pamoja katika kusukuma maendeleo na mimi nasema huu ugomvi wa wewe kama mwakilishi wa wananchi umechaguliwa, uko pale, una dhamana ya wananchi na mwingine ameteuliwa yuko pale ana dhamana ya Kiserikali, ameteuliwa na Rais, ugomvi unatoka wapi. Kila mmoja ana majukumu yake, mlengwa ni mwananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi natoa mwito tu, tushirikiane kwa kweli tuwasaidie wananchi wetu kuleta maendeleo. Kazi nzuri zinazofanywa na viongozi wetu hawa katika kulinda amani, kusukuma maendeleo, zipo na mimi nasema viongozi wetu hawa pamoja na kwamba wanateuliwa na Mheshimiwa Rais, wanafanya kazi zao bila ubaguzi wa kisiasa katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mimi ninayo mifano hai ipo, mingi tu. Jimboni kwangu kwenye Wilaya yangu, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ni kimbilio, kimbilio la vyama vyote vya kisiasa. Wanapokuwa na tatizo wanakwenda pale na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inasaidia.

Sasa tunataka tuwe na Ofisi ya namna gani nyingine na siungi mkono kabisa wazo la kusema Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa achaguliwe. Tutakuwa na watu wa kuchaguliwa wangapi pale. Mbunge achaguliwe, Diwani achaguliwe, Mwenyekiti wa Kijiji achaguliwe. *(Kicheko)*

Mimi nafikiri haya yaliyopo sasa hivi ni mambo mazuri sana yanatusaidia kututenganisha, watu wa kuchaguliwa ni akina nani, watu wa kuteuliwa ni akina nani. Na kila mmoja ana majukumu yake na tusifike mahali tunawaogopa Wakuu wa Wilaya, wako pale kwa kutusaidia kazi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mimi sina maneno mengi sana isipokuwa naunga mkono kabisa kwa nguvu zote marekebisho haya na vile vile nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuyaunge mkono tukasaidiane kuleta maendeleo huko vijijini na mijini kwa wananchi wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Mimi nataka kuzungumzia maeneo machache sana na ndio maana dakika tano zitanitosha. *(Kicheko)*

Ni eneo hili la kuogopwa kivuli cha Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Lazima tufahamu Waheshimiwa Wabunge kwamba Mkuu wa Mkoa ni kiungo cha Serikali Kuu na Mkoa ule kama ilivyo kwa Mkuu wa Wilaya kuwa kiungo cha Mkoa na Wilaya. Ukiacha tu Serikali inaning'inia haina pa kujikita kule Mkoani na Wilayani hasara yake ni kubwa zaidi kuliko woga mlio nao Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

*RC* na *RAS, DC* na *DAS* ni vyeo viwili tofauti kabisa. Yuko Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kaka yangu, amesema bora abakie *RAS* na *DAS* kuliko *RC* na *DC.* Hawa watu hawafanyi kazi moja hata kidogo. Kuna watawala na watendaji, watendaji ndio hao *RAS. (Makofi)*

Labda tungeulizana swala moja, hivyo Serikali inapatikanaje ndani ya nchi yetu. Ni chama kuuza sera zake kwa wananchi. Uchaguzi unapofika wananchi huchagua sera ambazo wamezipenda kutokana na dhana kadha. Serikali inapokaa madarakani lazima ihakikishe kwamba sera zake zinatekelezwa kivitendo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama unamkubali Waziri kuwa Kamisaa katika ngazi ya Wizara, unachekesha sana unapokataa Mkuu wa Mkoa kuwa Kamisaa wa sera hizo katika ngazi ya Mkoa hivyo hivyo kwa *DC* Wilayani na kadhalika na kadhalika. *(Makofi)*

Chama hicho ndiyo kitakachowajibika kuulizwa baadaye, mlitekelezaje mambo haya? Ndiyo! Na kama kinawajibika kuulizwa lazima kiweke wasimamizi wake. Nitakapokwenda mie Mbunge au Diwani kuhimiza maendeleo kwenye Wizara yangu lugha yangu inakuwa ni ile ya kuweka akiba ya kupata kura miaka mitano mingine. *(Makofi)*

Na kumpeleka Mkuu wangu wa Mkoa au wa Wilaya lugha yake ni ya kiserikali ya kuhakikisha ya kwamba sera ile inatekelezwa na mipango inasimamiwa vizuri. Lazima tutofautishe kati ya Mkuu wa Mkoa na *RAS,* Mkuu wa Wilaya na *DAS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mmoja amezungumza hapa kwamba inawezekana Rais akashinda ngazi ya Taifa lakini Wilaya moja Chama cha upinzani kikashika hatamu. Sasa haya mambo ya Wilaya mbili kati ya Wilaya mia na thelathini wanasikilizwa, wengi wanapewa. Ndiyo demokrasia. *(Makofi)*

Lakini ukoloni ni kwa ua-*RC* tu na kwa *DC?* Mbona vyeo vingine vingi bado tunavihusudu na viliwepo wakati wa ukoloni. Sasa tusichukue ugomvi labda wa Mheshimiwa Mbunge kadha na *DC* akasema, huko ni kuua upinzani, akasahau kwamba *DC* huyu ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa wa Wilaya yake. Tukataka kugeuza suala hili mtaji wa hoja hii iliyo hapa mbele yetu leo. *(Makofi)*

Mifano mingine watu wengine mmejitolea wenyewe. Anasema ukiona maua yanapendeza katika mti fulani, basi siyo dalili kwamba na matunda yake ni matamu, hivyo hivyo kama yanavyopendeza maua. Sijui kayaona hayo maua hapo mbele. *(Kicheko)*

Kwa sababu utamu wa matunda si maua hata siku moja. Na ndiyo maana pamoja na maneno hayo mazuri ya baadhi ya wanasiasa Watanzania unapofikia uchaguzi hustaajabu uchungu wa ukweli na uwazi lakini wenye kuleta mafanikio kuliko utamu wa ahadi ya majigambo ambazo matokeo yake ni mbili mara mbili kutoa nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tutatofautishe tabia ya *DC* fulani kwa jina lake labda Mudhihir na nafasi ya *DC* na umuhimu wake katika mlolongo wa utawala wetu. *(Makofi)*

Inawezekana *DC* akawa mbovu wa hulka yake na hiyo inaweza kutokea hata kwa Mbunge mmoja akawa mbovu kwa hulka yake. Ikawa anapozungumza badala ya kufurahisha akawa anachefua wenzake. Huu ni uanadamu, siyo daraja, siyo ngazi iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii niweze kuhitimisha hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu. Na kama kawaida nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii kwa kusema humu Bungeni na kwa kuchangia kwa maandishi.

Nikianza na Naibu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Mzee wangu Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Edson M. Halinga, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Mheshimiwa Said J. Nkumba na mwisho ni Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. *(Makofi)*

Kwa maandishi wamechangia Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Frank M. Mussati na Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye. Wote hawa nawashukuruni sana na nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kusikiliza hoja hii na kuitafakari kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uhaba wa muda sitafafanua sana maeneo yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini niseme tu kwa hilo upande wa mafao ya viongozi wetu Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, nashukuru sana michango ya Waheshimiwa Wabunge, hasa Mheshimiwa Mudhihir na Mheshimiwa Nkumba kwa yale mazuri ambayo wameyasema kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na viongozi hawa katika kulinda amani na utulivu tunayoiona katika nchi yetu. Hawa ni viongozi mihimili muhimu sana katika amani na utulivu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini leo Mheshimiwa Naibu Spika, hatuongelei kuhusu muundo wa utawala wa Mikoa, tunaongelea mafao ya viongozi hawa. Ni vizuri tukaiona hoja hiyo katika mtazamo huo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuiunga mkono hoja hiyo na kwa kuielewa kwamba viongozi hao wanafanya kazi nzuri na kama mtu yoyote anayefanya kazi anastahili akapewa tuzo na tuzo hii ni tuzo unapofikia umri wako wa kustaafu.

Mheshimiwa Nasibu Spika, naomba nifafanue tu kwa upande wa viongozi hawa ambao ni watumishi wa umma, kama alivyoelezea Mheshimiwa Lubeleje, Serikali haipendekezi pawepo na chaguo kwamba uwende kwenye Sheria, *Political Leaders* au uendelee, hapana.

Ila kwa kutaka kuwatendea haki kwa sababu tunajua hizi kazi huombi, unasikia tu Mheshimiwa Rais amekuteua Mheshimiwa Iddi Simba, ameteuliwa na Rais kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza. Sasa inakuwaje, ni vigumu sana kukataa uteuzi, maana utumishi hakuna kitu kizuri kama kukubali kuwatumikia watu wako na ndiyo maana mara nyingi inakuwa kwa unyenyekevu kabisa watu wanakubali kuchukua nafasi hizi. Sasa kwa mtu ambaye ana utumishi wake wa nyuma katika utumishi wa umma, mtumishi wa Serikali au alikuwa kiongozi mtendaji katika shirika la umma, sasa inakuwaje.

Sasa Sheria lazima iwe wazi, ndicho tunachosema. Ni kwamba kwa vile Bunge hili mwaka 2000 lilifanya marekebisho kwenye kifungu cha saba (7) cha Sheria ya Viongozi wa Kisiasa na kusema kwamba utumishi wake kama kiongozi wa kisiasa utahesabiwa kwa madhumuni ya kupata ule mwuunganisho ile *qualifying period* ili aweze sasa kusema, wewe ulikuwa *State Attorney,* Wakili wa Serikali una kipindi cha miaka 10 kabla ya kuteuliwa kuwa *DC,* umeenda tena ukafanya kazi kwa kipindi cha miaka 10.

Sasa umefikia au umesita kuwa kiongozi au umefikia umri wa kustaafu kwa lazima. Sasa tunasema katika hali hiyo kile kipindi chake hiki cha miaka 10 hii ya uongozi wa kisiasa, iunganishwe na ile miaka 10 ya kwanza, apate ile *qualify period* na kwa mtu huyo kwa sababu sasa hivi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma *qualifying period* ni miaka 15.

Kwa hiyo, tayari mtu kama huyo atakuwa amepata stahili ya kulipwa pensheni na hapo hapo kwa sababu alikuwa anachangia. Sasa hivi wanachangia, atapata mafao mazuri katika kustaafu kwake. Hiyo ndiyo hoja iliyo mbele yetu. Tunaomba mtuelewe na mtuunge mkono katika hili.

Mheshimiwa Mussati na Mheshimiwa Dr. Slaa. Mheshimiwa Mussati ametoa wazo zuri kwenye Kamati ya Bunge Zima nitasimama linisaidie. Marekebisho haya kwa kosa la unyang'anyi kwa kutumia silaha Mheshimiwa Slaa amesema tuwe waangalifu. Ni kweli, bahati mbaya zinatokea. Lakini tunaamini Polisi inavyoendelea kuimarishwa kwa njia mbalimbali hasa kwa mafunzo, watafanya kazi yao kwa makini. Lakini hatimaye anayeamua kwamba kosa hili limethibitika ni Mahakama na ndiyo maana ni suala la ushahidi.

Hoja iliyo mbele yetu kwenye eneo hili ni kwamba kifungu cha Sheria hiyo kilivyokaa sasa hivi kimetupatia matatizo sana Mahakamani. Sasa tunakinyosha na niseme tu *a dangerous weapon* siyo lazima liwe panga, unaweza kuja na rungu hapa, ukamtwisha tu yule mtu. Sasa katika kufanya hivyo na rungu lako ukaweza kutimiza dhamira yako kwamba una rungu, isije kwamba hiyo siyo chombo hatari kwa madhumuni ya kosa tunalolisemea hili. Adhabu, tunasema jamani miaka 15 huwa nasema kama unadhani kwamba hiki kipindi cha miaka 15 ni kipindi kifupi sana jaribia tu wewe mwenyewe hata baada ya dakika moja tu kuingia mle ndani. Tuziachie Mahakama, tunasema hii kwamba ni *minimum,* ilivyoandikwa isomeni vizuri. Mimi nadhani kwamba haya ni makosa mazito na ni vizuri yakapewa adhabu zinazoendana na uzito wa kosa hilo. *(Makofi)*

Nikimbie mara tu kwa upande wa Sheria ya Madini. Niseme tu kwamba Sera ya Madini ipo. Sheria ya Madini ipo. Tunachofanya sasa hivi kwenye eneo hili ni kuiboresha zaidi Sheria ya Madini. Lakini hatutungi Sheria mpya. Sera ya Madini ambayo inafafanuliwa sasa itekelezwe kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ambayo Bunge lako lilipitisha, katika kifungu cha 5 maana tunaanza. Juzi nilisimama mbele yenu hapa nikaelezea na wote tunaifahamu dhana ya miliki ya ardhi. Ardhi Tanzania ni mali ya uma na itaendelea kuwa mali ya umma.

Tunachofanya ni kuainisha *definition* ya *law for expire* ili iendane vizuri na *definition* ya Sheria ya Ardhi. Lakini la msingi tunalosema ni kwamba ardhi ni mali ya uma. Madini yaliyo juu ya ardhi, yaliyo chini ya ardhi ni mali ya uma. Na yatatumiwa kwa manufaa ya nchi hii, wenyewe ni wananchi, mmoja mmoja au kwa makundi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 5 cha Sheria ya Madini kinasema wazi kabisa: *"the entire mineral property* and *control of minerals in, on or under the land to which this Act applies is first in the United Republic of Tanzania".* Hii ndiyo Sheria, kwa hiyo, wewe una haki sasa ya kutumia ukiyapata, madini yote haya yana utaratibu, ukitaka. Ndiyo leo tumemsikia vizuri sana Mheshimiwa Rais akiyaelezea haya. *(Makofi)*

Fursa zinatolewa siyo kwa wageni tu, lakini kwa Watanzania tujitume na ndiyo maana najua hata humu ndani ya Bunge wako Waheshimiwa Wabunge ambao wanajihusisha kikamilifu na suala zima la utafutaji na uchimbaji wa madini. Lazima tuwe wadau wa karibu sana katika utajiri wa nchi yetu. *(Makofi)*

Niseme tu hapa Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina utajiri mkubwa sana wa madini. Kwa taarifa tu za utafiti uliofanywa, mkienda hapa Ofisi yetu ya Madini hapa, ukiomba wakuonyeshe *theological data* iliyopo kwa nchi nzima, utasema kweli tunachofanya sasa hivi ni kidogo mno. Lakini narudia kwamba Watanzania hatuwezi kuendelea kila siku tunasema, tuna *potential* nzuri sana. Hatuwezi kuishi kwa kula *potential.* Madini haya lazima tuyatafute kokote yalipo, tuyapate, tuyachimbue, tuyasafishe, tuya-*process* na kisha tuweze kuyauza na tutumie mafao yanayotokana na mauzo hayo kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu na watu wake.

Sasa ili tuongeze jitihada zetu za kuweka mazingira mazuri, Serikali imeshaanza na itaendelea kufanya hivyo. Lakini madini yaliyopo siyo madini ya dhahabu peke yake au almasi au vito, yapo madini mengi sana, madini ya vyuma, mkaa wa mawe na *odium,* unaweza kusema *uranium* na mengine yote

mpaka kule maeneo ambayo yana madini mengi tunayafahamu lakini kwa leo mimi nasema tunaboresha maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mrahaba unalipwa na Kampuni au na mtu anayechimbua madini bila ya kujali kana kwamba yeye anapata faida. Tunachukua ushauri wa Wabunge kwamba *you know,* labda Serikali ingelifanya utafiti tuone viwango vya *royalties* mrahaba katika nchi zingine ikoje na Waziri wa Nishati na Madini nakumbuka *last time* aliahidi kufanya hivyo. Naamini hilo litatekelezwa.

Lakini niseme viwango vya mrahaba vinavyotolewa na Tanzania ni vya ushindani sana katika ukanda wetu hapa. Hilo mimi nafahamu. Lakini kwa sababu nimepewa hiyo *narrow function* ya kuwasilisha haya, nawaachia wahusika wakati muafaka kuweza kuyatoa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yale ya kusema *or vetically below the ground within horizontal boundaries* hayakusudiwi kabisa kwamba sasa hivi tunataka kuwashughulikia wachimbaji wadogo wadogo, Mererani au mahali pengine hapana. Kwa sababu haya yana utaratibu.

Unapewa eneo la mita 50 kwa 50. Tunachotaka kusema ni kwamba haiwezekani eti ukichimba tu *vertically* hivi hivi unaenda tu hivi hivi. Tunachosema ni kwamba wewe unaruhusiwa kabisa, ukaenda *vertically* na *horizontally* lakini usivuke mipaka halali uliyopewa. Wewe leseni yako ina-*co-ordinate* ile mipaka inaonyesha kabisa hata ukiwa chini kule ukiwa juu utajua kabisa *co-ordinate* hii inaishia hapa.

Lakini unakuta wengine wana mchezo wa ku-*in crock* kwenye maeneo mengine. Tunasema ile itakuwa ni kuvunja Sheria. Mheshimiwa Dr. Slaa aligusia hili suala la kufutiwa leseni za *Primary Prospecting Licence* na *Mining Licence, again* ni mchezo wa kuwaumiza wadogo, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunaweka utaratibu nzuri tu na kwa wachimbaji wakubwa, naomba tu Bunge lako kwa sababu ya muda, nitaje tu vifungu husika kwenye Sheria ya Madini. Sheria ya Madini ambayo ina-*govern* haya utaikuta kwenye ibara ya 57, *sorry* kifungu cha 57 cha Sheria ya Madini kifungu cha (ii) *the Minister shall not suspend,* amepewa *power* ya ku-*suspend* na ku-*cancel* lakini kabla ya kufanya hivyo lazima amtendee haki mwenye leseni na ndiyo maana tunasema na Kamishna naye wa Madini afanye hivyo hivyo, mpe ilani mhusika nakusudia kufuta au kusitisha leseni yako, kwa sababu zifuatazo:-

Ninakupa siku fulani, uweze kuwa umerekebisha tabia yako hiyo. Sasa hii ni utaratibu nzuri tu na kama akifuta au kusitisha na wewe huridhiki tunasema, kata rufaa kwa Waziri ili suala hilo liende likashughulikiwe. *Environment* (mazingira) kama kuna sheria kali ni hii Sheria ya Madini. Ukiisoma kwenye kifungu cha 10, kifungu kidogo cha (ii) na kifungu cha 47 kifungu kidogo cha (ii) utayakuta haya ambayo Mheshimiwa Dr. Slaa alikuwa anasema, *environmental impact assessment* lazima iwekwe na hiyo lazima iwe ni sehemu ya *mining plan* unayowasilisha ukiiombea leseni ya kuchimba madini. Hilo liko *covered very well* na hakuna wasiwasi na hiyo.

Waheshimiwa Wabunge mnapokwenda kutembelea migodi hiyo angalieni wanavyofanya ni kwa sababu sheria ndivyo inavyowataka. Tuna matatizo tu na hawa wachimbaji wadogo kwa suala hili la kuchafua mazingira kwa kuchimba mashimo halafu wanayaacha lakini hilo litaendelea kushughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Halinga ameongea kwa uchungu sana kuhusu fidia. Kifungu cha 96 wenye *surface right,* ukishakubali kwamba madini ni mali ya umma na ardhi ni mali ya umma umepewa tu kutumia, tunachosema wewe unayetafuta madini endapo katika eneo ulilopewa utaharibu mali ya mtu uliyemkuta pale kama vile mazao yake, nyumba na nini sheria hii inasema ulipe fidia na ndiyo yote haya yamekuwa yanatokea.

Ndiyo, madini haya yamekuwepo tangu shetani alipokuwa mtoto mdogo na yataendelea kuwepo lakini narudia tena hatuwezi kuendelea kusema kwamba *potential, potential* na Watanzania wanaojihusisha na utafutaji na uchimbaji wa madini hawa wachimbaji wadogo wadogo na hawa wa kati wamefanya kazi

nzuri kwa sababu hawa ndio wamekuwa wakionyesha njia kwamba hapa yapo madini na watu wanakwenda kuangalia na hatimaye kweli ukifanya utafiti yanapatikana.

Lakini tunasema basi kwa sababu wao wanachimba kwa kutumia zana hizi duni unaya-*scratch* tu madini huyafikii tulisikia juzi hapa tukielezwa na uongozi wa Kahama Mining sasa hivi wako kilometa karibu moja na kitu na wanakusudia kwenda kilometa mbili na nusu chini ya ardhi.

Sasa hiyo hata ukisema babu yangu Mzee Mwinula Chenge aligundua yale madini hangeweza kabisa hata angetambika namna gani kwenda kuyafikia kule chini yaliko sasa hivi. Tunashukuru katika kujenga mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji na kuweza kufika hapa tulipofika na tutaendelea kufanya hivyo kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo ya Bima kwa Wabunge tumesikia ni wazo zuri sana Mheshimiwa Isingo. Lakini Mbunge unapokufa kabla ya kupokea mafao yako Kifungu cha 22 cha Sheria ya *Political Service Retirement Benefits* kinasema ni nini kitokee kwa familia yako. Kwa hiyo, hilo sio tatizo kwa sasa lakini suala la Bima nadhani tutaendelea kulizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba radhi kama sikuweza kuwajibu Waheshimiwa Wabunge wote hoja zao nzuri walizozitoa lakini tutaendelea kufafanua na kuwapa majibu pale inapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana pia kupitia kwako nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na kwa kusema hivyo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2003**
***(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) (Bill 2003)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nilitaka kuwaambia tu Muswada huu una vifungu viwili tu, kifungu cha kwanza na cha pili, tunaendelea kwa utaratibu huo.

Kifungu cha 1

*(Kifungu Kilichotajwa hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nifanye marekebisho kwenye hii orodha ya marekebisho. Ukurasa wa kwanza (a) kwenye sheria maneno yanayosema *commencement of certain amendments* sasa hapo tatu tunasema, mstari wa pili kutoka chini sasa inasema *come into operation on the first day of May, 2004.* Napendekeza neno mwezi *May* lifutwe na badala yake tuweke *July.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*, tumeiona lakini Makatibu hapa wanasema hicho ni kifungu kipya cha tatu cha Muswada tunachohoji sasa ni cha pili.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sawasawa!

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kuna vifungu vitatu.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 3

**MWENYEKITI:** Sasa *AG* unaweza kutoa maelezo yako au ulishamaliza?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hilo. Kama nilivyoeleza awali napendekeza neno *May* lisomeke *July* ili tujipange vizuri katika kushughulikia mafao ya viongozi hawa.

Kwa ruksa yako kwa sababu baada ya hapo tunakwenda moja kwa moja kwenye *schedule,* kwenye kifungu kipya cha 287(a) mstari wa saba kutoka chini neno personal naomba tulifute tu ibaki *violence.*

*(Kifungu Kilichotajwa hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja Mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2003 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2), Bill 2003)* na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Naomba taarifa hii ikubaliwe

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndipo tumefikia mwisho wa shughuli za leo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.39 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa*
*Tarehe 13 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*